

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA NNE

Kikao cha Tisa – Tarehe 26 Juni, 2006

(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE JUMA J. AKUKWETI)

Hotuba ya Bajeti ya Waziri Mkuu, kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE - MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:-

Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala Kuhusu Utekelezaji wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka wa Fedha uliopita pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka 2006/2007.

MHE. DR. WILLBOD P. SLAA (K.n.y. HAMAD R. MOHAMED) - MSEMADI WA UPINZANI KWA OFISI YA WAZIRI MKUU:-

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Kuhusu Hotuba ya Bajeti ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni kadhaa. Naona Waheshimiwa Wabunge wamekuwa na Utamaduni mpya sasa wa kuleta majina mengi tu ya wageni wetu. Naomba sana ili tusiingiliane sana na kipindi cha maswali, basi niwatangaze mara baada ya kipindi cha maswali.

Waheshimiwa Wabunge, ila ninalo tangazo na ni kawaida yangu kwamba yakinoteka matukio mazuri tu kwa wenzetu Waheshimiwa Wabunge ni vizuri niweze kuwafahamisha. Nimearifiwa na Chama cha Mapinduzi kwamba jana Halmashauri Kuu ya Chama hicho ilifanya uteuzi wa uongozi mpya ndani ya Sekretarieti ya Chama na kwa kuwa wanen kati ya hao walioteuliwa au waliochaguliwa na Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM ni Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili nilikuwa naomba niweze kuwatambua kwa sababu ni wenzetu humu. Ninaviomba Vyama vingine inapotokea hivyo basi watuarifu hatutasita kuwatangaza. (*Makofi*)

Wa kwanza ni Mheshimiwa Yusuf Rajab Makamba, Mbunge wa Kuteuliwa, ambaye amechaguliwa na NEC kuwa Katibu Mkuu wa CCM. Mwingine ni Mbunge wa Siha Mheshimiwa Aggrey Mwanri, huyu sasa Waheshimiwa Wabunge, ndiyo Katibu Mwenezi wa Taifa wa Chama cha Mapinduzi.

Waheshimiwa Wabunge, mwingine ni Mbunge wa Igunga, Mheshimiwa Rostam Aziz huyu sasa ndiyo Mweka Hazina wa Chama cha Mapinduzi. Halafu upande wa Idara wenyewe wanaita *Organization* ameteuliwa Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe. Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro ameteuliwa kuwa ni Katibu wa Masuala ya Mambo ya Nje katika Chama cha Mapinduzi. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyota wito kwa wenzetu wa Vyama vyote vingine nadhani ni vizuri tuipongeze CCM kwa kutambua Hazina kubwa ya uwezo uliomo ndani ya Bunge letu hili. Tunaomba Vyama vyote vingine vinapotaka kupata watu madhubuti wa kuendesha mambo yao waangalie ndani ya Bunge hili. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

MASWALI NA MAJIBU

Na. 78

Utekelezaji wa Sheria ya The Parliamentary Services Commission 1997

MHE. MOHAMED R. ABDALLAH aliuliza:-

Kwa kuwa Bunge lilipitisha Sheria ya “*The Parliamentary Services Commission Act*” ya 11, 12 (1) na (3) inatoa madaraka kwa Bunge kuwa na Bajeti yake na kuisimamia na kwa kuwa mahitaji ya vifungu hivyo hayatekelezwi hivi sasa kama inavyotakiwa na hivyo sheria kutekelezwa bila ujumla wake:-

- (a) Je, ni nini sababu inayosababisha sheria hiyo isitekelezwe kwa ujumla wake?

- (b) Je kwa nini Bunge lisiwe na *Vote* zake na kuzisimamia lenyewe kama ilivyo kwa Wizara za Serikali?

NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU(MHE. DR. LUKA J. SIYAME) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkoo, naomba kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mbunge wa Jimbo la Pangani, kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mwaka 1997, Bunge lako Tukufu lilipitisha Sheria ya Tume ya Huduma za Bunge, yaani “*The Parliamentary Services Commission Act, 1997 (Act No. 14 of 1997)*” ambayo pamoja na mambo mengine, imeweka utaratibu wa kushughulikia fungu la fedha kwa ajili ya kikidhi mahitaji mbalimbali ya Bunge. Katika Sheria hiyo, kifungu cha 11 kinatamka bayana kuwa, fedha zinazohitajika kwa shughuli za Bunge zitalipwa na Hazina ikiwa makisio yake yamepitishwa na Bunge na kuwa fedha hizo zitatoka katika Mfuko Mkoo wa Serikali (*i.e. Consolidated Fund*). Aidha, kifungu cha 12(1), (2) na (3) kimetamka hatua mbalimbali za kuzingatiwa wakati wa kutayarisha Bajeti ya Bunge hadi kuidhinishwa na Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, mafupi, naomba sasa kwa niaba ya Mhesimiwa Waziri Mkoo, kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mbunge wa Pangani, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kwa mujibu wa Sheria Na. 14 ya mwaka 1997, utaratibu unaotumika kuandaa Bajeti ya Ofisi ya Bunge unazingatia maelekezo ya Sheria hiyo kama nilivyobainisha katika maelezo ya ufanuzi na Mheshimiwa Waziri Mkoo ndiye mwenye dhamana ya kuwasilisha makisio ya Bajeti hiyo kwenye Baraza la Mawaziri na hatimaye hapa Bungeni ili kuidhinishwa. Utaratibu huu ndio unaotumika kwa baadhi nchi za Jumuiya ya Madola ambazo zinatumia Mfumo uitwao *Westminster*. Mionganoni mwa nchi hizo ni pamoja na Australia, India, Jamaica na Malaysia.

(b) Bunge lina fungu lake kama ilivyo Wizara na Taasisi nyingine na linapewa fedha zinazohitajika kutoka katika Mfuko Mkoo wa Serikali yaani *Consolidated Fund* kupitia Fungu (*Vote*) 42. Pia Mahakama ni Mhimili wa Dola kama ilivyo Bunge na lenyewe kwa mfumo unaotumika hivi sasa inapewa fedha kutoka Mfuko Mkoo wa Serikali kupitia Fungu 40.

Mheshimiwa Spika, mfumo huu unalenga zaidi katika mgawanyo wa madaraka na majukumu kwa mihimili ya Dola iliyopo kama ilivyofafanuliwa ndani ya Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977.

MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sheria hii inatokana na Katiba ambayo ipo kwenye Cap.2. Mheshimiwa Spika, naomba ninukuu kidogo anasema: “*This Act shall be read as one with the Constitution of the United Republic of Tanzania.*” Kwa maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri na procedure zote kwa ajili ya gharama za kuendeshea Bunge kama alivyoeleza. Mimi naamini kwamba utaratibu ule hauko wazi kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri kama vile tunavyopitisha bajeti za Wizara. Tunapitisha tu kifungu cha Bunge ili kupitisha gharama za Bunge. Hilo moja.

La pili, sheria pia inatambua kuwepo kwa Waziri ambapo inasema: “*the Minister responsible for Parliamentary Affairs.*”

Mheshimiwa Spika, naomba niulize Waziri analisaidiaje Bunge katika kupanga na kuratibu shughuli za mafungu ya fedha kwa kuendeshea Bunge wakati sisi hatuoni kama kuna dalili hizo za Waziri kulisaidia Bunge katika shughuli zake za kila siku? Ahsante sana. (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. JUMA J. AKUKWETI): Mheshimiwa Spika, kama tulivyojibu kwenye swalii la msingi au jibu letu la msingi kuna mihimili mitatu ambayo yote inafanya kazi katika nchi hii moja. Kila mhimili unajitegemea katika masuala yake. Sasa inapofika wakati wa fedha kila mhimili unapanga Bajeti yake na baada ya kupanga Bajeti yake inapelekwa kule ambako inaweza kutafutiwa fedha na kwa hivi sasa ni Hazina na Hazina ndiyo baada ya kujua fedha ziko kiasi gani katika Taifa letu inagawa sasa zipi ziende wapi kutokana kwanza na mahitaji. Lakini pia mapato ya Taifa letu na kazi ya Waziri ni kuhakikisha hiyo *process* yenewe.

Mheshimiwa Spika, lakini Mheshimiwa Mbunge nadhani anafahamu katika sheria yetu kifungu 13 kinasema ifuatavyo na naomba nikisome moja kwa moja. Kifungu cha 13 katika sheria ya Bunge ambacho kina *guide* mambo ya Bunge kinasema hivi: “*The Commission shall from time to time prepare and recommend to the President the rates of salaries, allowances and other recommendations to be paid to Members of Parliament.*” Nadhani utaratibu huu ni mzuri kwamba Bunge lenyewe baada ya mahitaji yake linapeleka moja kwa moja kwa Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Rais anatumia utaratibu wake ili kuhakikisha anakubali au anakataa yale maombi ya Bunge. Mimi nadhani huu ni utaratibu mzuri ili nguzo hizi tatu zisiweze kugongana, lakini wote tutatafuta fedha kwenye Mfuko mmoja kwa ajili ya Taifa letu. (*Makofi*)

MHE KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii la nyongeza na wakati huo huo nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Aggrey Mwanri kwa kuwa Katibu Mwenezi wa Chama, kweli kimepata mwenezi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swalii langu ni dogo tu. Kwa kuwa matamkwa ya swalii la msingi ni matamkwa ya Kisheria na matamkwa haya yameonekana kwamba hayafanyiki. Je, Serikali haioni kwamba imefika wakati muafaka Bunge liwe huru zaidi na kujipangia *vote* yake na Bajeti yake na kuisimamia yenewe ili kuepuka kuwekwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na chini ya Wizara ya Fedha?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. JUMA J. AKUKWETI): Mheshimiwa Spika, nionavyo mimi utaratibu huu unafuata kabisa jinsi sheria inavyotaka. Mimi naomba niseme hivi Mheshimiwa Kabwe Zitto, kama nia ni kwamba kila nguzo ijipangie yenyewe basi kuna hatari ya nguzo hii ambayo ina mamlaka makubwa katika nchi yetu ikajipangia marupurupu makubwa kuliko hata kutoangalia nguzo zingine. Utaratibu unaotumika sasa ndiyo unaojenga haki ya mgawanyo sawasawa katika Taifa letu. Kuhakikisha Mahakama inapata kiasi chake ili isikwame na kuhakikisha kwamba Bunge linapata kiasi chake ili lisikwame na *Executive* inapata kiasi chake ili isikwame.

Mheshimiwa Spika, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Kabwe Zitto, kwamba kwa utaratibu huu mpaka sasa Bunge halijawahi kukwama kufanya kazi kwa sababu *Executive* haikutoa fedha. Na yeze tayari naweza kum-*challenge* aseme ni lini Bunge limeshindwa kufanya kazi kwa kukosa fedha kutoka Hazina. (*Makofî*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naona tuendelee kwa sababu suala hili litashughulikiwa kwa namna ambayo ni tofauti kidogo. (*Makofî*)

Na. 79

Hospitali ya Mkoa wa Kagera

MHE. ELIZABETH N. BATENGA aliuliza:-

Kwa kuwa, hospitali ya Mkoa wa Kagera ni moja kati ya hospitali nzuri sana hapa nchini hasa baada ya kufanyiwa ukarabati miaka michache iliyopita:-

- (a) Je, hospitali hiyo inastahili kuwa na watumishi wangapi yaani kwa upande wa Madaktari, Matabibu na Wauguzi?
- (b) Je, kwa sasa hospitali hiyo ina watumishi wangapi?
- (c) Kama ni wachache hawatoshelezi. Je, ni kwa nini?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Elizabeth Nkunda Batenga, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Mkoa wa Kagera inastahili kuwa na jumla ya watumishi, 229 kama ifuatavyo:-

% Utawala	34	
% Afya ya Kinga		6
% Huduma ya Tiba	33	
% Huduma ya Uuguzi	130	
% Idara ya Famasia		5
% Idara ya Maabara		11
% Idara ya Afya ya Mazingira	4	
% Idara ya Radiologia		4
% Fisiotherapia		2
Jumla	229	

Mheshimiwa Spika, kati ya watumishi 229, hospitali inastahili kuwa na jumla ya Madaktari 31 na wauguzi 130 kwa mujibu wa Sera ya Afya. Na pia kwa mujibu wa Sera ya Afya hiyo hiyo Matabibu hawahitajiki katika Hospitali za Mikoa.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa sasa hospitali ya Mkoa wa Kagera ina watumishi 251. Idadi hii ya watumishi inajumuisha na wale watumishi ambao hawawahudumii wagonjwa moja kwa moja. Hospitali ya Mkoa wa Kagera ina upungufu wa Madaktari Bingwa 5, Madaktari wa kawaida mmoja (1) na Madaktari wasaidizi watati (3). Idadi ya watumishi waliopo inaonyesha kuwa ni kubwa ikilinganishwa na idadi ya watumishi wanaohitajika kwa mujibu wa Sera ya Afya. Hii ni kwa sababu walijiriwa wahudumu Wauguzi wengi ili kusaidiana na Madaktari wachache waliopo katika kupunguza uhaba wa watumishi uliopo.

(c) Mheshimiwa Spika, tatizo la upungufu wa Madaktari uliopo unatokana na uhaba mkubwa wataalam hasa Madaktari Bingwa na Madaktari wa kawaida hapa nchini. Aidha, hata wataalam wachache waliopo nchini baadhi yao hawapendi kufanya kazi katika Mikoa yenye mazingira magumu ya kazi ukiwemo Mkoa wa Kagera.

Na. 80

Ukosefu wa Hospitali Buchosa

MHE. SAMUEL M. CHITALILO aliuliza:-

Kwa kuwa katika Jimbo la Buchosa hakuna hospitali kubwa na yenye vifaa vinavyostahili na hivyo wananchi hulazimika kwenda kutibiwa Sengerema Mjini, hali inayosababisha vifo vya akina mama wengi wajawazito na watu wasio na uwezo wa kusafiri kwenda Sengerema na kwa kuwa Sensa ya hivi karibuni ilionyesha kuwa idadi ya watu wa Buchosa ni zaidi ya laki mbili na kwamba, wananchi hao nao wana haki kama walivyo wa maeneo mengine:-

- (a) Je, Serikali ipo tayari kuimarisha Vituo vya Afya vilivyopo pamoja na kuongeza waganga?

- (b) Je, Serikali ipo tayari kujenga hospitali kubwa kulingana na idadi ya watu waliopo?
- (c) Je, Serikali itakuwa tayari kuweka *Radio calls* katika Vituo vya Afya vya Nyehunge, Rugasa, Nyamisi, Kakobe na Mwangika?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Samuel Mclele Chitalilo, Mbunge wa Buchosa, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Jimbo la Buchosa lina Vituo vya Afya vinne ambavyo ni Nyehunge, Nyamisi, Kakobe na Mwangika. Vituo hivi vimeimarishwa na vinatoa huduma za kulaza wagonjwa (*in patient*) na huduma za wagonjwa wa nje (*out patient*) pamoja na huduma za Afya na Uzazi kwa mama na mtoto. Kituo cha Kakobe, mbali na huduma hizi kinatoa pia huduma ya upasuaji mkubwa na upasuaji mdogo. Vituo vingine vya Kakobe, Nyamisi na Mwangika vina uwezo wa kulaza wagonjwa zaidi ya 80. Jumla ya watumishi waliopo katika Vituo hivi ni 47 akiwemo Daktari Msaidizi mmoja (1), Wauguzi kumi na mbili (12), Tabibu wa nane (8), Tabibu Msaidizi mmoja (1). Waliobaki ni watumishi Wasaidizi (*Supporting Staff*) ambao jumla yao ni 25. Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema iko katika mpango wa kukarabati Vituo vya Afya ulio chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikai za Mitaa. Kwa kipindi cha mwaka 2005/2006 Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema ilitengewa kiasi cha sh.539,000,000/= katika mgao wa pili wa Wilaya 21 kati ya Wilaya 46 ambazo zilitegemewa kupewa fedha kwa mwaka huo 2005/2006. Fedha hizo zimetengwa kwa mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango wa kuboresha huduma katika Vituo vya Afya na Zahanati Jimboni Buchosa kwa kuendelea kutoa mafunzo kwa watoa huduma za Afya Vituoni. Mwaka 2006/2007 jumla ya watoa huduma 212 watapatiwa mafunzo mbalimbali. Aidha, katika Jimbo la Buchosa Serikali ina mpango wa kukabati majengo na nyumba za watumishi kwa awamu mbalimbali katika kipindi cha 2006/2007, Vituo vya Afya 2 na zahanati 7. Serikali pia ina mpango wa kuboresha upatikanaji wa dawa, kuajiri Waganga wenye ujuzi wa kila kada kufuata ikama na kuwaendeleza kitaaluma Waganga na Wauguzi walioko kazini.

(b) Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema inayo Vituo vya Afya saba na Zahanati 51. Jimbo la Buchosa lina Vituo vya Afya vipatavyo vinne (4) na zahanati 20. Kati ya Zahanati hizo, zahanati 17 zinamilikiwa na Serikali na 3 zinamilikiwa na Shirika la Dini la *African Inland Church of Tanzania (AICT)*. Kulingana na Sera ya Afya ya Taifa kila Kituo cha Afya kinao uwezo wa kuhudumia wananchi zaidi ya hamsini elfu. Jimbo la Buchosa linao wananchi wapatao laki mbili na kuna Vituo vya Afya vinne ambavyo vinakidhi haja ya tiba kwa wananchi wa Jimbo hilo. Hivyo, Serikali haina mpango wa kujenga Hospitali kubwa katika Jimbo hilo kwa sababu Wilaya

ya Sengerema inayo Hospitali teule ya Wilaya ambayo inatumika kama Hospitali ya Rufaa kwa Vituo vya Afya. (*Makofi*)

(c) Mheshimiwa Spika, Vituo vyote vya Afya vilivyopo katika Jimbo la Buchosa havina *Radio Calls*. Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema ina mpango wa kuweka *Radio Calls* katika Vituo vyote kwa kuanzia na Vituo vya Kome na Mwangika katika Bajeti yake ya mwaka 2007/2008.

MHE. SAMUEL M. CHITALILO: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwanza, kabla sijaauliza swali napenda kusahihisha jina langu mimi ni Samuel Mchele Chitalilo siyo Samuel Mchale Chitalilo. Naomba kumuuliza Naibu Waziri, kwamba watu wa Buchosa ni zaidi ya laki mbili, ukilinganisha na Wilaya nyingine kama Pangani isiyokuwa na watu zaidi ya watu 40,000 ingawa ina hospitali ya Wilaya. Je, Buchosa kuna ubaya gani kuweka hospitali kubwa yenye hadhi ya Wilaya?

NAIBU WA WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, kama nilivyo sema katika jibu langu la msingi kiutaratibu kila Wilaya ina hospitali ya Serikali moja. Lakini hata hivyo, Serikali iko mbioni katika kuimarisha huduma za afya. Kwa hiyo, suala lake tutaangalia kulingana na unyeti wa Jimbo lake.

SPIKA: Mheshimwia Waziri wa Afya majibu ya ziada.

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili nitoe majibu ya ziada zaidi ya majibu mazuri aliyotoa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji. Ningombaa nimfahamishe Mheshimiwa Samuel Chitalilo kwamba kigezo cha kujenga hospitali ni katika mfumo mzima wa maeneo yote ya utawala hatuchukui idadi ya watu peke yake. Kwa sababu hatutaishia hapo tutasema kwamba kwa nini kusiwe na Ma-DC mawili kwa sababu kuna watu wengi kuliko Pangani. Sasa hivi tunachojitahidi kusema kweli ni kwamba tungependa kila Wilaya iwe na hospitali na tuziimarishe na sasa hivi kuna Wilaya mpya ndiyo tunaelekeza nguvu kusudi ziwe na hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningemshauri Mbunge wa Buchosa kwamba hatutasikitika kama wakiweza kuanza kujenga hospitali tutawasaidia. Majirani zao Bukombe wamejenga hospitali ambayo tunataka kuifungua mwezi ujao na ningependa kuwashukuru kwa hilo, waige mfano huo. Ahsante sana. (*Makofi*)

Na. 81

Kilimo cha Mazao ya Chakula na Biashara

MHE. LUCAS L. SELELII aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wengi katika Mikoa ya Magharibi (Tabora, Kigoma na Rukwa) pamoja na Mikoa ya Kanda ya Ziwa (Mwanza, Shinyanga, Kagera na Mara) ni wakulima stadi wa mazao ya chakula na biashara:-

- (a) Je, ni kwa nini Mikoa hiyo inabaguliwa kupewa ruzuku ya mbolea?
- (b) Je, bei ya mbolea iliyotolewa ruzuku na Serikali ni kiasi gani?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucas Lumambo Selelii, Mbunge wa Nzega, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kutoa ruzuku ya mbolea ulianza mwaka 2003/2004 kwa kulenga zaidi ya Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kwa kuzingatia uchache wa fedha na upatikanaji mzuri wa mvua katika Mikoa hiyo.

Kutokana na maombi ya wananchi wengi kupitia kwa Waheshimiwa Wabunge na kutokana na mafanikio yaliyopatikana katika miaka ya 2003/2004 na 2004/2005, Serikali inaendelea kutoa ruzuku ya mbolea kwa nchi nzima na madawa ya korosho kwa mikoa inayolima korosho.

Napenda kumhakikisha Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali haibgui Mkoo wowote katika suala la kilimo na pale ambapo hatua za makusudi zinachukulia, inafanywa hivyo kwa faida ya Taifa zima.

Mheshimiwa Spika, Mikoa ya Kanda ya Ziwa ni miongoni mwa Mikoa ilioyoingizwa katika utaratibu wa kupatiwa mbolea yenye ruzuku katika mwaka wa 2004/2005. Ili kuhakikisha kuwa Mikoa hiyo inapata mbolea, Serikali ilitengea Mikoa ya Mwanza na Mara jumla ya tani 60 kupitia katika kituo cha kupokelea mbolea cha Mwanza na Mikoa ya Tabora na Shinyanga ilitengewa jumla ya tani 19,521 kupitia kituo cha Tabora.

Mheshimiwa Spika, baada ya kufanya tathmini katika mwaka wa 2005/2006, Serikali iliamua kuongeza idadi ya vituo vya kupokelea mbolea kutoka 14 hadi 22 ambapo mgao wa mbolea yenye ruzuku ulifanywa, Mkoo wa Mwanza ilitengewa jumla ya tani 400, Mkoo wa Shinyanga tani 400, Mkoo wa Kagera tani 300 na Mkoo wa Mara tani 460.

Mheshimiwa Spika, uzoefu wa miaka mitatu ya utekelezaji wa mpango wa ruzuku ya mbolea umeonyesha kwamba kuna mapungufu ya usimamiaji hasa katika ngazi za Mikoa na Wilaya. Usimamizi wa karibu wa Kamati za Mikoa na Wilaya unahitajika sana kuhakikisha kuwa mbolea inasafirishwa hadi vituo vikuu vya usambazaji vya Mikoa, Wilaya na kwenye maduka. Serikali inaendelea kuchukua hatua za kuimarisha utaratibu wa usimamizi kwa kutumia Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri za Wilaya na Miji.

(b) Mheshimiwa Spika, bei za mbolea zilizopangwa na Serikali ziliwu ni shilingi 17,000/= kwa mfuko wa kilo 50 kwa mbolea za aina ya *DAP*, *UREA*, *CAN* na *TSP* katika Mikoa yote ya Tanzania Bara. Kwa mfuko wa kilo 50 mbolea ya *NPK* 25:5:5 iliuzwa kati ya shilingi 22,675/= na 23,000/=, *NKP* 20:10:10 iliuzwa kati ya shilingi 24,075/= na 24450 na *NPK* 10:18:24 iliuzwa kati ya shilingi 25,675/= na 26,050/= katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa Spika, mtetezi wa kwanza wa wakulima ni Mheshimiwa Mbunge wake. Kwa hiyo, Serikali itahakikisha Waheshimiwa Wabunge wanauelewa vizuri utaratibu wa usambazaji wa mbolea ili waweze kuhoji pale yanapotokea mapungufu na udanganyifu katika bei iliyopangwa.

MHE. LUCAS L. SELELII: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa usambazaji wa mbolea huo hutokea ukachelewa sana kinyume na msimu katika maeneo mengi hasa ya Kanda ya Ziwa pamoja na Kanda ya Magharibi. Je, haoni kwamba ni mojawapo ya mapungufu makubwa ambayo yanababisha mkulima kuchelewa kutumia mbolea hiyo na hivyo kupata bei ya kulanguliwa kutoka kwa wafanyabiashara? Lakini la pili, Mkoa wa Tabora ni mkoa unaongoza kwa zao la biashara hasa tumbaku na tumbaku hutumia mbolea zaidi hasa *NPK* haoini kwa mkoa wa Tabora ambao unaongoza kwa zao la tumbaku akaongeza mgao hivyo kuondokana na wakulima kukopeshwa na wafanyabiashara kwa wanunuizi wa tumbaku kufanya bei ya tumbaku kuwa chini na kuwanufaisha wafanyabiashara hao? (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA): Mheshimiwa Spika, kuhusu mbolea kuchelewa inatokana na mifumo ya usafirishaji tuliyonayo. Hata hivyo Serikali inafanya bidii sasa kuhakikisha kwamba maandalizi yote yanafanya ili pembejeo zote ikiwa ni pamoja na mbolea ziweze kuwafikia wananchi kabla ya msimu kuanza.

Pia kuhusu mbolea ya *NPK* naomba kumhakikishia Mheshimiwa Selefii kwamba Serikali inatambua mapungufu tuliyonayo hasa ya mbolea na kwa kweli bado hatujatosheleza mahitaji, lakini tumejaribu kuongeza mbolea katika kipindi cha miaka mitatu mara tatu. Tulipoanza hii mbolea ya ruzuku tulianza na Shs. 7 bilioni sasa katika miaka mitatu tumeongeza mara tatu tunatarajia kufikia 21 bilioni katika msimu huu. .

Mheshimiwa Spika, Serikali inafanya bidii.

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniruhusu kuuliza suala moja la nyongeza.

Je, Serikali inafuutilia vipi kuhakikisha kwamba bei ya mbolea iliyotolewa ruzuku na Serikali ndio bei ambayo wakulima wanauziwa?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA NAUSHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA): Mheshimiwa Spika, Serikali inazo Kamati za Kusimamia Mbolea ya Ruzuku katika Mikoa. Kwa hivyo kama nilivyojibu katika majibu yangu ya swali la msingi tunaimarisha usimamizi kupitia Sekretariat za Mikoa, Halmashauri zote za Wilaya na Manispaa kuhakikisha kwamba hakuna watu wanajiingiza hapo katikati na kumwibia mkulima kwa kupanga bei ambayo sio iliyopangwa.

Na. 82

Mishahara ya Wafanyakazi Hoteli za Kitalii

MHE. ALI KHAMIS SEIF aliuliza:-

Kwa kuwa ni wazi kuwa malipo ya wafanyakazi katika hoteli za kitalii kama Senonera ni madogo sana na kuwa kila mwananchi anatakiwa alipwe kwa mujibu wa kazi anazofanya:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha wafanyakazi wa hoteli za kitalii wanalipwa malipo yanayostahili?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba nitoe maelezo mafupi kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mbunge wa Mkoani. Kisheria, waajiri wote nchini wana uhuru wa kujipangia viwango vya mishahara ili mradi hawalipi chini ya kima cha chini kinachopangwa na Serikali. Hoteli nyingi za kitalii ikiwemo Hoteli ya Seronera hulipa mishahara ambayo si chini ya kima cha chini kilichopangwa. Pamoja na nyongeza inayotokana na *service charge* nyongeza hii ni motisha, hutokana na asilimia 5 ya mauzo na hugawiwa kwa wafanyakazi wote.

Mheshimiwa Spika, uchunguzi uliofanywa hivi karibuni na maofisa wa Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana umegundua kuwa kwenye hoteli nyingi hazina Matawi ya Chama cha Wafanyakazi (CHODAWU). Hali hii inawapunguzia wafanyakazi nguvu ya kudai kutoka kwa waajiri wao mishahara bora na stahili nydingine ikiwemo mikataba ya hiari. Baada ya maelezo hayo mafupi napenda nijibu swali la Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mbunge wa Mkoani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha hali ya kipato cha wafanyakazi, Wizara kwa kushirikiana na wadau kama *Tourism Confederation of Tanzania (TCT)* na *Hotel Association of Tanzania (HAT)* na CHODAWU itaandaa mkutano wa pamoja ili kuyachambua kwa umakini matatizo haya na kuyatafutia ufumbuzi

MHE. ALI KHAMIS SEIF: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda nimwulize maswali mawili ya nyongeza.

Je, Wizara inaelewa kuwa katika hoteli hizi kazi zinazofanywa za aina moja baina ya Watanzania na wageni malipo wanapata zaidi wageni?

Pili, kama hali hiyo anaelewa Mheshimiwa Naibu Waziri atairekebisha vipi?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, katika hoteli zetu za kitalii kama zilivyo hoteli nyingine kuna baadhi ya kazi ambazo zinahitaji utaalamu na kazi hizi nyingi ni zile za uongozi kwa mfano *General Manager*, Meneja wa Vinywaji, Meneja wa Chakula vinahitaji utaalamu. Lakini kazi zile ambazo hazihitaji utaalamu hufanywa na wafanyakazi wa nchini kwetu. Hata hivyo kutokana na tatizo hilo Serikali yetu ikishirikiana na Serikali ya Ufaransa ina mpango wa kujenga Chuo cha kitalii mjini Dar es Salaam na kitaanza mafunzo mwaka 2008. Chuo hicho kitatoa mafunzo kwa ajili ya uongozi katika ngazi mbalimbali.

MHE. ALOYCE B. KIMARO: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali inatoa leseni kwa mahoteli madogo madogo ambayo Watanzania wana uwezo nayo lakini Serikali inatoa leseni kwa wageni. Je, Serikali ina mpango gani wa kusimamisha utoaji wa leseni za namna hiyo?

WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA: Mheshimiwa Spika, katika zama hizi ambazo tunapenda sana na kuhamasisha kwamba tuwe na watalii wengi ni vyema pia tukajua kwamba watalii wa aina mbalimbali wana mahitaji mbalimbali ya vyakula na huduma za hoteli. Kwa hivi pale ambapo tunaona kwamba hoteli itakayofunguliwa itakuwa na manufaa katika azma yetu ya kukuza utalii basi wanapewa leseni kwa kuzingatia utaratibu huo.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge nimeletewa hoja hapa kwamba Naibu Waziri wa Maliasili amevaa sare za Chama chake. Sasa !!! Ndiyo lazima nifafanue. Waheshimiwa mavazi ya humu Bungeni kwa Wanawake. Mbunge mwanamke akivaa suti yake na blauzi Spika aangalie rangi yake ile ya suti na blauzi. (*Makofi*)

Kwa hiyo, blauzi inaweza kuwa nyekundu inaweza kuwa ya kijani, ya bluu zote zinaruhusiwa. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

Upande wa Upinzani Mheshimiwa Grace Kiwelu, umesimama sana swali la nyongeza?

MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Katika majibu ya Naibu Waziri amesema kwamba wageni wanaokuja na kupewa ajira ni wale ambao ni Mameneja wa Vyakula, Vinywaji. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kutuambia wataalamu hao Tanzania hatuna na kwa nini tuajiri kutoka nje?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, Sheria ya Uwekezaji inatoa ruhusa kwa mtu anayeleta *investment* hapa nchini kuajiri watu ambao anawaamini na ndiyo orodha ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameitoa. Watu ambao wako kwenye Menejimenti.

Lakini pia ni vyema kuelewa kwamba hapa kati kati Chuo tulichokuwa nacho ambacho ni Chuo cha *National College of Tourism* na kabla ya hapo tulikuwa na Chuo Forodhani ilikuwa inatoa mafunzo *Lower cadre* hawa Ma-waiter na watu wa jikoni na kadhalika.

Kwenye Menejimenti tulikuwa hatuna chuo. Tulikuwa tunategemea Chuo cha Utalii ambacho kiko Nairobi. Mameneja ambao utawakuta ni wa Kitanzania kwenye mahoteli haya ni wale ambao walipelekwa zamani *Scholarship* Uingereza, ufaransa na Uswiss. Katikati hapa hatujapata kuwa na mafunzo ya Programu ya namna hiyo.

Kwa hiyo, tatizo hilo tunalo kwamba katika *Management Level Management* Mameneja hatunao wengi na waliopo utakuta mahoteli yote yamo humu wamewaaajiri. Kwa hiyo, ni vyema wawekezaji wanapokuja sheria inawaruhusu na sio dhambi kwa vile tunaruhusu uwekezaji kwenye nchi yetu. (*Makofi*)

Na 83

Hifadhi ya Taifa ya Ruaha

MHE. STEPHEN J. GALINOMA aliuliza:-

Kwa kuwa, hivi karibuni kazi ya kuweka lami katika barabara ya kutoka Iringa kwenda Hifadhi ya Taifa ya Ruaha imeanza baada ya mradi huo kusubiriwa kwa muda mrefu, lakini kazi hiyo sasa imesimama:-

Je, Serikali inaweza kueleza mustakabali wa mradi huo hasa ikizingatiwa kwamba, mkazo umewekwa ili kustawisha utalii katika Hifadhi za Taifa ikiwa ni pamoja na Hifadhi ya Taifa ya Ruaha?

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swalil Mheshimiwa Stephen J. Galinoma, Mbunge wa Kalenga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Iringa – Msembe, ni barabara ya Mkoa yenye urefu wa kilometra 104.63 na inaunganisha Manispaa ya Iringa na Hifadhi ya Taifa ya Ruaha. Barabara hiyo inahudumiwa na Wakala wa Barabara (*TANROADS*) Mkoa wa Iringa na ilifanyiwa matengenezo makubwa kwa kiwango cha changarawe chini ya ufadhilli wa Serikali ya Denmark kupitia Shirika lake la Maendeleo la *DANIDA* kuanzia mwaka 2001 hadi mwaka 2006. Sehemu ya barabara hiyo ya Mwangata – Njipanda na

Tosamaganga, kilometra 8.7, ilipangwa kujengwa kwa kiwango cha lami kwa jumla ya shilingi milioni 816.15 kupitia msaada huo.

Kazi za ujenzi zimekamilika kwa kiwango kikubwa (*Substantial Completion*) na hivi sasa sehemu hiyo ya barabara iko kwenye uangalizi wa Mkandarasi (*Defects Liability Period*) mpaka mwezi Desemba 2006.

Sehemu iliyobaki kati ya Njipanda na Tosamaganga na Msembe (kilometra 95.5) ambayo ipo katika hali nzuri kwa tabaka la changarawe, itaendelea kupata matengenezo ya kawaida na kuwekewa changarawe pale itakapohitajika ili iendelee kupitika wakati wote.

MHE. SAMEER I. LOTTO: Mheshimiwa Spika, barabara zetu zinawekewa lami. Lakini barabara nyingi lami yake inakuwa ina udhaifu na baada ya muda mfupi inaanza kutitia. Je, Serikali itatuhakikishia vipi kwamba barabara zikishawekewa lami zinadumu angalau kwa muda fulani na kama kuna kiwango cha muda ambaio inakuwa na *guarantee* kwa barabara ile. Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA): Mheshimiwa Spika, Serikali inapotengeneza barabara zake ni nia yake iweze kudumu kwa muda mrefu na hasa inapokuwa barabara ya lami.

Mheshimiwa Spika, lakini kama kuna barabara ambazo hazikudumu katika muda ule ambaio unategemewa, hutegemea na kiwango cha barabara ambayo ilikuwa imokusudiwa kwa sababu hata barabara za lami zina viwango tofauti. Kwa hiyo, hata muda wa kudumu kwa barabara zina tofautiana.

Lakini kama muda huo ndio uliodhamiriwa kwa kiwango cha lami barabara fulani haikuweza kutimilizwa kwa sababu ama ukosefu wa utaalamu kwa upande wa mkandarasi au sababu zingine zozote Serikali huwa inafuatilia. Kama barabara bado iko katika *defects liability period* basi mkandarasi hutakiwa kuitengeneza kwa gharama zake.

Lakini kubwa katika hilo kama tatizo ni la mkandarasi basi Serikali imekuwa ikifanya juhudhi kuhakikisha kwamba mkandarasi wanaoteuliwa wanafanya kazi ambayo ni bora. Lakini kama kweli anayo mifano halisi ya barabara ambayo anadhani imeharibika kabla ya muda wake basi tunaweza kuwasiliana tuone tunafanya nini lakini pale ambapo kwa kweli hakuna lingine la kufanya Serikali hurudia kutengeneza barabara hiyo.

Na. 84

Uwanja wa Ndege Moshi

MHE. LUCY F. OWENYA aliuliza:-

Kwa kuwa, katika dunia ya utandawazi miundombinu bora ni nyenzo kubwa katika kukuza uchumi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha Kiwanja cha Ndege cha Moshi, ambacho pamoja na shughuli nyingi za kibiashara ni kiungo muhimu kwa kuhudumia wagonjwa wanaopelekwa katika hospitali ya *KCMC* kutoka Mikoa mbalimbali nchini katika mpango wa *Flying Doctor Service*?

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI)
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Kwa kutambua umuhimu na mchango wa Kiwanja cha Ndege katika kuboresha na kuinua sekta ya utalii, kutoa huduma za kijamii (afya) na kwa maendeleo ya wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro na nchini kwa ujumla, Wizara inafanya yafuatayo ili kuimarisha Kiwanja cha Ndege cha Moshi.

Mamlaka ya Viwanja vya Ndege nchini hutumia wastani wa shilingi 80.0 milioni kwa mwaka kwa ajili ya gharama za kutunza na kuendesha kiwanja hiki kwa shughuli zifuatazo:-

- Kutengeneza na kukarabati miundombinu. Kwa mfano, kukata nyasi, kuzibua mitaro ya maji ya mvua na kuziba mashimo kwenye njia ya kurukia na kuegesha ndege na kufanya matengenezo madogo madogo ya majengo yaliyopo kiwanjani.
- Kulipa mishahara ya wafanyakazi, gharama za utawala na kuendeshea ofisi.
- Matengenezo ya magari pamoja na vifaa vya zimamoto

Mheshimiwa Spika, gharama ya ukarabati wa miundombinu kwa kiwango cha lami (*re-surfacing*) na kuboresha majengo inakadiriwa kuwa shilingi 3.65 bilioni. Kutohana na gharama ya ujenzi kuwa kubwa, Wizara inaendelea kutafuta fedha kutoka vyanzo mbalimali ili kukamilisha mradi huu muhimu. Aidha, Wizara imekiweka Kiwanja cha Moshi katika orodha ya viwanja vinavyotafutiwa fedha chini ya mpango wa miaka kumi na uendelezaji miundombinu nchini.

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri. Kwa kuwa uwanja wa Moshi ukizingatia uko *strategically position*, uko karibu na mipaka ya nchi na watalii wengi wamekuwa waki-fly direct kwenda Nairobi na wanapanda *shuttles* kuja Moshi na wamekuwa wakichukua muda mwingi zaidi ya masaa sita (6). Mheshimiwa Naibu Waziri, haoni umuhimu wa kuharakisha uwanja ule ili watalii waweze ku-fly direct pale Moshi Airport? (*Makofit*)

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):
Mheshimiwa Spika, napenda tu nimfahamishe Mheshimiwa Lucy Owenya, kwamba nakubaliana naye kwamba Kiwanja cha Moshi kiko *strategically* lakini viwanja vingi

strategically allocated kama vile Kigoma, Tabora na sehemu nyingine. Utalii upo sehemu nyingi lakini napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tuko mbioni kulifanya kazi kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi.

MHE. AHMED ALLY SALUM: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri tatizo hilo la Uwanja wa Ndege linafanana kabisa Uwanja wa Ndege ulioko katika Mkoa Shinyanga. Mkoa wa Shinyanga Uwanja wa Ndege wake ni barabara ya mchanga *runaway* yake sio ya lami na jengo lake kwa kweli ni la zamaani. Ukizingatia Mkoa wa Shinyanga kwa sasa hivi unaendelea kwa kasi kubwa. Ni lini Serikali itafikiria kujenga Uwanja huo wa Ndege katika Mkoa wa Shinyanga?

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI): Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda nichukue nafasi hii niwashukuru wananchi wa Shinyanga kwa kusaidia kwa kima kikubwa kuujenga Uwanja wa Ndege wa Ibadakuli, Shinyanga.

Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kesho tu tunayo nafasi ya kupitia Kiwanja cha Shinyanga na tunakwenda na Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum na Mbunge wa Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika jibu la msingi tuna viwanja vya ndege 23 tuna *airstrips* karibu 300. Kwa hiyo, tunafanya shughuli hizi kwa awamu kutokana na mapato tunayoyapata. Fedha zikipatikana za kutosha Mheshimiwa Mbunge hatuna sababu kwa nini tusikijenge vizuri Kiwanja cha Shinyanga kikachangia uchumi wan nchi hii. (*Makofit*)

Na. 85

Chuo cha Maendeleo ya Jamii Misungwi

Kwa kuwa, Chuo cha Maendeleo ya Jamii Misungwi kimekuwa na matatizo ya muda mrefu kama vile watumishi kutopandishwa vyeo, *OC* ambayo haitoshi kwa shughuli za Chuo, Chuo kutokuwa na vitendea kazi kama vile gari, pikipiki, nyumba zisitosha na zisizokidhi ubora kwa Walimu, na ukarabati mkubwa wa vyumba vya kujifunzia na kadhalika:-

Je, Serikali inafahamu matatizo hayo na inajiandaaje kuyatatua, na ni yepi yaliyotekeliza?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, naomba kumjibu Mheshimiwa Jacob Dalali Shibili, Mbunge wa Missungwi, kama ifuatavyo:-

Nakubaliana na Mheshimiwa Shibititi kwamba Chuo cha Maendeleo ya Jamii Misungwi kimekuwa kikikabiliwa na matatizo mbalimbali yaliyotajwa na kwamba Serikali inafahamu kuhusu hali hiyo. Kwa kutambua hii Wizara yangu inaendelea kuyapatia ufumbuzi matatizo haya hatua kwa hatua kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara imefanya uchambuzi wa kina ili kubaini watumishi ambao wamecheleweshwa kupanda daraja. Zoezi la kuwapandisha vyeo watumishi waliocheleweshwa kwa sasa limekamilishwa na limewasilishwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Katika zoezi hilo watumishi watatu (3) wa Chuo cha Missungwi kati ya sita (6) waliohusika na tatizo hili kwa wale wengine bado linashughulikiwa.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Chuo cha Maendeleo ya Jamii Missungwi kinapewa fedha za *Other Charges (OC)* ambazo fedha hizo ni kidogo, lakini hii ni kutokana na bajeti ya Wizara yangu ya T.shs. 8.4b/= ambayo bado ni finyu sana ukilinganisha na mahitaji halisi ya uendeshaji ambayo ni Tshs. 18.476b/=.

(c) Mheshimiwa Spika, kuhusu tatizo la usafiri na vitendea kazi, kati ya mwezi Aprili – Juni 2006 Wizara imenunua na kukabidhi gari jipya aina ya *Land Cruiser Hard Top* kwa ajili ya matumizi ya Chuo hicho. Aidha, kwa mwaka 2004/05 Chuo kilinunuliwa vifaa vya maabara vyenye thamani ya shs.16m/= na kwa mwaka 2005/2006 Chuo kilitengewa na kutumiwa jumla ya shs. 60m=/. Fedha hizi ni kwa ajili ya kununua vifaa vya kufundishia, Kompyuta na vifaa vyake, T.V. na Radio. Ununuzi wa vifaa/vyombo hivyo imeshafanywa, hatua iliyobakia ni ya usafirishaji wa mali hizo kwenda Chuo cha Missungwi.

(c) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa kwa muda mrefu Chuo cha Missungwi kilikuwa hakijafanyiwa ukarabati mkubwa wa majengo yake. Kwa kutambua hili, kwa mwaka wa fedha 2005/2006 Wizara ilitenga na kutuma Chuoni fedha T.shs. 156.0m/= Fedha hizi ni kwa ajili ya ukarabati mkubwa kwa majengo yake ikiwa ni pamoja na madarasa. Ukarabati wa majengo ya Chuo hicho umeshaanza. Naomba nimalizie kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Shibili, Mbunge wa Jimbo la Missungwi kwa kuwa mfuataliaji mzuri sana na mchocheaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo ya Chuo na katika jimbo lake kwa ujumla. Aidha, kama Mjumbe wa Bodi ya Chuo, mchango wake huu unakisaidia sana Chuo cha Missungwi kupata maendeleo na ufanisi zaidi.

MHE. JACOB D. SHIBILITI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Labda nianze tu kwa kukubaliana na majibu mazuri aliyoyatoa Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na Waziri wake kwa kazi nzuri ambayo kwa kweli imeonyesha ukomavu wa hali ya juu kwa akinamama katika kutekeleza mambo mbalimbali.

Katika pongezi hizo siwezi kumsahau Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, ambaye mipango yake ndiyo iliyofanikisha mambo haya. Baada ya maelezo naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa Naibu Waziri amekubali kwamba ukarabati mkubwa utafanyika katika Chuo hicho cha Missungwi. Je, katika ukarabati huo wamekumbuka suala la samani katika majengo hayo?

Pili, kutokana na hali halisi ya wana Missungwi kufurahishwa na jinsi ukarabati ulivyofanyika na unavyoendelea kufanyika. Je, Waziri au Naibu waziri uko tayari kuwatembelea wana Missungwi angalau waje wakuchezee ngoma ya Masalikola? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:
Mheshimiwa Spika, kuhusu fedha kwa ajili ya ukarabati kama zilitengwa kwa ajili ya samani. Sisi Wizara kama nilivyosema bajeti yetu ni finyu, fedha 156m zilikuwa kwa ajili ya ukarabati mkubwa wa majengo.

Sasa nadhani tutazungumza na Mheshimiwa Mbunge ili tuone jinsi gani tunaweza tukahamasisha na kupata ufadhili hasa tukiangalia kwamba kuna baadhi ya vyuo ambavyo vimepata misaada kutokana na marafiki kama Chuo cha Singida ambapo wamekuwa na marafiki Swiden, Monduli wanamarafiki nje wanapata misaada. Kwa hivyo tutaongea na Mheshimiwa Mbunge tuone ni jinssi gani tunaweza tukapata misaada mbalimbali ili tukaongeza samani na vifaa mbalimbali vinavyohitajika katika chuo.

Aidha, napenda pia kushukuru pongezi zake kwa Wizara yetu, tunapokea kwa heshima na taadhima na unyenyekevu mkubwa na pia mwaliko wake tumepokea na nina uhakika Mheshimiwa Waziri wangu na mimi tutapenda kuja chuoni kuwatembelea na kuangalia maeneo ya Jimbo kwa ujumla. (*Makofi*)

Na. 86

Serikali Kugharamia Matibabu ya Ugonjwa wa Malaria

MHE. AMINA C. MPAKANJIA aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imefanya juhudu kubwa katika kupambana na magonjwa mbalimbali kwa lengo la kutokomeza kabisa au kupunguza magonjwa kama vile Matende, TB, na UKIMWI kwa kutoa dawa bure kwa waliopatikana na matatizo hayo, lakini uko ugonjwa wa Malaria ambao umekuwa sugu na tishio kwa maisha ya Watanzania walio wengi wakiwemo watoto wachanga/wadogo ambao wanaathirika kwa kiwango kikubwa na ugonjwa huo:-

Je, Serikali haioni kuwa ni busara kuondoa kabisa gharama za matibabu ya ugonjwa wa Malaria kama ilivyofanya kwa magonjwa niliyotaja ili kuyanusuru maisha ya akina mama, watoto na Watanzania wote kwa ujumla?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwi Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii napenda kujibu swali la Mheshimiwa Amina C. Mpakanjia, Mbunge wa Vita Maalum, kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, Malaria ni ugonjwa unaoathiri sana afya za watu katika jamii na hasa hapa Tanzania na maeneo mengine ya nchi za joto. Utafiti unaonyesha kuwa licha ya kupunguza uzalishaji kaya zinatumia asilimia 20 ya mapato yake kwa matibabu ya Malaria. Karibu Watanzania wote milioni 34 wanaishi katika maeneo yenye Malaria.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imekuwa ikishirikiana na wahisani na taasisi zisizo za kiserikali kwa lengo la kupunguza malaria nchini katika maeneo yafuatayo:-

- (i) Kuna mpango wa Hati punguzo kwa wajawazito.
- (ii) Kuondoa kodi ya vyandarua na dawa za viatilifu.

Mheshimimiwa Spika, akina mama wajawazito na watoto chini ya umri wa miaka mitano ambao ndiyo waathirika zaidi wa ugonjwa wa malaria kuliko watu wengine hawalipii huduma za afya katika hospitali za Serikali ikiwa pamoja na tiba ya malaria.

Mheshimiwa Spika, tangu mwaka 1993/1994, Serikali ilipoanzisha mpango wa uchangiaji gharama za matibabu katika hospitali za umma ilibainisha jamii ya watu wanaotakiwa kupata msamaha wa malipo kama ifuatavyo:-

- (i) Watoto wote chini ya miaka mitano ambao ni asilimia 20 ya ida ya wahapa nchini hawa wanatakiwa wasilipie .
- (ii) Akina mama wajawazito ambao ni asilimia nne ya jamii ya watanzania watu wate wasiojiweza na ambao hawana ndugu wa kuwasaidia na
- (iii) Wazee wote wenye umri zaidi ya miaka 60 wasio na uwezo wala ndugu wa kuwasaidia.

Mheshimiwa Spika, Tanzania mikuwa ikitumia dawa ya Sp, katika kutibu ugonjwa wa malaria. Dawa hii imekuwa ikiigharimu Serikali wa wastani wa shilingi bilioni 2 kila mwaka . kuanzia mwezi Novemba 2006 Serikali itaanza kutumia dawa mseto kwa ajili ya matibabu ya malaria baada ya SP kuonyesha usugu. Dawa hizi mpya zitagharimu Serikali kiasi cha shilingi bilioni 25 kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, makundi ya wagonjwa niliowataja hapo awali wataendelea kupata matibabu haya bila malipo na napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu na wananchi kwa ujumla kwamba hakuna mwananchi ye yeyote atakayekosa huduma au kukosa matibabu ya malaria kwa kukosa fedha ya malipo.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge nieleze tu kwamba ingawa muda wa maswali unaoneka kama umepita lakini kwa sababu tualinza na matangazo marefu kidogo basi naruhusu kwa mamlaka niliyonayo tuendelee hadi tumalize maswali ya leo yaliyoko kwenye *Order Paper*. Mheshimiwa Amina Mpakanjia swali la nyongeza.

MHE. AMINA C.MPAKANJIA: Mheshimiwa Spika ahsante kwa kunioa na kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini nilikuwa nina maswali madogo mawili ya nyongeza:-

La kwanza, kwa kuwa Serikali inatumia fedha nyingi sana kwa semina na warsha kwa ajili ya ugonjwa wa UKIMWI wakati ugonjwa ambao unaoongoza kwa kuua watu zaidi ni ugonjwa wa malaria. Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka kuelekeza fedha nyingi kwenye kuelimisha jamii kuhusiana na ugonjwa huu wa malaria pamoja na madhara ambayo yanapatikana katika ugonjwa huu?

La pili, kwa kuwa madawa ya *SP* yameonyesha kuwadhuru wananchi wenyе *allergy* ya *sulphur* na namshukuru pia Mheshimiwa Naibu Waziri amesema wataleta dawa mbadala ya *SP*, Je anaweza akatuambia hiyo dawa mbadala inaitwaje na itaanza kutumika rasmi lini?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba ugonjwa wa malaria unaua haraka kuliko ugonjwa wa UKIMWI, na ni kweli kwamba kuna semina nyingi zinafanyika. Lakini naomba nikarushe kwamba si kweli kwamba malaria haishughulikiwi kwa mapana zaidi. Kwa sasa hivi Tanzania kuna *program* maalum ambayo inashughulikia magonjwa ya malaria ambayo ni *program* inayohusisha suala la malaria, *TB* na ina mpango wa fedha kabisa ambao unashugulikia, na Serikali imeendelea kuongea na kuzungumza na wananchi katika Halmshauri ili kuona kwamba suala la malaria inafahamika na kueleza wananchi jinsi ya kujikinga na kuzuia kuambukiza na kueneza ugonjwa wa malaria.

Mheshimiwa Spika, suala la pili, ni kweli kwamba kuna baadhi ya wagonjwa ambao wanapata tatizo na dawa za *SP*. Ambayo ni kweli inahusiana na *sulphur* ambayo iko katika dawa ile, lakini napenda kusema si wagonjwa wengi sana ambao wanapata tatizo hilo la *reaction*. Lakini kama aliviyotaka kujua dawa hii ya mseto inaitwa *atemethecyne luthamethentrine*. Kwa sababu inawezekana asielewe vizuri basi nitakuwa tayari kumwandikia vizuri na wale Wabunge wote ambao watahitaji basi nitaliandika vizuri kwa kitaalam halafu nitawapitishia ili waweze kuifahamu, lakini kwa kifupi tunaita *ALU*.

MHE. CHACHA Z. WANGWE: Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri ametueleza kwamba Serikali inahakikisha kwamba hakuna Mtanzania atakayekufa kwa malaria na kuna watoto wale ambao ni yatima na watoto wanaoishi katika mazingira magumu na wale wa mitaani. Je, Serikali inawahudumiaje na idadi yao ni wangapi?

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge hilo ni swali jipya, linahusu watoto wa mitaani na hapa tunazungumzia dawa ya malaria.

MHE. ROSEMARY KIRIGINI: Mheshimiwa Spika ahsante sana kwa kunipa nafasi, swali la msingi linazungumzia matibabu ya malaria, kumekuwepo na dawa nyingi za *SP* ambazo hazina ubora kwenye soko na kupelekea wagonjwa wake kutopona malaria au kusababisha hali ya usugu wa ugonjwa huo. Je Wizara inashughulikia vipi dawa hizo za *SP* ambazo hazina ubora kwenye soko.

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, dawa za *SP* ambazo ziko katika masoko kama zimepitia katika mpango wa kudhibitiwa a kuonekana zinafaa mimi nasema sio kwamba zinaonekana hazina ubora dawa zote ambazo ziko madukani na kama zimeingia kwa njia ya halali na zimepimwa zote zinawezo wa kutibu malaria.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kueleza hapa ni kwamba usugu wa dawa sio kwa sababu ya ubora tu wa dawa lakini inawezekana pia ni kwa sababu ya matumizi mabaya ya zile dawa. Kwa mfano, kama wewe utatumia dawa hiyo ya *SP* ambayo ina ubora lakini hutatumia dozi ambayo ni sahihi. Hii itakusababishia kwamba malaria yako ikaleta usugu. Lakini vilevile kama utatumia dawa ambayo haipaswi kutumiwa wewe unafikiri una malaria, lakini huna malaria hii pia inaweza kusababisha ikaleta usugu wa malaria utapokuwa unaumwa. Kwa hiyo, ningeshauri kwamba wananchi kwa ujumla tutumie dawa baada ya kushauriwa na madaktari na twende tukanunue dawa katika maduka ambayo yamehakikiwa na vilevile twende kwenye vituo vyta kutolewa dawa ambazo zina ubora ili tuweze kupunguza tatizo hili la usugu.

SPIKA: Mheshimiwa Faida Mohamed Bakari umesimama mara kwa mara kwenye suala la malaria, kwa kuwa linalofuta ni la maradhi nitakupa nafasi ya pili ya swali la nyongeza.

Na. 87

Usugu wa Baadhi ya Magonjwa

MHE. ANASTAZIA WAMBURA aliuliza:-

Kwa kuwa, kuna tatizo la usugu wa baadhi ya magonjwa miongoni mwa wananchi:-

- (a) Je, Serikali inaweza kulihusisha tatizo hilo na matumizi ya dawa zisizokuwa na ubora halisi;
- (b) Je, Serikali inadhibiti vipi ubora wa dawa zinazoingizwa nchini?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii napenda kujibu swali la Mheshimiwa Anastazia Wambura, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kuna sababu nyingi zinazoweza kusababisha usugu wa dawa wakati wa kutibu baadhi ya magonjwa zikiwemo:-

- Matumizi mabaya ya dawa kwa maana ya mtumiaji kushindwa kumaliza dozi ya dawa aliyandikiwa na daktari au kuitumia isivyotakiwa

• Daktari kumuandikia mgonjwa dawa chache hivyo kusababisha dozi kamili kutotumika na vilevile matumizi ya dawa ambazo hazijafikia viwango vya ubora.

- Matumizi yasiyo ya lazima ya dawa mfano *antibiotics* ambapo dawa mbadala ingeweza kutumiwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na sababu nilizozitaja hapo juu, ni kweli kabisa kuwa baadhi ya matatizo ya usugu wa vimelea vinavyosabaisha magonjwa mbalimbali kwa baadhi ya wananchi yanasaababishwa na matumizi ya dawa zisizo na ubora unaotakiwa.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imejiwekea utaratibu ufuatao katika udhibiti wa ubora wa dawa zinazoingizwa nchini ikiwa ni pamoja na Usajili wa dawa zinazotumika nchini

Mheshimiwa Spika, dawa zote zinazoruhusiwa kuingizwa nchini ni zile ambazo zimesajiliwa na Mamlaka ya Chakula na Dawa (*TFDA*). Dawa hizi ni zile ambazo zimefanyiwa tathimini ya kina, inahusisha upitiaji wa taarifa za kisayansi za dawa, upimaji wa sampuli katika maabara na ukaguzi wa viwanda vinavyotengeneza dawa husika kuona kama vinakidhi mahitaji yetu ya kisheria.

Mpaka sasa *TFDA* imeweza kusajili dawa elfu tatu mia tano na tisini na tisa (3,599) ambazo zinatumika nchini kwa kutumia utaratibu huu. Udhibiti katika mipaka ya kuingiza dawa nchini

Mheshimiwa Spika, katika kudhibiti mipaka ya kuingiza dawa nchini, Serikali imeainisha mipaka inayoruhusiwa kuingiza dawa nchini na kuweka wakaguzi kuhakikisha kuwa dawa zinazoingizwa nchini ni zile zilizosajiliwa na kupewa kibali cha kuingizwa nchini.

Aidha, katika baadhi ya mipaka, *TFDA* imeweza maabara ndogo (*Mini lab Kits*) ambazo hutumiwa na wakaguzi kufanya uchunguzi wa awali (*Preliminary Screening*) kwa dawa muhimu kama zile za Malaria, UKIMWI na baadhi ya *antibiotics*. Baadhi ya mipaka iliyo na maabara ndogo ni Bandari ya Dar es Salaam, Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu J. K. Nyerere na mpakani Namanga. Ukaguzi na ufuutiliaji wa dawa katika soko. *TFDA* kwa kushirikiana na wakaguzi wa dawa waliopo katika Halmashauri au Manispaa mbalimbali nchini hufuutilia dawa zilizo katika soko kwa kuchukua sampuli wakati wa ukaguzi na kuchunguza katika maabaa ili kubaini kama zinafikia viwango vya ubora vilivyotumika wakati wa usajili wa dawa hizo.

MHE. ANASTAZIA WAMBURA: Mheshimiwa Spika ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza, namshukuru pia Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa upo uwezekano wa madawa ya kuingia katika soko kwa njia za panya kitu ambacho kinaweza kusababisha kuwepo kwa dawa ambazo si

halisi na ambazo hazina ubora. Je, Serikali inafanya jitihada gani kupambana na tatizo hili?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, kama nilivyokua nimezungumza hapo awali na katika majibu ya maswali mengine ambayo nimeshayajibu katika kipindi hiki, ni ukweli kwamba kuna dawa nyingine ambazo zinaweza kuingia kwa njia ya panya lakini tumeweka utaratibu kwamba ziko Kamati za Mikoa ambazo ziko chini ya uongozi wa Mkuu wa Mkoaa ambazo zinatakiwa kupita katika yale maduka ambayo huwa yanauza dawa na kufanya ukaguzi wa mara kwa mara. Lakini vilevile *TFDA* au Serikali kwa ujumla ina utaratibu wa kupita katika maduka ya dawa na kupertia katika viwanda ili kuangalia kwamba dawa zinazoingia ni za ubora unaoslahili.

Lakini kama haitoshi vilevile Serikali tunaomba tuendelee kusisitiza kwamba tunaomba wananchi wanapokuwa na matatizo waweze kwenda kwa wataalam na kununua dawa katika maduka ambayo yana viwango ili waweze kupata dawa ambazo zina viwango na zile ambazo zimepita kwa njia ya panya basi kama hazina ubora wakati wa ukaguzi zitakuwa zinachukuliwa na kutolewa katika soko. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge ningewaomba tusaidiane wote pamoja ilituweze kutatua tatizo hili.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge naona Mheshimiwa Faida Mohamed Bakary hakutaka kuongea tena, nahisi ameghairi lakini bado kipindi ni kirefu cha mkutano huu wa Bunge, tutampatia nafasi tuu.

Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na maswali yamekwisha. Ninayo matangazo machache.

Kwanza nimepata barua toka Kambi ya Upinzani, ambayo kidogo nadhani inataka maelezo kwa sababu walisema hata wao kuna Wabunge wa Upinzani ambaa wanavyeo. Maelezo ni hivi tukio lazima liwe ni tukio la hivi karibuni siwezi kutangaza kila kitu hata cha mwaka jana. Tukio la CCM ni la jana usiku na tuko hapa Dodoma Bungeni. Lakini la pili baadhi ya vyeo chama chochote kikiniletea kwamba Wabunge wamepewa vyeo hivi mimi sitatangaza. Ila leo nawapeni mfano tu, upande wa CHADEMA wanasema Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya ameteuliwa kuwa Afisa Maendeleo hili siwezi kutangaza.(*Makofit/Kicheko*)

Wanaendelea na kusema kwamba Mheshimiwa Halima Mdee, ni Afisa wa Sheria na Haki za Binadamu. Maafisa ni cheo cha kawaida tu kwa hiyo ni lazima ifanyake kama ilivyofanyika kwa CCM, unapata Mkuu wa Idara kama ilivyo kwa Dr. Wilbrod Slaa ambaye yeye ni Katibu Mkuu wa chama lingetokea wakati huu ningelitangaza. Tunabahati sana leo na hili nieleze nimepata lawama, kwamba napenda sana kuwatangaza walipo kwenye *gallery*. Hili ni Bunge la watu na mimi nina mamlaka nikiwa kwenye kiti hiki na kuendesha shughuli za Bunge. Mimi nadhani itakuwa ni udhaifu kwa Bunge letu kama tutakuwa hatuwatambui wananchi tena mkumbuke ndiyo wapiga kura pamoja na wageni ambaa baadhi yao wanawakilisha mataifa ambayo tuna uhusiano mzuri sana na baadhi wakiwa ni wahisani. Kwa hiyo, mnivumile nataka niwatambue wafuatao:-

Kwanza Mheshimiwa Balozi George Kahama, kwa wale vijana kama kina Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa George Kahama, alikuwa katika Baraza la Mawaziri wa Serikali ya Kwanza ya Uhuru mwaka 1961, na amekua ndani ya utumishi kwa uaminifu mkubwa katika nchi yetu kwa miaka yote hadi sasa. Binafsi napenda nimbambue zaidi, kwa sababu ananigusa zaidi. Nilipoingia kuanza Utumishi wa Umma mwaka 1969, Balozi Kahama alikuwa *Boss* wangu pale *National Development Cooperation (NDC)*, na si mimi peke yangu Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, Mheshimiwa Basil Mramba, tulikuwa pamoja alikuwa mwanafunzi wake pia na Waziri wa Usalama wa Raia, Mheshimiwa Bakari Mwapachu na Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Joseph Mungai wote tulikuwa pamoja katika Jumuiya hiyo ya *NDC* na tulilelewa vizuri sana. Nimemsahau Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii pia, nadhani mnaweza kuona sasa umuhimu wa Mzee wetu huyu Mheshimiwa George Clemence Kahama. Kwa kweli tunamshukuru sana kwa kutusaidia. Huku kote wengine tulipofika ni kutokana na malezi mazuri sana ya Mzee George Kahama ahsante sana.(*Makofi*)

Miongoni mwa wageni pale *Speaker's Gallery* yuko Mheshimiwa Balozi Ali Mchumo, ni maarufu wengi mtamkumbuka alikuwa Mbunge machachari sana wa Temeke na baadaye akawa Waziri ameshika Wizara mbalimbali katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hivi sasa ye ye ndiyo Mkurugenzi Mwendeshaji wa *The Common Fund for Commodities* kule Amsterdam ana hadhi ya Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa. Naomba pia nimbambue miongoni mwa Wakuu wa Mikoa, Mheshimiwa Kapteni Jaka Mwambi, ambaye hadi sasa amekua ndiyo Mkuu wa Mkoa wa Iringa, lakini sina hakika kama ataendelea na ukuu wa mkoa kwa muda mrefu kwa sababu jana aliteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi (CCM). (*Makofi*)

Pamoja naye wako Wakuu wa Mikoa ifuatayo na majina yao mitayatamka. Mheshimiwa Meck Sadiki, Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Mheshimiwa Isidore Shirima, Mkuu wa Mkoa wa Mara, Mheshimiwa John Mwakipesile alikuwa Mbunge mwenzetu huyu sasa ni Mkuu wa Mkoa Mbeya, Mheshimiwa Meja Jeneral Said Kalembo, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Mheshimiwa Brigedia Jeneral Balele, Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Mheshimiwa Dr. Christine Ishengoma, Mkuu wa Mkoa wa Pwani na Mheshimiwa Abbas Kandoro, Mkuu wa Mkoa wa Arusha. (*Makofi*)

Wamefuatana pia na Ma-RAS wafuatao, Ndugu Joshua Kileo, RAS wa Shinyanga, Mama Getrude Mpaka, RAS wa Pwani, Mama Betha Swai, RAS wa Dar es Salaam na Chrisant Rubunga, RAS wa Mkoa wa Mara. (*Makofi*)

Kama nimewaacha wengine wowote watakuwa waliingia baada ya karatasi hizi kunifika wote wanakaribishwa. Naambiya yupo Mkuu wa Mkoa wa Singida, Mheshimiwa Parseko Ole Kone, kwa sababu si tu alikua Mbunge machachari humu ndani ya Bunge, lakini pia alikua ni Kamishina wa Tume za Huduma za Bunge. Nimeambiwa piwa tunaye Mheshimiwa Henry Shekiffu, Mkuu wa Mkoa wa Mtwara,

Mkuu wa Mkoa Kilimanjaro Mheshimiwa Mohammed Babu, Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Mheshimiwa Ditopile Mzuzuri, Mkuu wangu huyu. Basi nadhni kwa wageni walioko *Speaker's Gallery* nadhani nimemaliza ila tu ninayo heshima, nalo limenifikia sasa hivi, ama sivyo ningelitanguliza kutokana na umuhimu wake. Yupo hapa Mama Regina Lowassa, Mke wa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Lakini kwa mtiririko huo huo yupo pia mke wa Mheshimiwa Omar Kwaangw' Mbunge wa Babati. (*Makofî*)

Sasa kwa haraka haraka tunao wageni wengine ni Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM kutoka Rukwa, wageni wa Mheshimiwa Mizengo Pinda ni wale pale ahsante sana. Yupo Mheshimiwa Karama, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Muleba, yule pale. Wapo wajumbe wa Kamati ya Siasa kutoka Dimani Zanzibar, wageni wa Mheshimiwa Hafidh, wapo pia Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Tanga Mzee Shekimweri. Viongozi wa CCM wa Wilaya ya Lushoto wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya, Diwani Mbughuni, hawa ni wageni wa Mheshimiwa Shellukindo. Miongoni mwa wageni yupo Ndugu Nzaeli Kyomo, aliyetupa heshima kubwa kwa kuwa mwanariadha bingwa wa kimataifa miaka ya 1978 hadi 1986. Viongozi wa CCM kutoka wa Wilaya ya Manyoni ambao ni wageni wa Mheshimiwa Waziri Chiligati, Mwenyekiti wa CCM, Hussein Masao pamoja na wenzake wale pale. Tuna wageni wa Joyce Machimu, wanaotoka Shinyanga nao ni Ndugu William Machibya, ambaye ni mumewe Mheshimiwa Joyce Machimu, lakini pia ni Mjumbe kutoka Bariadi Shinyanga. Wageni wengine ni madiwani ambao ni Mheshimiwa Lameck Mkilila na Getrude Ngokolo. Pia viongozi wa Chama cha Mapinduzi Bariadi, Mheshimiwa Silvester Buyaga na Mheshimiwa Athuman Shesha.

Mwisho sio mwisho kwa umuhimu basi tu ni mpangilio wa karatasi, naomba nimbambulische Mheshimiwa Hashim Saggaf, aliyekuwa Mbunge wa Dodoma Mjini. Waheshimiwa Wabuge kinachofurahisha hapa ni kwamba aliyeleta karatasi hii ni Mheshimiwa Mbunge wa sasa wa Dodoma Mjini, Mheshimiwa Ibrahim Madeje. Hii inadhihirisha kwamba hapa Dodoma Mjini wana utamaduni mzuri wa kupokezana vijiti bila nongwa nawapongeza sana. (*Makofî*)

Waheshimiwa Wabunge wa Umoja wa Wabunge wa Kupambana na Ukimwi (*TAPAC*) wanaombwa kukutana saa saba kamili katika Ofisi ya *TAPAC* leo mchana. Mara baada ya shughuli za asubuhi. (*Makofî*)

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2006/2007 Ofisi ya Waziri Mkuu

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika naomba kutoa Hoja kwamba kutokana na Taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala iliyochambua Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge lako sasa lipokee na kujadili Taarifa ya mapitio ya utekelezaji wa kazi za Serikali kwa mwaka 2005/2006 na Mwelekeo wa kazi za Serikali kwa mwaka 2006/2007. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuitisha Makadirio ya Matumizi ya fedha ya ofisi ya Waziri

Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Asasi zilizo chini yake na yale ya Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2006/2007. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Napenda kumpongeza pia kwa kuchaguliwa jana kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi. Aidha nampongeza Dr. Ali Mohamed Shein kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Amani Abeid Karume, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Ushindi wao ni uthibitisho wa imani kubwa waliyo nayo wananchi kwao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, na mimi naomba nijiunge na wewe na Waheshimiwa Wabunge kumpongeza Mheshimiwa Rajab Yusufu Makamba kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi. Nimpongeze Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanri, Mbunge wa Siha, kwa kuchaguliwa kuwa Katibu Mwenezi wa Chama Cha Mapinduzi. Nimpongeze Mheshimiwa Kidawa Saleh kwa kuchaguliwa kuwa Katibu wa Oganaizesheni ya Chama cha Mapinduzi. Nimpongeze Mheshimiwa Asha-Rose M. Migiro, kwa kuchaguliwa kuwa Katibu wa Uhusiano wa Kimataifa wa Chama cha Mapinduzi. Na nimpongeze Mheshimiwa Jakka Mwambi kwa kuteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rostam Aziz, kwa kuwa Mweka Hazina wa Chama cha Mapinduzi (CCM).

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kukupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Imani kubwa uliyopewa na Waheshimiwa Wabunge ni kwa kutambua uwezo na uzoefu wako katika uongozi. Aidha, tuna matumini makubwa kuwa utaliongoza Bunge hili ili liweze kutimiza matarajio ya wananchi. Nampongeza vilevile Mheshimiwa Anne S. Makinda, Mbunge wa Njombe Kusini, kwa kuchaguliwa na Waheshimiwa Wabunge kuwa Naibu Spika. Ninaamini kuwa uwezo na uzoefu wake wa uongozi katika Bunge, utamwezesha kutoa mchango mkubwa katika kumsaidia Mheshimiwa Spika na Bunge hili kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge kama ifuatavyo:- Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda, Mbunge wa Handeni, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi; Mheshimiwa John M. Cheyo, Mbunge wa Bariadi Mashariki, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, Mheshimiwa George Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, Mheshimiwa Anna Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum, Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Mheshimiwa William Kusila, Mbunge wa Bahi, Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mbunge wa Ilaje, Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mbunge wa Babati Mjini, Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Juma Nh'unga, Mbunge wa Dole, Mwenyekiti wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama,

Mbunge wa Peramiho, Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Job Ndugai, Mbunge wa Kongwa, Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili na Mazingira, na Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mbunge wa Singida Kusini, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu.

Mheshimiwa Spika, vilevile, napenda kuushukuru uongozi wa awamu zilizopita ambazo zimejenga misingi ya Serikali ya Awamu ya Nne. Waheshimiwa Wabunge mtakubaliana nami kwamba uongozi wa Awamu ya tatu, chini ya Rais Mstaafu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, umewezesha kuendeleza mazingira mazuri ya kisiasa na kiuchumi nchini. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Frederick Tluway Sumaye, Waziri Mkuu mstaafu wa Awamu ya Tatu, kwa kudumisha mahusiano mema baina ya Serikali na Bunge, kusimamia na kuratibu vizuri shughuli zote za Serikali. Namshukuru pia Mheshimiwa Pius Msekwa, Spika mstaafu na uongozi wake hapa Bungeni kwa kutuachia misingi mizuri ya kuongoza shughuli za Bunge.

Mheshimiwa Spika, na mimi naomba nitumie nafasi hii kwa mara nyingine tena kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa imani kubwa aliyonipa kunitfea kuwa msaidizi wake wa karibu wa kuongoza shughuli za Serikali ya Awamu ya Nne hapa Bungeni. Nawashukuru tena Waheshimiwa Wabunge chini ya uongozi wako thabit wa kasi na viwango kwa kuthibitisha uteuzi wangu kwa kura nyingi. Kazi hii si nyepesi na kwa kipindi cha takriban nusu mwaka nimeona uzito wa majukumu yaliyo mbele yangu, lakini imani yenu kubwa kwangu ilinitia moyo na ushirikiano wenu unaoendelea kunipa nguvu. Ninamini tutaendelea kushirikiana katika ujenzi wa Serikali tunayotarajia kuiendesha kwa misingi ya utawala bora kwa Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya. Nichukue nafasi hii pia kuwapongeza viongozi wote waliochaguliwa na kuteuliwa katika nyadhifa mbalimbali za kuliongoza Taifa hili. Ni matumaini yangu kwamba wote kwa pamoja tutajitahidi kwa nguvu na uwezo wetu wote kuhakikisha kwamba tunafanya kile ambacho wananchi waliotuchagua wanakitegemea. Matumaini ya wananchi ni makubwa sana. Wanayo imani na mategemeo makubwa sana kwetu, naomba tusiwaangushe. (*Makofii*)

Ni vema nichukue nafasi hii kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba tarehe 5 Mei, 2006 aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Ndugu Melkizedeck Sanare, alifariki dunia. Marehemu atakumbukwa kwa mchango wake mkubwa wa uongozi siyo katika Ofisi ya Waziri Mkuu tu lakini vilevile katika Taasisi nyingine za Umma alizopewa fursa ya kuziongoza. Wapo vilevile wananchi waliofariki katika maafa na ajali mbalimbali nchini na wengine kujeruhiwa. Nachukua fursa hii kutoa pole kwa wafiwa wote na kuwatachia afya njema waliojeruhiwa. Mwenyezi Mungu azilaze roho za Marehemu hao mahali pema peponi. Amin.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi kisichopungua siku tano Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakijadili taarifa kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa katika Mwaka 2005 na Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2006/2007 na hatimaye kuitisha Bajeti ya Serikali ya mwaka 2006/2007. Napenda kutumia fursa hii kuwapongeza kwa dhati Mheshimiwa Dr. Juma Alifa Ngasongwa, Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezesaji na Mheshimiwa Zakia Hamdan Meghji, Waziri wa Fedha, kwa hotuba zao nzuri sana. Vile

vile napenda nitumie nafsi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri ambayo itaisaidia Serikali wakati wa utekelezaji wa Bajeti na mpango wa mwaka 2006/2007. Sote humu ndani tumeandika historia. Bajeti ya mwaka huu imepita kwa asilimia 100. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, tumeanza vizuri. Naomba tuendelee na kumalizia hivyo hivyo. Natoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Katiba Sheria na Utawala chini ya uongozi wa Mwenyekiti wake Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, kupitia Makadirio ya Matumizi ya fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Ofisi ya Bunge. Ninazishukuru vile vile Kamati za kudumu za Bunge lako Tukufu kwa kupitia Makadirio ya Matumizi kwa kila Wizara, Idara za Serikali zinazojitegemea na Asasi zilizo chini ya Wizara zote kwa michango na ushauri uliotolewa kwa Bajeti ya mmwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Spika mwaka 2006/2007 ni wa kwanza wa Serikali ya Awamu ya Nne kuandaa na kuwasilisha Bajeti ya Serikali. Lengo kuu la Serikali ni kuwawezesha wananchi kubadili maisha yao na kuwa bora zaidi yaani maisha bora kwa kila Mtanzania. Lengo hilo litafikiwa kwa kutumia Bajeti ya Serikali, misaada ya wadau mbali mbali pamoa na juhudhi za wananchi wenyewe. Mipango ya Serikali iliyoainishwa na kutengewa fedha kwenye Bajeti ya Serikali inazingatia ahadi zilizomo katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005. Majukumu mawili ya msingi yaliyoainishwa kwenye Ilani ya uchaguzi ya CCM ni haya:-

- (i) Kuitoa Tanzania kutoka kwenye dimbwi la uchumi ulio nyuma na tegemezi na kuiingiza katika mkondo wa uchumi wa kisasa wa taifa linalojitegemea.
- (ii) Kuwashirikisha wananchi wote kwa njia ya uwezeshaji katika ujenzi wa uchumi na kuutokomeza umaskini.

Mheshimiwa Spika, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, ametoa tamko la jinsi Serikali anayoiongoza itakavyotekeliza ahadi hizo. Tamko hilo alilitoa kwenye hotuba yake ya uzinduzi wa Bunge lako Tukufu tarehe 30 Desemba, 2005. Tamko hilo lina mambo kumi ambayo Watanzania wanatakiwa wayatarajie kutoka Serikali ya Awamu ya Nne katika miaka mitano ijayo kama ifuatavyo:-

- (i) Kuhakikisha kuwa amani, utulivu na umoja wan chi yetu na watu wake vinadumishwa;
- (ii) Kudumisha na kuendeleza mafanikio yaliyopatikana tangu Serikali ya Awamu ya Kwanza hadi leo;
- (iii) Kuendeleza vita dhidi ya Umaskini, ujinga na maradhi, tena kwa Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya;
- (iv) Kutimiza ipasavyo wajibu wake wa utawala na maendeleo, na kuendesha dola kwa misingi ya utawala bora na uwajibikaji, utawala wa sheria unaoheshimu na kulinda haki za binadamu;

- (v) Kuimarisha uwezo wake wa kulinda maisha na mali za raia wake. Kupambana na uhalifu wa kila aina, na kwamba majambazi hayataachwa yatacombe yatakavyo;
- (vi) Kuhakikisha mipaka ya nchi yetu ipo salama. Kutomruhusu mtu au nchi yoyote kuchezza mipaka ya nchi yetu na uhuru wetu;
- (vii) Kufanya kila tuwezalo kuhakikisha Tanzania ina mahusiano mazuri na mataifa yote duniani, pamoja na Mashirika ya Kimataifa na Kikanda;
- (viii) Kujali maslahi na mahitaji ya makundi maalum katika jamii kama vile wanawake, vijana, watoto, wazee, walemaavu na yatima;
- (ix) Kuongoza mapambano mapya ya kuhifadhi mazingira ili vizazi vijavyo virithi nchi nzuri na msingi imara wa maendeleo endelevu; na

(x) Kuendeleza michezo na shughuli za utamaduni na burudani.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Serikali iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu kwa mwaka 2006/2007, imezingatia ahadi hizo. Aidha, Serikali inapoanza utekelezaji wa majukumu yaliyoanishwa katika mpango wa mwaka 2006/2007, itaongozwa na ahadi hizo maalum pamoja na zile za jumla zilizopo katika ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, MKUKUTA, Dira ya Maendeleo ya Taifa 2005 na Malengo ya Maendeleo ya Milenia. Viongozi na Watendaji wa Serikali wanategemewa kuelewa ahadi na mikakati hiyo na kuhakikisha kuwa fedha zinalekezwa kwenye maeneo yaliyoanishwa kwenye mpango wa Maendeleo.

Serikali katika ngazi zote inahitaji umakini na umahiri katika utekelezaji wa mpango yake, hivyo haitakubali vikwazo vya aina yoyote visivyo vya lazima. Viongozi na watendaji wote wa Serikali wanao wajibu wa kuimarisha usimamizi na ufuutiliaji na kila mara kutoa taarifa za utekelezaji kwa mamlaka husika.

Mheshimiwa Spika, viongozi na watendaji wa Serikali wanao wajibu wa kutambua kuwa hawatakiwi kuachwa nyuma kama alivyowahi kusema Mwandishi mmoja aitwaye David Henry Thoreau kuwa *I quote: “If a man does not keep pace with his companions, perhaps it is because he hears a different drummer. Let him step to the music he hears, however measured or far away.”*

Tafsiri ya Kiswahili isiyo rasmi ya maelekezo hayo ni kuwa: “Mtu asipoweza kuhimili kasi ya wenzake inawezekana anasikiliza midundo ya mpiga ngoma tofauti. Hivyo, aachweacheze kulingana na midungo ya ngoma anayoisikia hata kama usikivu ni hafifu au mpiga ngoma huyo yuko mbali” (*Makofit*)

Serikali ya Awamu ya Nne haiwezi kumwachia kila kiongozi wake au kila mtendaji kusikiliza na kucheza ngoma anayoipenda. Tumeahidi maisha bora kwa kila Mtanzania. Tutekeleza ahadi hiyo kwa Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya. Asiyeweza kucheza ngoma hiyo kwa midundo hiyo inayopigwa na Serikali ya Awamu ya Nne, itabidi atupishe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Changamoto Kubwa zilizoikabili Serikali 2005/2006, Katika kipindi cha mwaka 2005/2006, Taifa lilikabiliwa na changamoto kuu tano ambazo zimegusa ustawi na Maendeleo ya nchi yetu. Serikali ilijizatiti kukabiliana na changamoto hizo kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, Kujitosheleza kwa Chakula, katika miaka miwili mfululizo kuanzia mwaka 2004 sehemu kubwa ya nchi yetu ilikabiliwa na ukame. Ukame huo umesababisha upungufu mkubwa wa chakula, vifo vya mifugo katika baadhi ya maeneo, upungufu wa maji na kusababisha mgao wa umeme katika kukabiliana na tatizo la upungufu wa chakula nchini, katika mwaka 2005/2006, Serikali iligawa jumla ya tani 122,638 za mahindi yenye thamani ya shilingi bilioni 24.5 kwa watu milioni 3.8 walioainishwa kwenye tathmini zilizofanyika mwezi Agosti mwaka 2005 na Januari 2006.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilitoa pia shilingi bilioni 5.5 kwa ajili ya kugharamia usafirishaji wa chakula na shilingi bilioni 1.5 kwa Halmashauri za Wilaya kwa ajili ya kununulia mbegu za mazao ya chakula na kuzigawa bure kwa wananchi walio na upungufu. Kati ya fedha hizo, shilingi milioni 100 zilitolewa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukubwa wa tatizo la upungufu wa chakula nchini, Serikali iliomba msaada kutoka nje na ndani ya nchi. Hadi mwezi Mei mwaka huu, wahisani wa nje walikuwa wametoa shilingi bilioni 12 na wahisani wa ndani shilingi bilioni 5.2 zikiwa fedha taslimu, vyakula na vifaa vingine vyenye thamani ya shilingi bilioni 1.8. Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wahisani wote wa nje na ndani kwa ushirikiano waliounyesha na kuiwezesha Serikali kukabiliana na tatizo la njaa nchini.

Mheshimiwa Spika, ufumbuzi wa kudumu wa tatizo la upungufu wa chakula nchini ni kuhakikisha kwamba kila kaya inahamasishwa ili iwe na utaratibu wa kujiwekea akiba ya chakula kila baada ya mavuno hadi mavuno ya msimo unaofuata. Halmashauri za Wilaya zinao wajibu wa kusimamia suala hili na ninawaomba Waheshimiwa Wabunge tushiriki kikamilifu katika usimamizi wa suala hilo. Aidha, Serikali kwa upande wake itaimarisha hifadhi ya chakula ya taifa ili kuwezesha kuwepo akiba ya chakula cha kutosha angalau miezi mitatu wakati wa njaa. Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika itaandaa utaratibu wa kuwezesha hifadhi ya chakula ya taifa kutekeleza maelekezo haya.

Mheshimiwa Spika, Kuongeza Uwezo wa Kuzalisha Umeme, hali ya uzalishaji umeme nchini haikuwa nzuri kutokana na ukame wa muda mrefu uliosababisha upungufu mkubwa wa maji kwenye mabwawa ya vituo vya kuzalisha umeme. Wastani wa

uzalishaji katika mabwawa hayo ulishuka kutoka uwezo wake wa Megawati 559 hadi Megawati 120 tu. Hali hii ilifanya Shirika la Umeme Tanzania kutegemea umeme unaozalishwa na mitambo inayotumia gesi ya Songo Songo iliyopo Ubungo na umeme unaozalishwa na Kampuni ya *IPTL*. Ili kuongeza uzalishaji umeme, Serikali imefanya yafuatayo:-

- (i) Kukodi mitambo ya Megawati 100 ya kuzalisha umeme kwa kutumia gesi.
- (ii) Kununua mitambo mipyä itakayotumia gesi kuzalisha umeme wa Megawati 100 ambayo itafungwa Ilala (Megawati 40) na pale Ubungo (Megawati 60) ifikapo mwezi Desemba mwaka 2006.
- (iii) Kwa kushirikiana na Serikali ya Uholanzi kuweka jenereta ya Megawati 45 Tegeta, Dar es Salaam ifikapo mwezi Desemba 2006.
- (iv) Kuongeza uzalishaji wa umeme kwa kutumia makaa ya mawe ya Kiwira na kujenga mitambo ya gesi yenye uwezo wa kuzalisha megawati 200 za umeme eneo la Kinyerezi, Dar es Salaam. Hii itasaidia kuondokana na utegemezi wa umeme utokanao na nguvu za maji.

Mheshimiwa Spika, Kupanda kwa Bei za Mafuta, kupanda kwa bei ya mafuta katika soko la dunia kumeathiri sana maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini. Gharama za uzalishaji wa bidhaa na utoaji wa huduma mbalimbali kwa wananchi zimepanda kutoptaka na hali hiyo. Kama alivyoeleza Waziri wa Fedha, kuongezeka kwa kasi ya upandaji bei wa mafuta kumechangia pia kupanda kwa mfumuko wa bei. Pamoja na hatua za kibajeti zilizochukuliwa na Serikali, napenda kusisitiza kwamba wafanyabiashara wa mafuta nchini wasitumie bei ya mafuta iliyopo katika soko la dunia kujipatia utajiri wa haraka haraka. Narudia, wafanyabiashara wa mafuta nchini wasitumie bei ya mafuta iliyopo katika soko la dunia kujipatia utajiri wa haraka haraka. Naitaka Mamlaka ya udhibiti wa Nishati na Maji (*EURA*) isimamie kikamilifu mwenendo wa bei za mafuta nchini na kuchukua hatua pale inapobidi.

Mheshimiwa Spika, Kuongeza Nafasi za Elimu ya Sekondari, mwaka 2005. Wanafunzi wapatao 493,946 walifanya mtihani wa darasa la saba nchi nzima. Kati ya hao, wanafunzi 305,062 ambaa ni sawa na asilimia 61.8 walifafulu. Hata hivyo, wanafunzi waliopata nafasi ya kuijunga na kidato cha kwanza walikuwa 140,055 sawa na asilimia 45.9 tu ya wanafunzi walifafulu. Jumla ya wanafunzi 165,007 sawa na asilimia 54.1 walikosa nafasi za kuingia kidato cha kwanza. Serikali ilichukua hatua za haraka ili kupunguza idadi ya wale waliokosa nafasi. Uongozi wa Mikoa uliagizwa kuhakikisha kwamba shule zilizokuwa zinajengwa zinakamilika na idadi ya vyumba vya madarasa vinaongezwa ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wanapata nafasi za kuijunga na masomo ya sekondari kabla ya mwezi Aprili mwaka 2006. Taarifa zinaonyesha kwamba tumefanikiwa katika mikoa yote nchini. Ninawapongeza Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya waliofanya kazi hii vizuri sana na Wizara ya Elimu. Idadi ya wanafunzi waliopata

nafasi ya kuingia kidato cha kwanza imeongezeka sasa kufikia asilimia 62.1 Changamoto kubwa sasa ni kupata walimu wa kutosha na wenyе sifa kwa ajili ya shule zilizoanzishwa.

Mheshimiwa Spika, Kuhifadhi Mazingira, nchi yetu inakabiliwa na uharibifu mkubwa wa mazingira na athari zake zimeanza kujitokeza kama vile kutoweaka kwa misitu na kupungua kwa rasilimali maji. Uharibifu huu kwa kiasi kikubwa umetokana na shughuli za kilimo zinazofanywa katika maeneo ya vyanzo vya maji pamoja na ufugaji wa kuhamahama na makundi makubwa ya mifugo wakati wa kutafuta malisho na maji Aidha, ukataji wa miti kwa ajili ya kuni na mkaa, kilimo cha umwagiliaji kisichozingatia taratibu, uchomaji wa misitu na mapori, uchimbaji wa madini usio endelevu, ushiriki na uelewa mdogo wa wananchi katika shughuli za hifadhi ya mazingira ni baadhi ya sababu za uharibifu mkubwa wa mazingira nchini.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na uharibifu huo, Serikali imeunda Kamati ya Mazingira ya Baraza la Mawaziri inayoongozwa na Makamu wa Rais. Kupitia Kamati hii, Serikali imetayarisha Mkakati wa kuhifadhi Mazingira na Vyanzo vya Maji nchini. Serikali imeanza kuchukua hatua za kutunza na kuhifadhi mazingira ambazo zikifanikiwa zitalinusuru Taifa letu kugeuka jangwa.

Baadhi ya hatua hizo ni kuwaondoa wananchi waliovamia vilima, mabonde na maeneo ya vyanzo vya maji na kuanzisha mashamba ya miti ya vijiji na miji kwa ajili ya nishati ya kuni, mkaa na mbaо. Pamoja na kuwaondoa watu hao hasa wafugaji kwenye vyanzo vya maji, ni lazima viongozi wa Mikoa na Wilaya washirikiane kuwaonyesha wafugaji hao mahali pa kwenda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Hali ya Uchumi na Kisiasa Nchini, Serikali inaendelea na jitihada za kusimamia mageuzi ya Sera za uchumi na Maendeleo ya Jamii. Pato halisi la Taifa lilikuа kwa asilimia 6.8 mwaka 2005 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.7 mwaka 2004. Kwa upande mwingine mfumuko wa bei ulipanda hadi kufikia asilimia 6.9 mwezi Aprili, 2006. Kuzingatia hali hiyo, Taifa letu lina changamoto kubwa ya kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi kwa namna ambayo itatafsiri maendeleo na maisha bora kwa kila Mtanzania. Changamoto hii ni kubwa, hasa kwa kuzingatia kuwa idadi ya watu inaongezeka kwa karibu asilimia tatu kwa mwaka. Kwa kasi hii ya ongezeko la idadi ya watu, ni dhahiri kuwa kiwango cha ukuaji wa uchumi kinatakiwa kiwe zaidi ya asilimia 10. Kiwango hiki kitatuwezesha kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa ambayo ni kuwa nchi ya pato la kati ifikapo mwaka 2025. Serikali itaendelea kuchukua hatua za kibajeti kwa lengo la kutoa huduma muhimu kwa wananchi ili waweze kushiriki kikamilifu katika shughuli za uzalishaji mali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mazingira ya kisiasa, kijamii na kiuchumi nchini yanatoa fursa kwa wananchi kushiriki katika shughuli za kisiasa kwa uhuru mkubwa. Shughuli za Uchaguzi Mkuu zilizoanza mwanzoni mwa mwaka 2005/2006 zilitoa msisimko mkubwa kwani Vyama vya Siasa vilipata fursa ya kujitambulisha kwa wananchi na hivyo kuwapa uhuru mpana wa kufanya uchaguzi. Changamoto kubwa kwa vyama vya siasa ni

kuendeleza msisimko huo ili kuipa uhai demokrasia ya vyama vingi vya siasa nchini kwetu.

Mheshimiwa Spika, Usajili wa Vyama vya Siasa, idadi ya Vyama vya Siasa inaongezeka nchini. Katika mwaka wa 2005/2006, Vyama vya Siasa vitatu vilipata usajili wa muda baada ya kutimiza masharti ya kisheria. Vyama hivyo ni Tanzania *Peoples Organisation for Democracy and Development (TAPODD), Solidarity of United Party (SUPA)* na *National Democratic Party for Rehabilitation (NDPR-MAREJESHO)*. Aidha, kazi ya kuipitia upya Sheria ya Vyama vya Siasa Na. 5 ya mwaka 1992 iliendelea kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali. Vilevile, wadau walishirikishwa katika kuandaa kanuni za maadili ya vyama vya siasa. Katika mwaka 2006/2007, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa itaendelea kusajili vyama vya siasa vinavyotaka kuendelea kujisajili, kutoa mafunzo kwa viongozi mbalimbali na kuhakiki uhai wa vyama vya siasa.

Mheshimiwa Spika, Shughuli za Uchaguzi, nchi yetu imefanya Uchaguzi Mkuu mwaka 2005 kwa mara ya tatu chini ya mfumo wa vyama vingi vya siasa. Uchaguzi huo ulifanyika tarehe 14 Desemba, 2005 badala ya tarehe 30 Oktoba, 2005 kutokana na kifo cha Bwana Jumbe Rajab Jumbe, aliyekuwa Mgombea Mwenza wa Mgombea Urais kwa tiketi ya CHADEMA.

Kwa mara ya kwanza uchaguzi nchini umeendeshwa kwa kutumia Daftari la kudumu la Wapiga Kura. Maandalizi ya Daftari hilo yaligharimu shilingi bilioni 39, kati ya fedha hizo, Serikali itoa shilingi bilioni 30 na wahisani walitoa shilingi bilioni 9. Jumla ya wapiga kura walikuwa 15,935,493 waliojiandikisha katika daftari.

Mheshimiwa Spika, katika zoezi la Uchaguzi Mkuu jumla ya vyama 10 vya siasa vyenye usajili wa kudumu, vilishiriki katika kugombea nafasi ya Urais na vyama vyote 18 vyenye usajili wa kudumu vilishiriki katika kugombea nafasi za Ubunge na Udiwani. Vyama vilivyoshiriki ni CCM, CUF, CHADEMA, NCCR-MAGEUZI, UDP, TLP, PPT-Maendeleo, DP, NLD, DEMOKRASIA MAKINI, SAU, UMD, UPDP, NRA, TADEA, FORD, CHAUSTA na JAHAZI ASILIA. Jumla ya wananchi 11,875,927 walipiga kura, kati ya 16,401,634 walioandikishwa na Tume zote mbili.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya uchaguzi yalionyesha kuwa katika Uchaguzi wa Rais, CCM ilipata asilimia 80.28 ya kura zote zilizopigwa. Vyama vingine vilipata kura kama ifuatavyo: *CUF* asilimia 11.68, *CHADEMA* asilimia 5.8, *TLP* asilimia 0.75, *NCCR-MAGEUZI* asilimia 0.49, *DP* asilimia 0.27, *NLD* asilimia 0.19, *PPT* asilimia 0.17, *DEMOKRASIA MAKINI* asilimia 0.15 na *SAUTI YA UMMA* asilimia 0.14. Kwa upande wa matokeo ya Ubunge, Chama cha Mapinduzi kilipata viti 206 kati ya 232, sawa na asilimia 88.79 ya viti vya majimbo vilivyogombewa.

Vyama vingine vilipata viti kama ifuatavyo: *CUF* (19), *CHADEMA* (5), *TLP* (1) na *UDP* (1). Kwa upande wa madiwani, Chama cha Mapinduzi kilipata viti 2,371, *CUF* (61), *CHADEMA* (61), *TLP* (27), *NCCR-MAGEUZI* (12) na *PPT-MAENDELEO* (1).

Mheshimiwa Spika, Tume ya Uchaguzi iliwatangaza Wabunge wanawake wa Viti Maalum 75. Mgawanyo wa Wabunge hao ni kama ifuatavyo: CCM (58), CUF (11) na CHADEMA (6). Matokeo hayo ya uchaguzi yameongeza idadi ya Wabunge Wanawake kufikia 97. Idadi hii ni sawa na asilimia 30.4 ikilinganishwa na asilimia 20 ya mwaka 2000 na hivyo kuliwezesha Bunge letu kufikia malengo yaliyowekwa na Jumuia ya Nchi za Kusini mwa Afrika ya kuongeza idadi ya Wabunge wanawake hadi asilimia 30.

Katika mwaka 2006/2007, Tume ya Uchaguzi itakamilisha tathmini ya uchaguzi wa mwaka 2005 kwa kushauriana na wadau mbalimbali kwa lengo la kuboresha zaidi uendeshaji wa chaguzi zijazo. Aidha, Tume itafanya maandalizi ya kuboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa kuwaondoa wasiostahili na kuingiza wale waliotimiza sifa za kuijandikisha na ambao hawakujandikisha katika kipindi kilichopita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Muungano wa nchi yetu ni matokeo ya mahusiano ya kijamii, kisiasa na kiuchumi baina ya wananchi wa pande zote mbili za Muungano. Muungano unakua na unatupa changamoto za kisiasa na kiuchumi. Moja ya kazi ya msingi ya Serikali ya Awamu ya Nne ni kulinda, kudumisha, kuendeleza na kuimarisha Muungano wetu. Tunao wajibu wa kuepuka hulka za wananchi wachache wanaotaka kupanua wigo wa matatizo ya Muungano kwa kuwagawa Watanzania. Tunatakiwa sote kama Taifa tuelekeze nguvu zetu katika kurekebisha kasoro zilizopo na kupunguza matatizo. Lengo liwe ni kujenga badala ya kubomoa Muungano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, Serikali zetu zilichukua hatua za kuziwezesha Idara, Asasi, Wizara na Sekta zisizo za Muungano kukutana na kuimarisha mahusiano. Dhamira ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuchukua hatua za dhati za kuweka mazingira ya kuwezesha kujenga Muungano imara, zimedhihirishwa kwa kauli ya Mheshimiwa Rais alipozindua Bunge lako Tukufu, akasema kama ifuatavyo:- Ninanukuu.

“Tunakusudia kuongeza mchango wa Serikali ya Muungano katika maendeleo ya uchumi na kijamii ya Zanzibar bila kuathiri haki na mamlaka kamili ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mambo ambayo siyo ya Muungano. Lakini naamini uchumi ambao ni mkubwa zaidi una wajibu wa kusaidia uchumi wa Zanzibar (ambao ni mdogo).” Kwa kutambua umuhimu wa kauli hiyo ya Mheshimiwa Rais, tarehe 22 Mei mwaka 2006 kilifanyika Kikao cha pamoja kati ya Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi. Baadhi ya masuala yaliyojadiliwa ni pamoja na ugawaji wa mapato; utozaji wa kodi kwa wafanyabiashara wa Zanzibar wanapoingia Tanzania Bara; utekelezaji wa sheria kuhusu haki za binadamu; utafutaji na uchimbaji wa mafuta, gesi na uvuvi katika Ukanda wa Bahari Kuu. Masuala mengine yanafanyiwa kazi na Tume ya Pamoja ya Fedha, ambayo inatarajiwa kutoa taarifa yake ya kwanza mwaka 2006/2007. Katika Mkutano huo yalitolewa mapendekezo mbalimbali kwa Serikali zote mbili ambayo yanaendelea kufanyiwa kazi. Mkutano kama huo umepangwa kufanyika tena mwezi Septemba, 2006 ili kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa.

Mheshimiwa Spika, Shughuli za Bunge. Katika mwaka 2005/2006, Serikali imeliwezesha Bunge kukamilisha miradi mikubwa ya ujenzi wa majengo yake ya

Zanzibar, Dodoma na Dar es Salaam. Ujenzi wa Ofisi Ndogo ya Bunge Zanzibar umekamilika, upanuzi wa jengo la Ofisi Ndogo ya Bunge - Dar es Salaam unaendelea na ujenzi wa Ukumbi mpya wa kisasa wa Bunge Dodoma umekamilika na kufunguliwa rasmi na Mheshimiwa Rais tarehe 12 Juni, 2006. Napenda kutumia fursa hii kuwapongeza wote walioshiriki katika kuandaa na kukamilisha miradi hiyo muhimu. (*Makofi*)

Uzinduzi wa Bunge jipya la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ulifanyika tarehe 30 Desemba, 2005 na hivyo kuliwezesha Bunge kuanza utekelezaji wa majukumu yake ya Kikatiba. Katika kipindi cha mwaka 2006/2007, Serikali itaiwezesha Ofisi ya Bunge kuboresha menejimenti na mazingira ya Ukumbi huo wa kisasa na kuwapatia Wabunge ofisi zinazofanana na majukumu waliyopewa katika Majimbo yao. Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa Bajeti ukilinganishwa na mahitaji makubwa, utaratibu wa kuimarisha Ofisi za Waheshimiwa Wabunge utafanyika kwa awamu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2005/2006, hali ya ulinzi na usalama wa raia na mipaka ya nchi yetu na nchi jirani kwa ujumla ilikuwa shwari. Matukio machache ya uhalifu yaliendelea kujitokeza katika mpaka wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na ule wa Burundi. Serikali kwa kushirikiana na wananchi imewafichua wahamiaji haramu na kuwarudisha makwao. Misako ya kudhibiti wageni haramu ilifanyika katika sehemu mbalimbali nchini na jumla ya wageni haramu 1,016 walikamatwa kati ya Julai, 2005 na Aprili, 2006 ikilinganishwa na wageni haramu 308 waliokamatwa katika kipindi cha Julai, 2004 na Aprili, 2005. Aidha, kati ya Januari na Mei, 2006 jumla ya silaha haramu 730 za aina mbalimbali zimekamatwa nchini. Nyingi ya silaha hizo hutumika kwa uhalifu. Ili kudhibiti hali hiyo mwezi Aprili, 2006, kilifanyika Kikao cha kuandaa mikakati ya kukabiliana na mattatizo ya wahamiaji haramu, mifugo inayoingizwa nchini kiholela na kudhibiti uingizaji holela wa silaha. Kikao hicho kilihusisha Mikoa ya mipakani ya Kagera, Kigoma na Rukwa. Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Usalama wa Raia, Mambo ya Ndani, Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Maendeleo ya Mifugo nazo zilishiriki.

Hatua kadhaa zimeanza kuchukuliwa za kuandaa utaratibu wa kuorodhesha wageni katika daftari la kuandikisha wageni wote waishio katika Mikoa yote ya mipakani. Serikali pia imeendeleza juhudzi za kuwarudisha wakimbizi makwao ambapo kati ya Julai, 2005 na Machi, 2006 jumla ya wakimbizi 230,000 walirejeshwa makwao. Nawaagiza viongozi wa Mikoa, Wilaya na Vijiji kwa kushirikiana na Wizara husika kuimarisha udhibiti wa mipaka yetu ili kuzuia uingiaji haramu wa mifugo na wageni.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, matukio ya ujambazi ya kutumia silaha yaliongezeka katika baadhi ya Mikoa nchini. Matukio hayo yamehusisha zaidi mabenki na maduka ya fedha. Kiasi kikubwa cha fedha kiliibwa na baadhi ya watu kupoteza maisha au kujeruhwa. Serikali imechukua hatua madhubuti za kukabiliana na ujambazi na matukio mengine ya uhalifu na ujambazi na matukio mengine ya uhalifu nchini. Baadhi ya hatua hizo ni pamaja na kuundwa kwa Wizara mpya ya Usalama wa Raia, kufanya mabadiliko makubwa ya safu za uongozi na utendaji ndani ya Jeshi Jeshi la

Polisi na kuliongezea vitendea kazi. Vile vile, kumekuwa na matukio ya ajali za barabarani ambazo zimesababisha vifo vingi, majeruhi na upotevu wa mali.

Taarifa zinaonyesha kuwa, nyingi ya ajali hizo zimetokana na mwendo wa kasi, kuzidisha abiria na uzembe wa kutozingatia sheria. Serikali imelielekeza Jeshi la Polisi kuimarisha doria na ukaguzi wa magari yote na kusimamia kikamilifu Sheria za Usalama barabarani. Katika mwaka 2006/2007, Serikali itatekeleza mikakati mingine ya muda mfupi na mrefu ili kuliwezesha Jeshi la Polisi kufanya kazi zake kwa ufanisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani zangu za dhati kwa wote wanaolitakia mema Taifa letu kwa ushirikiano mkubwa walioutoa kusaidia Serikali kuwafichua wanaojihusisha na uhalifu nchini. Serikali pia inawahakikishia ulinzi na usiri mkubwa wale wote wanaotoa taarifa hizo. Dhana ya ushirikiano kati ya wananchi na Vyombo vyta Ulinzi na Usalama, katika suala la ulinzi limepokelewa kwa ari mpya na kasi mpya. Tumepokea taarifa nyingi zinazohusu uhalifu na tunaendelea kuzifanyia kazi. Hatua za kisheria zitachukuliwa kwa wote watakaothibitika kujihusisha na uhalifu ikiwa ni pamoja na baadhi ya Watendaji wanaokiuka maadili yao ya kazi.

Mheshimiwa Spika, Udhibiti wa Dawa za Kulevya. Nchi yetu imeendelea kukumbwa na tatizo la matumizi na uingizaji wa dawa za kulevya. Katika kipindi cha mwaka 2005/2006, kumekuwa na ongezeko la ukamataji wa dawa za kulevya. Dawa za kulevya za aina mbalimbali zilikamatwa na jumla ya watuhumiwa 4,532 walikamatwa na kesi 3,368 zilifunguliwa Mahakamani. Tume ya kuratibu udhibiti wa dawa za kulevya imeendelea kuratibu shughuli zote zinazofanywa na wadau mbalimbali yakiwemo Mashirika yasiyo ya Kiserikali, Vyombo vyta Dola na Asasi mbalimbali. Katika kuongeza mbinu za kupambana na tatizo hilo, Serikali inaandaa Sera ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya na kuanza mchakato wa kuifanyia marekebisho Sheria ya Dawa za Kulevya Na. 9 ya mwaka 1995.

Katika mwaka 2006/2007, Serikali itaendelea kukuza uelewa wa Umma kuhusu matatizo yatokanayo na matumizi pamoja na biashara ya dawa za kulevya, kuelimisha wananchi juu ya uhusiano wa dawa za kulevya na maambukizi ya virusi vyta UKIMWI. Aidha, itashirikiana na wadau wengine katika kudhibiti dawa za kulevya na utoaji wa huduma za matibabu na ushauri nasaha kwa waathirika. Vile vile, mafunzo na vitendea kazi vitatolewa kwa Vyombo vyta Dola kama Polisi, Uhamiaji na Forodha ili kuviwewesha kupambana kikamilifu na uhalifu wa dawa za kulevya.

Mheshimiwa Spika, Utawala Bora. Ili kujenga Taifa linaloongozwa kwa misingi ya haki na utawala bora, Serikali imeendelea kutekeleza programu ya Kisekta ya kurekebisha na kuboresha mfumo wa sheria chini ya mkakati wa muda wa kati mwaka 2005/2006 na mwaka 2007/2008. Madhumuni ya Mkakati huo ni kuhakikisha kuwa upo utoaji wa haki wenye ufanisi nchini na utawala wa haki wenye ufanisi nchini na utawala wa sheria kwa kutoa haki na kwa wakati. Mkakati huo utaboresha maeneo ya sheria, kanuni na taratibu za nchi yetu.

Katika mwaka 2006/2007, Serikali itaendelea kutekeleza majukumu yake ya kusimamia utoaji wa haki kwa wananchi na kuhakikisha taratibu zinafuatwa katika masuala ya mikataba na kisheria. Aidha, Serikali itaziwezesha Mahakama kutekeleza majukumu yake ili kupunguza mlundikano wa kesi Mahakamani na wa Mahabusu Magerezani. Serikali pia itaboresha mfumo wa huduma za kisheria, kufanya utafiti na kuzipitia sheria zilizopitwa na wakati na kuandaa Miswada. Kazi zote hizi zitafanyika kwa kuishirikisha jamii katika kuendesha shughuli za kisheria.

Mheshimiwa Spika, Serikali vile vile itaendeleza kwa kasi vita dhidi ya rushwa. Ili kuziba mianya ya rushwa katika Utumishi wa Umma, Serikali kwa kushirikiana na Wahisani na Mashirika ya yasiyo ya Kiserikali, itahakikisha mkakati wa kitaifa wa kupambana na rushwa na mipango mingine ya utawala bora inatekelezwa. Katika mwaka 2006/2007, awamu ya pili ya utekelezaji wa mkakati wa Taifa wa kupambana na rushwa utakaozihusisha Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji na Sekta Binafsi utaanza. Serikali itaimarisha Taasisi ya Kuzuia Rushwa ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Napenda kusisitiza kuwa Serikali haitakuwa na suluhu na wale watakaobainika kujihusisha na vitendo vya rushwa. Kama kuna aliyeponyoka kubanwa huko nyuma, basi ni vyema sasa akabadilika kwa kufungua ukurasa mpya wa maisha.

Mheshimiwa Spika, Watumishi wa Umma wanatoa mchango mkubwa katika kuwezesha Serikali kutekeleza majukumu yake inavyostahili. Kwa kuzingatia hilo, Viongozi Wakuu wa Serikali wakiongozwa na Mheshimiwa Rais, walifanya Semina elekezi iliyofanyika Ngurdoto, Arusha mwezi Machi, 2006 ili kutoa dira na mwelekeo wa uongozi wa Serikali. Kila kiongozi anawajibika kutekeleza wajibu wake kwa kuzingatia maelekezo ya Mkutano huo. Lengo ni kuufanya Utumishi wa Umma uendeshwe kwa misingi ya utawala bora utakaowezesha Tanzania kuwa nchi yenye uchumi endelevu wenye kuleta matumaini ya kutokomeza umaskini. Semina elekezi kama hizi zitafanyika pia kwa viongozi wa Mikoa na Wilaya.

Mheshimiwa Spika, Sekretarieti za Mikoa zimeanzishwa kwa Sheria ya Tawala za Mikoa Na. 19 ya mwaka 1997 ambayo inafanua wajibu wa Mikoa katika kuzijengea Halmashauri uwezo wa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kutoa ushauri wa kitaalam kwa Halmashauri ili ziweze kutoa huduma bora kwa wananchi; vile vile, kuhakikisha kwamba kunakuwepo amani na utulivu katika Mikoa; kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya Serikali na Sera za Kisekta katika Halmashauri. Ili kutekeleza majukumu hayo, katika mwaka 2005/2006, Serikali imeandaa programu ya miaka mitano ya kukuza uwezo wa Sekretarieti za Mikoa 2005 – 2010. Chini ya Programu hiyo, muundo wa Sekretarieti hizo unapitiwa upya ili uweze kukidhi mahitaji ya sasa. Vitendea kazi vitanunulia na mafunzo yenye lengo la kuwajengea uwezo wa kufanya kazi kwa umahiri na umakini yataendeshwa. Katika mwaka 2006/2007 Serikali itaendelea kutekeleza programu hiyo na kuhuisha muundo wa Sekretarieti za Mikoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuziimarisha Serikali za Mitaa ili ziwe vyombo shirikishi vya wananchi vinavyotekeliza majukumu yake kwa ufanisi na uadilifu wa kiwango cha juu na vinavyowajibika kikamilifu kwa wananchi. Mkakati ambao Serikali inatumia katika kuboresha mfumo wa Serikali za Mitaa ni kupeleka madaraka,

majukumu na rasilimali zaidi kutoka Serikali Kuu hadi kwa wananchi kupitia Serikali zao za Mitaa.

Chini ya Mkakati huo, madaraka yanayopelekwa kwa wananchi kupitia Serikali za Mitaa ni pamoja na madaraka ya kufanya maamuzi ya kisiasa katika mambo ambayo hadi sasa yamekuwa yakiamuliwa katika ngazi mbalimbali za Serikali Kuu na kuweka jukumu la kutoa huduma mbalimbali za msingi kwa Serikali za Mitaa.

Pamoja na kuwepo mgawanyo huo wa majukumu, Serikali Kuu ndiyo inayowajibika kwa ujumla kwa wananchi katika kuhakikisha kuwa huduma zinawafikia wananchi na zina ubora wa kiwango kinachostahili. Kwa sababu hiyo, ni muhimu Serikali Kuu na Serikali za Mitaa kuingia katika Mikataba ya kiutendaji. Utekelezaji wa Mikataba hiyo utahakikisha pande zote mbili zinawajibika kisheria na zinatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Katiba, Sera za Kitaifa, Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali. Utaratibu huo utaanza kutumika mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, Mikataba ya kiutendaji itaziwezesha Serikali Kuu na Serikali za Mitaa kukabiliana na matatizo ya udhaifu mkubwa wa ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri, upungufu mkubwa wa uwajibikaji na uadilifu, udhaifu wa usimamizi kwa upande wa Madiwani na ulegevu katika utekelezaji wa majukumu ya Halmashauri ambapo maamuzi ya Mabaraza hayasimamiwi ipasavyo. Aidha, itawezesha kukabiliana na udhaifu katika kusimamia sheria na sheria ndogo kunakosababisha matatizo mbalimbali kama vile uchafuzi wa mazingira na ujenzi holela wa nyumba. Ushauri wa Waheshimiwa Wabunge katika kutekeleza shughuli za Serikali za Mitaa ni muhimu sana, kwani kwa mujibu wa sheria, Wabunge nao ni Madiwani katika Halmashauri. (*Makofi*)

Kupitia Bunge hili Tukufu, natoa wito maalum kwa Waheshimiwa Wabunge kwa nafasi yao ya Udiwani wajihishe zaidi na shughuli za Serikali za Mitaa katika Majimbo yao. Aidha, ratiba za Vikao vya Halmashauri nazo zipangwe kwa namna ambayo inamwezesha Mbunge kushiriki kwenye Vikao hivyo. Matarajio ya Watanzania kwa Serikali yanategemea jinsi Serikali za Mitaa zitakavyotekeliza majukumu yake. Serikali haitasita kuchukua hatua zinazofaa kurekebisha utendaji kazi katika Halmashauri inayolegalega kutimiza wajibu wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, matumizi ya mapato ya Halmashauri kutoka vyanzo vyake yanahitaji kusimamiwa kwa uadilifu mkubwa kwa mujibu wa Kanuni za Fedha. Aidha, Halmashauri zote zinatakiwa kufunga vitabu na kuwasilisha kwa Wakaguzi kwa wakati. Kwa mujibu wa Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, inayoishia Juni, 2005 kati ya Halmashauri 117, Halmashauri 62 zilipata hati safi, Halmashauri 51 zimepata hati yenye masharti na nne zilipata hati chafu. Serikali itaendelea kufuatilia kwa karibu ili kuhakikisha fedha zinazotumika katika Halmashauri zinawiana na ubora wa kazi inayofanyika. Nachukua nafasi hii kuzipongeza Halmashauri zilizopata hati safi na kuziagiza Halmashauri nyingine kuchukua hatua za haraka kurekebisha utunzaji na uandikaji wa vitabu vya hesabu kwa mujibu wa Kanuni za Fedha na Serikali na kuboresha utendaji ndani ya Halmashauri hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza mradi utakaoziwezesha Serikali za Mitaa kupata fedha zaidi kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Mradi huo unagharamiwa kwa pamoa na fedha za mkopo kutoka Benki ya Dunia, mchango wa Serikali Kuu na Halmashauri husika. Kupitia mradi huo, Serikali za Mitaa zitapatiwa ruzuku ya maendeleo kwa kazi zifuatazo:-

- (i) Kutekeleza miradi ya miundombinu itakayobuniwa kwa kuwashirikisha wananchi na kuzijengea Halmashauri uwezo wa kutekeleza mradi kwa ufanisi.
- (ii) Kuboresha miundombinu katika Manispaa za Jiji la Dar es Salaam, zikiwemo barabara, mifereji ya maji ya mvua, taa za barabarani, barabara na madaraja ya waenda kwa miguu, vizimba vyta taka ngumu katika maelezo ya makazi duni, kuboresha ukusanyaji wa mapato na utekelezaji wa programu ya afya na usafi ngazi ya kaya.
- (iii) Kuijengea uwezo Wizara yenye dhamana ya Serikali za Mitaa ili iweze kusimamia utekelezaji wa mradi na kuziwezesha Halmashauri kutimiza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, chini ya utaratibu huo, hadi mwezi Aprili, 2005 jumla ya Shilingi bilioni 22.7 zimetolewa kwa Halmashauri 66 zilizofuzu kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo na Shilingi bilioni 2.2 kwa Halmashauri 113 kwa ajili ya kuzijengea uwezo wa kiutendaji. Zaidi ya miradi midogo midogo 1,000 ya maendeleo katika Halmashauri mbalimbali imetekelizwa au ipo katika hatua za mwisho za utekelezaji kutokana na fedha za ruzuku ya maendeleo zilizopelekwa. Miradi hiyo ni katika Sekta za Barabara, Elimu, Afya, Maji na Kilimo. Natoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge kujihusisha kikamilifu katika upangaji na utekelezaji wa mradi huo wenye lengo la kuleta maendeleo kwa wananchi na kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuzijengea uwezo Halmashauri kwa kuzipatia ruzuku isiyo na masharti kwa ajili ya fidia kwa vyanzo vyta mapato vilivyofutwa. Katika mwaka 2005/2006, Serikali ilitenga Shilingi bilioni 40.1 kama ruzuku bila masharti. Aidha, kuanzia Julai, 2005 hadi Machi, 2006, Halmashauri zimekusanya kutoka vyanzo vyake vyta mapato jumla ya Shilingi bilioni 37.1 sawa na asilimia 78.6 ya lengo la Shilingi bilioni 47.2. Katika Mwaka wa Fedha 2006/2007, Serikali imetenga jumla ya Shilingi bilioni 43.1 kama ruzuku kwa Halmashauri. Halmashauri zinatarajia kukusanya Shilingi bilioni 71.3 kutoka katika vyanzo yake vyta mapato.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua upungufu wa Watumishi wenye sifa zinazotakiwa katika Serikali za Mitaa. Ili kukabiliana na tatizo hilo, Serikali itafanya tathimini ili kufahamu mahitaji halisi ya watumishi katika Serikali za Mitaa kwa kulinganisha na uzito wa kazi uliopo. Serikali itajiri watumishi wapya katika Sekta ya Afya na Elimu moja kwa moja kutoka Vyoni kwa waliofuzu mafunzo yao bila kufanyiwa usaili. Vile vile, Serikali itahuisha mishahara ya wafanyakazi wa Serikali za Mitaa ili ilingane na mishahara ya Watumishi wa Serikali Kuu.

Kwa upande wa Watendaji wa Vijiji na Mitaa, hadi kufikia mwezi Machi, 2006, jumla ya Maafisa Watendaji wa Vijiji 7,651 na Maafisa Watendaji wa Mitaa 1,183 wameajiriwa. Kuanzia mwaka wa 2006/2007, mishahara ya Maafisa Watendaji wa Vijiji na Mitaa imetengwa katika Bajeti za Halmashauri. Hivyo, kila Halmashauri inao wajibu wa kuhakikisha kuwa inazo takwimu sahihi za Maafisa Watendaji wa Vijiji na Mitaa na kuwalipa kwa wakati mishahara yao kutokana na Bajeti iliyotengwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, maendeleo Vijijini, ushirikishwaji wa wananchi katika utekelezaji na usimamizi wa masuala yanayohusu maendeleo yao ni msingi mkubwa wa kuwawezesha kubadili maisha yao. Ili kuhakikisha ushirikishwaji huo unakuwepo, Serikali imeanzisha Mfumo wa Upangaji Mipango Shirikishi Jamii wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo. Katika mwaka 2005/2006 Halmashauri 78 zimefanikiwa kueneza mfumo huo katika kila Kijiji na Mtaa. Katika mwaka 2006/2007, Serikali itaziwezesha Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri kufuatilia utekelezaji wa mipango ilioibuliwa. Vile vile, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo na wananchi itawezesha kuenezwa kwa mfumo huo katika Halmashauri zote.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imeendelea kutekeleza programu na miradi mbalimbali inayolenga kuwawezesha wananchi hususan wanaoishi Vijijini kuongeza pato na kuwa na uhakika wa chakula. Moja ya programu hizo ni ile ya uendelezaji wa mifumo ya masoko ya mazao ya kilimo. Programu hii itagharimu Dola za Kimarekani milioni 42.5 na itatekelezwa katika Wilaya 38 za Mikoa minane nchini ambazo pamoja na kupata mavuno mazuri zinakabiliwa na tatizo kubwa la masoko ya mazao ya kilimo. Mikoa hiyo ni pamoja na Arusha, Manyara, Kilimanjaro, Tanga, Iringa, Mbeya, Rukwa na Ruvuma. (*Makofi*)

Programu hii inalenga kuimarisha mifumo ya masoko ya mazao ya kilimo ambayo itawezesha kupatikana kwa masoko ya uhakika na hivyo kuinua maisha ya wananchi. Aidha, inafanya kazi ya kuunda au kuimarisha vikundi vya wazalishaji, wafanyabiashara na wasindikaji wadogo na wa kati. Hadi hivi sasa kuna zaidi ya vikundi 660 ambavyo viko katika hatua mbalimbali za kufundishwa na kuimarishwa kibiashara. Idadi hii imejumuisha wafanyabiashara wadogo wa mazao ya kilimo, wasindikaji na wazalishaji katika Wilaya 20 za mwanzo. Vile vile, programu inaziwezesha Halmashauri kuboresha miundombinu inayohusiana na masoko ya mazao ya kilimo kama barabara za Vijiji na masoko ili kuhamasisha mwingiliano baina ya wazalishaji, wasindikaji na Wafanyabiashara Vijijini.

Mheshimiwa Spika, programu hiyo pia imeanzisha mfumo wa stakabadhi za mazao kwenye maghala ili kuwawezesha na kuwanufaisha wakulima wadogo, kuitia kwenye vikundi/Vyama vya Ushirika au wazalishaji kutoka Asasi za Fedha. Mfumo wa Stakabadhi za Mazao kwenye maghala ya kuhifadhia mazao mbalimbali ya kilimo. Utaratibu huu huwapa uwezo wa kisheria watanza maghala hayo kutoa Stakabadhi kwa wakulima au wafanyabiashara wa mazao ya kilimo watakaotunza mazao yao kwenye maghala. Stakabadhi hizo hujulikana kama Stakabadhi za Maghala. Stakabadhi hizo zina hadhi na thamani kama zilizonazo nyaraka za fedha kama vile hundi. Kwa kutumia

Stakabidhi hizo, wakulima watapata mikopo kwenye Asasi ya Fedha kwa kuziweka rehani.

Chini ya utaratibu huu, katika mwaka 2005/2006, jumla ya Shilingi milioni 120 zilikopeshwa kwa wakulima waliowekewa mazao yao ghalani na Mabenki ya CRDB na *Exim* katika maeneo yao ya majoribio ya Chimala Mkoani Mbeya na Magugu na Quash Mkoani Manyara. Wakulima wote waliokopa wamerejesha mikopo yote kwa asilimia mia moja na wamekiri kupata faida ya zaidi ya asilimia 100 kutokana na mfumo huo. Ningependa kutumia nafasi ya kuwepo Balozi George Kahama, kumpongeza, maana ndiye aliyeanzisha utaratibu huu alipokuwa Waziri wa Ushirika na Masoko. Hivyo, natoa wito kwamba juhudhi hizo ziendelezwe ili mfumo huo upanuliwe katika maeneo mengi zaidi nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile Serikali inatekeleza programu ya huduma za fedha Vijijini. Programu ya huduma za fedha Vijijini, itagharimu Dola za Kimarekani milioni 23.8 na inatekelezwa katika Halmashauri za Wilaya 22. Halmashauri hizo ni hizi zifuatazo: Sumbawanga Vijijini, Nkasi, Mbeya Vijijini, Mbarali, Rungwe, Kyela, Mbozi, Mufindi, Njombe, Namtumbo, Songea Vijijini, Mbanga, Dodoma Vijijini, Kondoa, Mpwapwa, Singida Vijijini, Iramba, Manyoni, Moshi Vijijini, Mwanga, Rombo na Same. Programu hii inalenga kuwawezesha wakulima wadogo au kaya zenyenye kipato kidogo kujiunga pamoja na kuanzisha vikundi imara vya kuweka akiba na kukopa. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2006, vikundi 86 vyenye wanachama 43,157 vilikuwa vimeimarishwa.

Amane zimeongezeka kutoka Shilingi milioni 269.7 mwaka 2002 hadi Shilingi bilioni 3.7 mwaka 2006. Hadi mwezi Aprili, 2006 vikundi vimeweza kukopesha jumla ya Shilingi bilioni 7.1 kwa wanachama wao na marejesho yamekuwa zaidi ya asilimia 90. Aidha, baadhi ya vikundi vilivyoimarika vimeanza kupata mikopo kutoka Benki ili viweze kuwakopesha wanachama wake kufanya shughuli mbalimbali za kiuchumi ikiwa ni pamoja na kununulia pembejeo za kilimo. Uzoefu wa program hiyo unaonyesha kuwa kuna uwezekano mkubwa wa wananchi kujiwekea akiba Vijijini. Kwa hiyo, natoa wito kwa wananchi kujiunga na Vyama vya Akiba na Mikopo ili waweze kupata mikopo na kuanzisha miradi ya kujiongezea kipato.

Mheshimiwa Spika, moja ya ahadi kubwa za CCM kwa wananchi ni kushughulikia tatizo la ajira nchini hasa kwa vijana na wanawake. Mkakati wa awali wa kutuwezesha kutekeleza ahadi hii ni kutekeleza kwa dharti Sera ya uwekezaji wa wananchi kiuchumi, mpango wa kurasimisha biashara na mali za wanyonge Tanzania (MKURABITA) na programu nyingine kama vile Mfuko wa Maendeleo ya Jamii. Katika kutekeleza sera, mikakati na programu hizo, napenda kusisitiza kuwa eneo la kujiajiri binafsi ndilo lenye nafasi nyingi za ajira katika nchi yetu.

Aidha, maeneo yenye fursa za kujiajiri ni kilimo, ufugaji, uvuvi, viwanda, biashara, ukandarasi, ualimu na uchimbaji madini. Lengo ni kuona kila Mtanzania anashiriki kikamilifu katika kukuza uchumi na kuondoa umaskini. Ili kutekeleza azma hiyo, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu, kuwa Serikali katika mwaka 2006/2007,

imetenga wastani wa Shilingi milioni 500 kwa kila Mkoa kuitia Benki zilizopo kwa ajili ya uwezeshaji wa wananchi kiuchumi na kuongeza ajira nchini. Imetenga Shilingi milioni 500 kwa riba maalum kwa ajili ya uwezeshaji wa wananchi kiuchumi na kuongeza ajira nchini. (*Makofi*)

Fedha hizo zitatolewa kwa mtu mmoja mmoja au vikundi kwa njia ya mikopo yenye masharti nafuu kwa kutumia taratibu za kibenki kulingana na uwezo wa kibashara wa mwombaji. Narudia! “Hatutafuata riba, zilizopo ni riba maalum ya kuwawezesha wananchi kujipatia ajira.” Serikali inakusudia kuunda Bodi ya kusimamia mikopo hiyo na Waheshimiwa Wabunge watashirikishwa kikamilifu. Aidha, Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana na Uongozi wa Mikoa ziandae kanuni na taratibu za kuweshera wananchi wengi kunufaika na mpango huo na utaratibu huo uanze haraka iwezekanavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma iliundwa kwa mujibu wa Sheria kwa tamko la Rais Na. 230 la mwaka 1973 na kupewa majukumu ya kupanga, kupima, kugawa na kusimamia uendelezaji wa ardhi kwa lengo la kufanikisha mpango wa uendelezaji Mji Mkuu Dodoma. Kutokana na ufinyu wa Bajeti ya miaka iliyopita, Mamlaka haikuweza kutekeleza majukumu yake kwa kasi kama ilivyokusudiwa. Katika mwaka 2005/2006, Mamlaka iliendelea na matayarisho ya mipango ya uendelezaji wa maeneo ya makazi ya Itega na Nzuguni yenye zaidi ya viwanja 6,500. Aidha, mamlaka iliendelea kutekeleza kazi za uimarishaji na utunzaji wa maeneo ya misitu ya zaidi ya hekta 20,000 na utunzaji wa mifereji mikuu ya mvua. Vile vile, mamlaka ilikamilisha awamu ya kwanza ya uendelezaji wa Bustani ya Mwalimu Nyerere, katikati ya Mji wa Dodoma, eneo ambalo litatumika kama kumbukumbu ya kuenzi juhud za Mwalimu Nyerere katika maendeleo ya Taifa letu.

Katika mwaka 2006/2007, mamlaka itaendelea na usimamiaji na utekelezaji wa majukumu yake ikiwa ni pamoja na kukamilisha kupima eneo la hekta 4,000 kwenye eneo la Chimwaga kwa ajili ya ujenzi wa Chuo Kikuu kipycha Serikali cha Dodoma.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, Serikali iliendelea kutekeleza Sera ya Menejimenti ya Maafa inayoweka umuhimu mkubwa katika usalama wa maisha ya watu na mali zao kwa kuhakikisha kuwa athari za kiuchumi na kijamii zinapunguzwa kwa kiasi kikubwa. Kamati za Maafa za Mikoa yote zimeundwa.

Aidha, mafunzo yametolewa kwa Kamati za Maafa za Mikoa na Wilaya katika Mikoa mitano ya Mtwara, Lindi, Tanga, Pwani na Mwanza. Serikali pia imeendelea kuhamasisha Umma juu ya Menejimenti ya Maafa kuitia vipindi vya radio, kutoa makala katika magazeti, uchapishwaji wa Kalenda zenye ujumbe wa maafa na usambazaji wa video na kanda zenye nyimbo za kuhamasisha Umma.

Kwa kuzingatia Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu upunguzaji maafa duniani, Serikali imeunda Kamati za Kitaalam zinazohusisha wadau mbalimbali za kushauri na kufuatilia masuala ya maafa ya aina mbalimbali. Lengo la Kamati hizo ni kujenga uwezo

wa nchi katika kupunguza athari za maafa kwa kuingia mikakati ya Kamati hizo katika mipango ya maendeleo ya nchi yetu.

Katika mwaka 2006/2007, Serikali itakamilisha marekebisho ya msingi katika Sheria Na. 9 ya mwaka 1990 ya uratibu wa utoaji wa misaada ya maafa. Muswada wa Marekebisho hayo utawasilishwa katika Bunge lako Tukufu ili kukidhi mahitaji ya Sera ya Taifa ya Menejimenti ya Maafa ya mwaka 2004. Kuanzishwa kwa Tume, kutaiwezesha Serikali kushughulikia kikamilifu masuala ya maafa nchini.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni moja ya nchi zilizoathirika na ugonjwa wa Ukimwi. Inakadiriwa kuwa nchi yetu hadi sasa ina watu milioni 2.5 ambaao tayari wameambukizwa virusi vya Ukimwi. Aidha, inakadiriwa kwamba kuna watoto yatima wapatao milioni 2.5 nchini. Ukimwi umeenea Mijini na Vijiji na kila mmoja wetu sasa ameatheririka kwa njia moja au nyingine kwa kuhusisha ndugu, jamaa na marafiki ambaao wamepoteza maisha yao. Katika kipindi cha mwaka 2005/2006, Tume ya Kudhibiti Ukimwi iliweka mikakati mbalimbali ya kupambana na ugonjwa wa Ukimwi na kuelekeza sehemu kubwa ya Bajeti yake katika Sekta ya Umma kuzuia na kupunguza kasi ya maambukizo.

Aidha, vikundi mbalimbali vya kijamii yakiwemo Mashirika yasiyo ya Kiserikali na ya watu waishio na virusi vya Ukimwi yalipata fedha kwa ajili ya kusaidia wenye Ukimwi ikiwa ni pamoja na kununulia dawa za kurefusha maisha. Jumla ya waathirika 27,000 wanapewa dawa za kurefusha maisha.

Katika mwaka 2006/2007, Tume ya kudhibiti Ukimwi ilitoa elimu kwa wananchi Mijini na Vijiji. Tume pia itaweka kipaumbele katika kutoa miongozo, elimu na nyenzo zaidi kwa jamii, kuhudumia yatima na kuhakikisha kwamba kila Halmashauri ina mipango ya kukabiliana na Ukimwi, lakini vile vile ina utaratibu wa kusaidia yatima walioko humu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukuaji wa Sekta ya Kilimo bado siyo wa kuridhisha kwa mfano, katika miaka mitano kuanzia mwaka 2001 hadi mwaka 2005 Sekta ya Uzalishaji mali imekua kwa wastani wa asilimia 5.1 tu. Ili kuwezesha kilimo kukua kwa kiwango kikubwa zaidi, Serikali imeanza kutekeleza programu ya kuendeleza Sekta ya Kilimo. Programu hiyo ina lengo la kuweka mazingira bora ya uwekezaji hususan katika Sekta Binafsi ili kuongeza tija na faida katika kilimo.

Serikali itaendelea kuchukua hatua mbalimbali zinazolenga kumwezesha mkulima kuongeza tija, wingi na ubora wa mazao ya asili ya biashara ili kilimo kitoe mchango mkubwa zaidi katika vita dhidi ya umaskini. Hatua hizo ni pamoja na kuimarisha huduma za ugani, huduma za masoko na kuwapatia zana za kilimo na pembejeo, yaani mbolea, mbegu bora na madawa ya kilimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, uzoefu tuliuopata wakati wa kipindi cha ukame, unaonyesha kuwa hatuna budi kukipa kipaumbele kilimo cha umwagiliaji maji kama mkakati wa

kukabili ana ukame kwa siku zizazo. Kwa kutambua hivyo, katika mwaka 2006/2007, Serikali itatoa kipaumbele katika ujenzi na ukarabati wa skimu na mabwawa na ujenzi wa miradi mipyaa hasa inayoweza kuendelezwa na wananchi wenyewe kwa gharama nafuu.

Vile vile, mkazo utawekwa katika matumizi ya teknolojia ya uvunaji wa maji ya mvua katika Mikoa mbalimbali. Ili kuendeleza kilimo cha umwagiliaji maji, kuanzia sasa, Halmashauri za Wilaya zinatakiwa ziweke shughuli za kilimo cha umwagiliaji katika Mipango yao ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya. Aidha, zihamasishe Sekta Binafsi kuwekeza katika usanifu na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji. Serikali itatoa kipaumbele katika kuwajengea uwezo wataalamu na wakulima katika kilimo cha umwagiliaji, upatikanaji wa pembejeo na zana za kilimo.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha Sekta ya Mifugo, Serikali imeendelea kusambaza mifugo bora katika mashamba ya Serikali. Serikali ilizalisha mitamba 734 na kusambazwa kwa wafugaji wadogo katika Mikoa 15 ya Tanzania Bara ikilinganishwa na mitamba 611 katika msimu uliotangulia. Uzalishaji wa nyama uliongezeka kutoka tani 378,509 mwaka 2004/2005 hadi tani 388,294 mwaka 2005/2006.

Kwa upande wa uendelezaji wa miundombinu na masoko ya mazao ya mifugo, machinjio manne ya kisasa yalijengwa katika Manispaa ya Dodoma na katika maeneo ya Mkusa Mkoani Pwani, Nkundi Mkoani Rukwa na Mvomero Mkoani Morogoro. Ukarabati wa masoko ya mifugo Mikoa ya Kusini na Kaskazini unaendelea. Katika mwaka 2006/2007, Serikali itaendelea kusimamia na kuendeleza huduma za ugani kwa kuzingatia kanuni za ufugaji bora na endelevu na zisizoharibu mazingira. Aidha, Serikali itasisitiza ufugaji wenyewe kuongeza tija kwa lengo la kuongeza kipato cha mfugaji.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, Serikali iliendelea kutekeleza Programu ya Mageuzi na *Modernisation* ya Ushirika nchini. Chini ya Programu hiyo, Serikali ilisimamia kwa karibu marekebisho ya uendeleshaji wa Vyama vya Ushirika vya Msingi ili viweze kufanya shughuli zake kibiashara na kuweka uhusiano sahihi kati ya Vyama vya ngazi hiyo na vya ngazi ya juu vitakavyoundwa kulingana na mahitaji ya wanachama wenyewe. Serikali itaendelea na jukumu la kuimarisha uongozi na kujenga maadili mema ya utendaji ndani ya Vyama vya Ushirika. Aidha, Serikali itaendelea kuimarisha *SACCOS* nchini kwa kuziwesha kufanya chaguzi za Viongozi wapya na wenyewe sifa zinazokubalika na kuajiri Watendaji wenyewe ujuzi wa masuala ya biashara na usimamizi wa fedha.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2005/2006, Serikali iliendelea na utekelezaji wa Sera endelevu ya Viwanda. Malengo ya Sera hiyo yameweka mkazo katika kuendeleza viwanda vya usindikaji wa mazao ya kilimo ili kuongeza thamani, upatikanaji wa masoko na hivyo kukuza mapato kwa wakulima. Ongezeko la usindikaji wa mazao nchini utawawezesha wakulima wetu kupata masoko ya ndani zaidi kuliko yale ya nje ambayo yamekuwa na bei za kubadilika mara kwa mara.

Vile vile, Serikali iliendelea kutekeleza Sera ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo kwa kuweka kipaumbele katika kuwahamasisha wananchi wa kipato cha chini

kuanzisha miradi midogo midogo vikiwemo viwanda vya kukamua mafuta ya kula, samani, kusindika matunda, ufumaji na ushonaji wa nguo.

Serikali pia imeanza kutenga maeneo maalum ya uwekezaji wa viwanda kama vile *Benjamin William Mkapa Special Economic Zone* iliyoko Mabibo Dar es Salaam na kiwanda cha Nguo cha A-Z kilichoko Kisongo pale Arumeru, Arusha.

Mheshimiwa Spika, kutokana na sera na mipango hiyo, Sekta ya Viwanda iliendelea kuwa na mafanikio ya kuridhisha na uzalishaji wa bidhaa katika viwanda vyetu uliongezeka. Kwa mfano, uzalishaji wa bidhaa za saruji uliongezeka kutoka tani milioni 1.3 mwaka 2004 hadi tani milioni 1.4 mwaka 2005, sawa na ongezeko la asilimia 7.3. Uzalishaji wa sukari ulikuwa tani 268,772 mwaka 2005 ikilinganishwa na tani 209,859 mwaka 2004 sawa na ongezeko la asilimia 28.1. Uzalishaji wa bia pia ulikuwa lita milioni 216.6 mwaka 2005, ikilinganishwa na lita milioni 203.2 mwaka 2004 sawa na ongezeko la asilimia 6.6 na uzalishaji wa sigara ulikuwa milioni 4,445 mwaka 2005 ikilinganishwa na sigara milioni 4,220 mwaka 2004 sawa na ongezeko la asilimia 5.3.

Katika mwaka 2006/2007, Serikali iliendelea kuhimiza uenezaji wa teknolojia ya kisasa katika viwanda mbalimbali. Aidha, Serikali itaweka kipaumbele ili kufufua viwanda vilivyopo na kuboresha zaidi mazingira ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Madini inakabiliwa na migogoro kuhusu umiliki wa maeneo ya uchimbaji na mahusiano mabaya kati ya wachimbaji madini. Ili kuondokana na migogoro hiyo, Serikali imeanza kuchukua hatua za kuhakikisha kuwa tunajenga mfumo bora wa utoaji na usimamizi wa leseni za madini.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Wachimbaji wadogo wadogo, Serikali imeandaa mkakati mpya na programu ya kuwaendeleza. Mkakati huo unalenga kufanikisha upatikanaji wa maeneo, kuimarisha na kuunganisha nguvu katika utoaji wa mafunzo ya ufundi na ujasiriamali, kuhamasisha na kueneza matumizi ya teknolojia bora na salama na kuweka mfumo wa kutathmini kijiolojia maeneo ya wachimbaji wadogo ili kuwaongoza katika maeneo ya kuchimba, kushawishi wachimbaji wadogo na wafanyabiashara wadogo kuijunga katika vikundi ili waweze kuendelezwa kwa urahisi na kufanikisha upatikanaji wa mikopo kutoka kwenye Taasisi za Fedha.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, Serikali itajenga mazingira bora ya kuongeza thamani ya madini kwa kuweka mfumo wa masoko ya kushindanisha wanunuvi katika maeneo ya uchimbaji, kuboresha usimamizi na uratibu wa shughuli za uchimbaji mdogo na kujenga mfumo bora wa utoaji wa leseni za madini. Aidha, nitachukua hatua za kuhakikisha kuwa tunajenga mfumo bora wa utoaji na usimamizi wa leseni za madini.

Nachukua nafasi hii kuwahimiza wawekezaji wa ndani kushiriki kikamilifu katika utoaji huduma muhimu kwenye migodi mikubwa kama vile ulipuaji wa miamba, huduma za chakula, usafiri, mafuta na vilainishi vya mitambo. Hivi sasa huduma hizo zinatolewa na Kampuni za kigeni. Uzoefu wa nchi za Botswana, Sri Lanka na Afrika Kusini

unaonyesha kwamba zinafaidika na shughuli za aina hiyo. Hii ni fursa kwa Kampuni za ndani kuongeza kipato na kuongeza ajira.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutoa miongozo ya kisera ili kuboresha na kuendeleza Sekta za Ujenzi, Uchukuzi, Mawasiliano na Hali ya Hewa nchini. Katika mwaka 2005/2006, Serikali iliendelea kuimarisha miundombinu na huduma ya uchukuzi kwa njia ya barabara, reli, maji, usafiri wa anga kwa kuzingatia maelekezo ya Sera ya Taifa ya Uchukuzi na Sera ya Taifa ya Ujenzi.

Kwa upande wa Halmashauri, fedha za mfuko wa barabara zilizotengwa kwa mwaka 2005/2006 ni Shilingi bilioni 23.8 kwa ajili ya kutengeneza barabara zeny urefu wa kilomita 9,497. Hadi kufikia mwezi Mei mwaka huu fedha kiasi cha Shilingi bilioni 17.4 zimetolewa. Kati ya hizo, Shilingi bilioni 15.8 zimetumika kutengeneza barabara zeny urefu wa kilometa 4,190.

Ukaguzi uliofanyika umeonyesha kuwa asilimia kubwa ya Halmashauri zimetumia vizuri fedha za Mfuko wa Barabara ikilinganishwa na ilivyokuwa siku za nyuma. Napenda kupongeza wote waliofanya kazi hiyo. Serikali kwa kushirikiana na wafadhilli mbalimbali imeendelea kueneza mfumo wa menejimenti ya utengenezaji wa barabara za Wilaya kwenye Halmashauri nyingine 30 na kufanya jumla ya Halmashauri zilizofaidika na mfumo huo kufikia 54.

Katika mwaka 2006/2007, jumla ya Shilingi bilioni 25 zimetengwa kwa ajili ya Mfuko wa Barabara za Halmashauri. Aidha, Serikali itazifanya matengenezo barabara kuu na barabara za Mikoa zeny urefu wa kilometa 28,801 na madaraja 2,177. Vile vile, Halmashauri itaendelea kujengewa uwezo wa kupanga matengenezo ya barabara zake kwa ufanisi zaidi ikiwa ni pamoja na kuandaa mpango mzima wa kazi na kutoa taarifa ya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, Serikali iliendelea kutoa elimu kwa Umma kuhusu Sera, Sheria za Ardhi na Kanuni zake katika Wilaya mbalimbali nchini. Aidha, Serikali iliendelea kurasi misha ardhi na nyumba za wananchi ili zitambuliwe kisheria na kuwawezesha wananchi walio wengi kuingia kwenye mfumo rasmi wa uchumi.

Kazi ya kutambua makazi yaliyojengwa kiholela Mijini ilitekelezwa katika Jiji la Dar es Salaam, Mwanza na Manispaa ya Dodoma. Hadi Aprili 2006, jumla ya miliki 217,333 zilitambuliwa katika Miji hiyo. Kati ya idadi hiyo, taarifa za wamiliki 196,888 zimehakikiwa na kumbukumbu zao kuingizwa kwenye kompyuta. Serikali itaendelea kuboresha maeneo ya makazi hayo kwa kuyawekea huduma mbalimbali za jamii kama vile barabara, masoko na maji.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imefanya uhakiki wa Vijiji 10,337 kwa lengo la kuvisajili. Jumla ya Vijiji 9,828 vimepata usajili na zoezi hilo linaendelea kwa Vijiji vilivyobaki. Zoezi la kugawa na kuanzisha Vijiji ni gharama kwa Serikali. Hivyo, ni wajibu wa Viongozi wa Halmashauri kuangalia kwanza umuhimu wa kuanzisha Vijiji upya katika maeneo yanayohusika kabla ya kutuma maombi kwa Msajili. Aidha, maombi

ya kuandikisha Vijiji upya yafuate taratibu na vigezo vilivyoainishwa. Hata hivyo, Vijiji vya zamani ambavyo havina usajili vitaendelea kushughulikiwa ili vipate usajili.

Vile vile, katika mwaka 2005/2006, Serikali ilipima mipaka ya Vijiji 119 katika Mkoa wa Iringa. Aidha, jumla ya Vyeti vya Ardhi ya Vijiji 175 vilitolewa katika Wilaya za Mbozi, Iringa Vijijini, Handeni, Kilindi, Monduli, Kiteto, Namtumbo, Kilolo, Ngorongoro, Babati na Muleba. Jumla ya hatimiliki za kimila 842 zilitolewa kwa wananchi. Katika mwaka 2006/2007, Serikali itaendelea kutambua miliki katika maeneo yaliyojengwa kiholela katika Miji nchini na kutoa leseni za makazi. Kazi hii itakwenda sambamba na kuendeleza kasi ya kutoa hatimiliki za kimila kwa wanavijiji. Serikali pia itahakikisha kuwa angalau asilimia 50 ya Vijiji vyote nchini vilivyopimwa vinapata Vyeti vya Ardhi ya Kijiji.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2005/2006 Serikali iliendelea kushughulikia migogoro ya mipaka ya kimkoa na kiwilaya. Migogoro mingi ya mipaka inasababishwa na kutotafsiri kwa usahihi taarifa zinazotolewa katika Gazeti la Serikali na sheria ndogo kuhusu maelezo ya mipaka au maelezo hayo kutokidhi hali halisi iliyoko ardhini. Sababu nyingine ni wananchi kutojihusisha katika zoezi zima la kuweka mipaka na uwezo mdogo wa Mabaraza ya Ardhi kutoa maamuzi ya migogoro ya ardhi. Katika mwaka huu wa fedha, Serikali itaanza zoezi la kufanya mapitio ya maelezo ya mipaka ya Wilaya za nchi nzima ili kufanya marekebisho yanayohitajika. Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji yataanzishwa na kuimarishe ili yaweze kushughulikia migogoro ya ardhi. Aidha, Mabaraza ya Kata nayo yataimarishe ili yaweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo ikiwa ni pamoja na kusikiliza rufaa zinazotoka katika Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji na masuala mengine yanayohusu uvunjaji wa Sheria ndogo za Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza Sera ya Elimu na Mafunzo ili kuimarishe elimu katika ngazi mbalimbali. Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi umeendelea kutekelezwa kwa mafanikio makubwa tangu uanze. Kuanzia mwezi Julai, 2005 hadi kufikia Machi, 2006, jumla ya vyumba vya madarasa 4,847 na nyumba za Walimu 4,046 zilikuwa zimejengwa.

Aidha, jumla ya vyumba vya madarasa 2,160 vilikarabatiwa na nyumba za Walimu 3,128 zilikarabatiwa na nyumba 3,128 zilikuwa katika hatua mbalimbali za ujenzi. Ili kuimarishe ubora wa Elimu ya Msingi, Serikali iliendelea kutoa mafunzo ya Walimu Tarajali na kuwaendeleza Walimu walio kazini. Jumla ya Walimu Tarajali 7,500 walipelekwa kufundisha katika Shule za Msingi kwenye Halmashauri mbalimbali kuanzia mwezi Machi, 2005 na kundi lingine la Walimu Tarajali 4,599 lilipelekwa kuanzia Machi, 2006 kama sehemu ya mafunzo yao ya mwaka wa pili.

Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza Elimu ya Sekondari, Serikali inatekeleza Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (*MMES*). Ili kufanikisha azma hiyo, Serikali imetoa jumla ya Shilingi bilioni 11 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 1,569. Shule za Sekondari za Serikali zimeongezeka kutoka 1,206 mwaka 2005 hadi 1,538 mwaka huu wa 2006. Katika mwaka ujao wa fedha, 2007/2008, Serikali itaendeleza juhudzi za kupanua Elimu ya Awali, Elimu ya Msingi na upanuzi wa Elimu ya Sekondari. Aidha, kipaumbele kitawekwa katika kuimarishe mafunzo ya Ualimu ili ongezeko la wanafunzi

Sekondari liende sambamba na upatikanaji wa Walimu. Juhudi zitawekwa katika kuzingatia ubora wa elimu kama ilivyoshughulikiwa katika kuongeza idadi ya wanafunzi wa Shule za Msingi na Sekondari.

Mheshimiwa Spika, elimu ya juu hivi sasa imepata changamoto kutokana na ongezeko kubwa la wahitimu wa elimu hiyo. Idadi ya wanafunzi waliojiunga na Vyuo vya Elimu ya Juu vya Serikali na binafsi iliongezeka kutoka wanafunzi 48,145 mwaka 2004/2005 hadi 48,236 mwaka 2005/2006. Idadi ya wanafunzi wa kike waliopo katika Vyuo hivyo ni 15,782 sawa na asilimia 31.7. Ili kukabiliana na ongezeko la mahitaji ya kujiunga na Vyuo Vikuu katika mwaka 2006/2007, jitihada zinachukuliwa kupanua miundombinu kwa kujenga Kumbi za mihadhara na *Hostel* za wanafunzi, kukamilisha maandalizi ya Mpango Kamambe wa Upanuzi wa Elimu ya Juu na Ufundı, kujenga *Campus* ya Taasisi ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere huko Zanzibar na kuanza taratibu za ujenzi wa Chuo Kikuu cha Umma hapa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2005/2006, Serikali iliendelea kutekeleza Sera ya Maji kwa kuboresha huduma za maji Mijini na Vijijini kwa kushirikiana na Wahisani, Halmashauri za Wilaya na wananchi. Serikali ilifanya uchunguzi na kukamilisha usanifu wa kina wa miradi ya maji kwenye Vijiji 64 katika Mikoa ya Lindi na Mtwara. Serikali pia inatekeleza Awamu ya Pili ya mradi wa maji Chalinze.

Aidha, Serikali iliendelea kutekeleza programu ya maji na usafi wa mazingira Vijijini inayohusisha Wilaya zote za Mkoa wa Shinyanga kwa kuchimba visima virefu 15 na vifupi 52, ukarabati na ujenzi wa miradi ya bomba na uchimbaji wa mabwawa. Kwa upande wa maji Mijini, kiwango cha upatikanaji kiliongezeka toka mita za ujazo 271,500 mwaka 2004 hadi mita za ujazo 277,638 mwaka 2005. Ongezeko hilo limetokana na utekelezaji wa mpango wa kuimarisha huduma za majisafi na uondoaji wa majitaka katika Jiji la Mwanza, Mbeya na Manispaa za Songea na Iringa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, Serikali itaendelea na ujenzi wa mradi mkubwa wa kutoa maji Ziwa Victoria kwenda Miji ya Kahama, Manispaa ya Shinyanga na Vijiji 54 katika Mikoa ya Mwanza na Shinyanga. Kwa kutumia mkopo kutoka Mashirika Wahisani, Serikali itandelea na utekelezaji wa mradi wa kuboresha huduma za maji safi na maji taka katika Jiji la Dar es Salaam na Miji ya Kibaha na Bagamoyo. Aidha, itakarabati mitambo ya kuzalisha maji kutoka vyanzo vya Ruvu Juu na Ruvu Chini pamoja na kuboresha mabomba makuu yanayosafirisha na kusambaza maji kutoka mitambo hiyo.

Mheshimiwa Spika, ili kuzijengea uwezo Halmashauri katika kutoa huduma za afya, Serikali chini ya Mradi wa Ukarabati wa Vituo vya kutolea Huduma za Afya, inakarabati majengo, kutoa vifaa vya kitaalam na samani kwenye Hospitali za Wilaya, Vituo vya Afya na Zahanati. Katika mwaka 2005/2006, Serikali ilinunua magari 30 ya kubebea wagonjwa ambayo yatapelekwa katika Halmashauri za Wilaya ambazo ni mpya, zilizo pembezoni mwa nchi na zenye matatizo makubwa kijiografia. Katika mwaka 2006/2007, Serikali itanunua magari mengine 22 ya kubebea wagonjwa, kukarabati Hospitali za Wilaya 10 na kununua vifaa kwa ajili ya Hospitali hizo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, huduma za chanjo zimeboreshwa kwa kuimarisha usimamizi na upatikanaji wa mahitaji ya chanjo. Watoto 1,267,716 walipata chanjo ya surua mwaka 2005, ukilinganisha na watoto 1,237,771 mwaka 2004. Chanjo za dondakoo, pepopunda, kifaduro na homa ya ini zipatazo 1,249,399 zilitolewa mwaka 2005 ikilinganishwa na 1,245,056 mwaka 2004. Tanzania imeendelea kuungana na nchi nyingine duniani kutekeleza juhudini za kutokomeza polio, kudhibiti surua na kufuta ugonjwa wa pepopunda kwa watoto wachanga.

Vifo vya akina mama na watoto wachanga vimeendelea kuongezeka hadi kufikia vifo 578 kwa kila 100,000 ya vizazi hai, wakati vifo vya watoto chini ya mwaka mmoja na mitano vimeonyesha kupungua kufikia vifo 68 kwa 1,000 ya watoto hai na vifo 112 kwa 1,000 ya watoto hai sawia. Katika mwaka 2006/2007, Serikali itaanza utekelezaji wa mkakati kamambe wa miaka mitano wa kupunguza vifo vya wanawake na watoto wachanga vinavyotokana na uzazi. Mkakati huo utatekelezwa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali katika ngazi zote.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, Tanzania iliendelea kutekeleza wajibu wake katika Jumuiya ya Kimataifa. Nchi yetu imeshiriki katika Mikutano mbalimbali ya Kimataifa yenye maslahi kwa nchi yetu. Serikali imehamasisha Jumuiya ya wenyewe viwanda na wafanyabiashara nchini kutumia kikamilifu fursa mbalimbali zinazojitokeza kutokana na uanachama wetu katika Jumuiya mbalimbali kama vile Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika. Ili kuendeleza na kutekeleza diplomasia ya kiuchumi, Serikali imechukua hatua za kuimarisha ushiriki wetu katika Tume za pamoja za ushirikiano kati ya nchi yetu na nchi mbalimbali.

Aidha, uanachama wa muda wa nchi yetu katika Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, umetuwezesha sana kusukuma ajenda ya masuala ya amani na usalama katika maeneo ya Maziwa Makuu na migogoro iliyoko katika Bara la Afrika.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu vile vile imeshiriki kikamilifu katika kuwasaidia wananchi wa Burundi kupata suluhisho la kudumu la mgogoro baina ya Serikali ya Burundi na kundi la *PALIPHEHUTU FNL*. Tumepata faraja kubwa pale walipoafikiana na kusaini Mkatuba wa Amani tarehe 18 Juni, 2006 pale Mjini Dar es Salaam. Napenda kuwapongeza viongozi wetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Thabo Mbeki - Rais wa Jamhuri ya Afrika ya Kusini, kwa kuwezesha kwa kufikiwa kwa hatua hiyo muhimu kwa mustakabali wa nchi ya Burundi. Katika mwaka 2006/2007, Serikali itaendelea kutimiza wajibu katika Jumuiya ya kimataifa kushiriki katika Mikutano na ziara za kimataifa zenye maslahi kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Jinsia, Maendeleo na Watoto. Kwa kutambua na kuthamini nafasi za mchango wa wanawake katika maendeleo ya kisiasa, kiuchumi na kijamii, Serikali imeendelea kupiga vita mila, desturi na sheria zinazowabagua na kuwanyanya wanawake, pamoja na kusimamia Sheria na Mikataba ya kimataifa inayohusu haki na

ustawi wa wanawake. Katika kutimiza azma hiyo, Serikali inatekeleza Mkakati wa Taifa wa Maendeleo ya Wanawake na Jinsia unaotoa mwongozi kwa wadau kuzingatia masuala ya jinsia katika kuandaa na kutekeleza mipango yote ya maendeleo. Pia, utafiti wa kina umefanyika ili kubainisha mafanikio, matatizo na njia bora za kufikisha mikopo kwa wanawake. Katika mwaka 2006/2007, Serikali itaendelea kuchukua hatua mbalimbali zitakazowajengea uwezo wanawake kielimu na kiuchumi ili waweze kushiriki kikamilifu katika shughuli mbalimbali za maendeleo. Serikali pia itaimarisha vitengo vya jinsia katika Asasi na Idara mbalimbali za Serikali, kuendelea kutoa mikopo na kuendeleza Kampeni kwa kupanua wigo wa ushiriki wa wanawake katika umiliki wa rasilimali.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2005/2006, taarifa ya awali ya utekelezaji wa Mkataba wa Afrika kuhusu Haki na Ustawi wa Mtoto, ilitayarishwa. Pia, utafiti ulifanyika ili kuwatambua watoto yatima na walio katika mazingira magumu kwa lengo la kujua ukubwa wa tatizo na hatua zinazofaa za kuwanusuru. Wananchi wote tuna wajibu wa kuweka msukumo katika maendeleo, haki na ustawi katika maeneo ya elimu, afya na malezi ya watoto bila kuwanyanyasa. Aidha, tupige vita ajira kwa watoto na kuhakikisha sheria za kulinda watoto zinafuatwa. Ni vyema tufahamu kwamba, mtoto ana haki za msingi za kuishi, kuendelezwa, kulindwa, kushirikishwa na kutobaguliwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua mchango wa Wazee kama chimbuko la maendeleo ya nchi yetu. Kwa msingi huo, Serikali itaendelea kutekeleza Sera ya Taifa ya Wazee kwa kuwapa huduma muhimu kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa, zikiwemo huduma za afya, matunzo katika vituo maalum na kuwalipa mafao yao bila usumbufu. Aidha, Serikali itaendelea kutambua umuhimu wa kundi maalum la Walemvavu kwa kutekeleza Sera ya Taifa ya Watu Wenye Ulemavu ili wapate fursa za ajira, kushiriki katika siasa na uendeshaji uchumi kwa kuwapatia huduma za msingi za elimu na afya.

Mheshimiwa Spika, Mashirika na Taasisi. Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa una majukumu makuu matatu kama yaliyvoainishwa katika Sheria Na.6 ya mwaka 2000. Majukumu hayo ni kuhakikisha kuwa unakuwepo mpango wa malipo ya mafao kwa wanachama wanapostaafu, kusimamia mpango wa hifadhi ya jamii na kubuni mafao na maslahi mengine kwa wanachama na wale wanaojunga na Mfuko huo.

Katika mwaka 2005/2006 Mfuko umekuwa na wanachama 65,809 na umekusanya jumla ya Shilingi bilioni 41.6 sawa na asilimia 76 ya lengo la kukusanya Shilingi bilioni 54.8. Aidha, Mfuko umewekeza kiasi cha Shilingi bilioni 34.5 kwenye vitega uchumi mbalimbali vikiwemo dhamana za Serikali, amana za mabenki na hisa za Makampuni yaliyoorodheshwa kwenye Soko la Mitaji. Mfuko unatarajiwa kuwa na mtaji wa Shilingi bilioni 97.5 ifikapo tarehe 30/6/2006. Katika mwaka 2006/2007, Mfuko umepanga kuongeza idadi ya wanachama kutoka 65,809 hadi kufikia 72,400, kuboresha huduma zake kwa kuzisogeza karibu na walengwa, kuimarisha uwezo wake kifedha kwa kubainisha maeneo mapya ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaufanyia maboresho makubwa Mfuko huu wa LAPF kwa lengo la kuubadili na kuwa na malipo ya pensheni. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba zoezi hilo sasa limekamilika, hivyo, Serikali inatarajia kuwasilisha

katika Bunge hili Tukufu Muswada wa Sheria wa Kuunda Mfuko wa Pensheni kwa Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa. Ili kuhakikisha kwamba mafao na maslahi ya Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa yanaboresha, Serikali imekubali kimsingi kutoa kiasi cha Shilingi bilioni 107.3 kama ruzuku kwa Mfuko huu. Kiasi hicho kitatolewa kwa awamu kumi kuanzia mwaka 2007/2008 na kitawawezesha Wafanyakazi Wanachama wa Mfuko huu kuwa na sifa ya kulipwa mafao ya pensheni kwa kuzingatia muda wao wa ajira katika Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Elimu Kibaha lina jukumu kubwa la kupambana na adui maradhi, ujinga na umaskini. Katika mwaka 2005/2006, Shirika liliendelea kuwahudumia wagonjwa wa nje na waliolazwa katika Hospitali ya Tumbi. Shirika limeendelea kutoa elimu kwa akina mama kuhusu lishe bora, kuendesha Chuo cha Maafisa Tabibu na utoaji wa elimu katika Shule za Msingi na Sekondari zilizopo chini yake. Katika mwaka 2006/2007, mkazo zaidi utawekwa kwenye utekelezaji wa mambo yaliyoainishwa katika Mpango Mkakati wa Shirika amba ni pamoja na maeneo ya elimu, afya, maji na ukarabati wa miundombinu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2006/2007, Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa imeendelea kutekeleza nguvu zaidi katika kukusanya michango ya akiba na marejesho ya mikopo kama njia mojawapo ya kuongeza uwezo wa Bodi kifedha.

Hadi kufikia tarehe 31 Mei mwaka huu 2006, Bodi imefanikiwa kukusanya jumla ya Shilingi milioni 303.6 sawa na asilimia 75 ya Shilingi milioni 402.6 zilizokadiriwa kuchangwa na Halmashauri katika mwaka 2005/2006. Hivyo, kufanya jumla ya michango yote iliyokusanywa kuanzia mwaka 1982 kufikia Shilingi bilioni 2.3 kati ya Shilingi bilioni 5.5 zinazopaswa kuchangwa na Halmashauri. Aidha, kwa upande wa marejesho ya mikopo, jumla ya Shilingi milioni 186.5 zimerejeshwa sawa na asilimia 67 ya Shilingi milioni 278.7 zilizokadiriwa kurejeshwa katika mwaka 2005/2006. Jumla ya mikopo ya Shilingi bilioni 2.1 imetolewa kwa Halmashauri katika kipindi cha mwaka 1986 hadi Mei, 2006.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, Bodi itaendeleza kukusanya michango na marejesho ya mikopo pamoja na riba kama hatua mojawapo ya kuongeza mtaji. Napenda kutoa wito kwa Viongozi na Watendaji wa Halmashauri kuwa na mtazamo wa kimaendeleo ili waweze kukitumia chombo hiki kwa uwekezaji kwa ajili ya kusaidia maendeleo ya Halmashauri na wananchi kwa ujumla. Aidha, napenda kusisitiza umuhimu wa Halmashauri kuhakikisha kuwa katika kipindi cha mwaka 2006/2007, zinachangia kikamilifu katika Bodi na kurejesha mikopo kwa mujibu wa taratibu.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Serikali za Mitaa, Hombolo. Madhumuni ya Chuo hiki ni kutumia njia za mafunzo, utafiti na ushauri wa kitaalam, katika kuchangia uwezeshaji wa mchakato wa kupeleka madaraka kwa wananchi, kujenga na kukuza utawala bora, kukuza uchumi na kuondoa umaskini katika ngazi mbalimbali za Serikali za Mitaa hapa nchini.

Katika kipindi cha mwaka 2005/2006, Chuo kimeendelea kutumia katika uendeshaji wa mafunzo ya muda mfupi kwa lengo la kuwaandaa Walimu Maalum watakaoendesha Mafunzo ya Awali kwa ajili ya Wenyeviti Wapya wa Vitongoji, Vijiji na Mitaa. Katika kipindi cha mwaka 2006/2007, Chuo kitakamilisha ukarabati wa majengo, kukuza mitaala kwa ajili ya mafunzo ya muda mrefu, kuajiri watumishi wa kada mbalimbali wanaohitajika Chuoni, kuendesha mafunzo ya uboreshaji wa ujuzi na stadi za kazi kwa ajili ya Viongozi na Watendaji wa Kata, Vijiji na Mitaa na kuimarishe Maktaba ya Chuo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Mawaziri wote na Naibu Mawaziri wote kwa ushauri wao ambao umewawezesha Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Makamu wa Rais na Waziri Mkuu kutekeleza majukumu yao ya kitaifa kwa ufanisi. (*Makofî*)

Aidha, nawashukuru wafanyakazi wote wa Serikali na Taasisi zake chini ya uongozi wa Katibu Mkuu Kiongozi - Bwana Phillemon Luhanjo pamoja na vyombo vyote vya dola, kwa kuiwezesha Serikali kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kuiwezesha kukamilisha maandalizi yote ya Bajeti ya Serikali ya mwaka 2006/2007, pamoja na makadirio ya matumizi ya fedha ya kila Wizara, Mikoa, Idara na Taasisi zinazojitegemea. (*Makofî*)

Nawashukuru Watanzania wote na Washiriki wetu wa Maendeleo mbalimbali kwa michango yao iliyoiwezesha Serikali yao kutoa huduma mbalimbali kwa wananchi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, napenda vile vile kuwashukuru Mheshimiwa Juma Jamaldini Akukweti - Mbunge wa Tunduru na Waziri wa Nchi, Bunge na Uratibu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda - Mbunge wa Mpanda Mashariki na Waziri wa Nchi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Dr. Luka Jelas Siyame - Mbunge wa Mbozi Magharibi na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu na Mheshimiwa Celina Ompeshi Kombani - Mbunge wa Ulanga Mashariki na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa msaada mkubwa na ushirikiano walionipa katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nawashukuru pia viongozi wa Mikoa, Wilaya na Halmashauri zote nchini. Vilevile, nawashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu, chini ya uongozi wa Makatibu Wakuu, Bwana Vicent F. Mrisho na Bibi Tarishi Maimuna Kibenga na Manaibu Katibu Wakuu, Bwana Michael Mwanda na Bwana Wilson Mukama, kwa ushauri wao wa kitaalam ambao wamenipa katika kipindi hiki cha mwanzo katika uongozi wangu. Nawashukuru kwa kukamilisha maandalizi yote ya Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka 2006/2007, aidha, kuchapisha hotuba hii ambayo leo naiwasilisha katika Bunge lako Tukufu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, katika mwaka 2005/2006, nchi yetu imepata misaada na mikopo kutoka kwa Wahisani wetu mbalimbali. Misaada na mikopo hiyo imetoka kwa nchi rafiki, nchi fadhili, Taasisi za fedha duniani, Mashirika ya Umoja wa Mataifa, Mifuko mbalimbali Duniani, Madhehebu ya Dini na Mashirika yasiyo ya

Kiserikali. Misaada na Mikopo hiyo imechangia sana katika kubuni na kutekeleza miradi ya maendeleo na kuboresha utoaji wa Huduma kwa wananchi. Napenda kuwashukuru wote kwa dhati na kuwahakikishia kuwa Watanzania tunathamini misaada na mikopo yao na tutaendelea kushirikiana nao katika harakati za maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba hii nimezungumzia mambo mengi ambayo Serikali imefanya kwa kipindi cha mwaka 2005/2006 na mwelekeo wa kazi zitakazofanyika katika mwaka 2006/2007. Napenda kukamilisha hotuba hii kwa kusisitiza kipaumbele katika mambo muhimu yafuatayo:-

- (i) Uchumi wa nchi yetu unategemea sana kilimo. Tuweke nguvu zetu zote sasa kusisitiza kilimo bora na cha kisasa pamoja na upatikanaji wa mbegu bora, mbolea na madawa yote ya kilimo. Aidha, tusisitez kilimo cha umwagiliaji katika maeneo yanayofaa na yanayoweza kutumia mbegu zinazokomaa katika muda mfupi.
- (ii) Elimu ndiyo msingi wa maisha ya watoto wetu. Tuhimize umuhimu wa kupeleka watoto wenyewe umri wa kwenda Shule waende Shule. Aidha, msisitizo uwe katika kuwapatia nafasi watoto wote wanaofaulu katika Shule za Msingi kuingia Kidato cha Kwanza. Tuongeze juhudzi za ujenzi wa Shule na vyumba vya madarasa ili wote wanaofaulu wapate nafasi ya kusonga mbele. Msisitizo uwekwe katika kuhakikisha upatikanaji wa elimu kwa wote bila kuathiri ubora wa elimu itolewayo mashulen. Aidha, juhudzi ziongezwe katika kuhakikisha walimu wa kutosha wanapatikana;
- (iii) Wananchi wote tushirikiane katika kulinda usalama wa raia na mali zao. Tushirikiane kuwafichuka majambazi na Wahamiaji haramu. Mkono wa Serikali ni mkubwa, lakini ukaribu wa wahalifu kwa jamii ni mkubwa zaidi. Ushirikiano ndiyo siri pakee ya usalama wetu;
- (iv) Tushirikiane na Serikali katika kulinda na kutunza mazingira. Kila mwananchi ajiweke katika mstari wa mbale kutekeleza maagizo ya Serikali ambayo yametolewa kutekeleza jambo hilo;
- (v) Tulio ndani ya Serikali; tuongeze kasi katika utendaji na kutoa maamuzi ya kazi zetu kwa kulenga katika kuondoa kero za wananchi. Kila mwenye dhamana ya utendaji awajibike na kuwa mbunifu wa kuandaa mikakati ya utekelezaji sahihi wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii itatekeleza vizuri kama watumishi watawajibika ipasavyo kulingana na masharti ya ajira zao. Ni muhimu sasa wafanyakazi wabadilike waaache kufanya kazi kwa mazoea. Kila mtumishi anapaswa kupima kazi kwa kujiuliza ametoa mchango gani wa majukumu yake siku hiyo.

Naagiza Viongozi wa Wizara, Idara za Serikali, Mikoa na Halmashauri kuhakikisha kwamba watumishi wote wanafanya kazi kwa malengo, tija na ufanisi. Ni vyema sasa utumishi wa Umma uendeshwe kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya.

Mheshimiwa Spika, mwanafalsafa maarufu Frantz Fanon aliwahi kusema maneno ambayo naweza kuyatafsiri kama ifuatavyo:-

“Kuelimisha watu kupita majukwaa ya kisiasa hakuna maana ya kuwahutubia. Tafsiri ya hatua hizi ni kujaribu kwa nguvu zote kuwaelimisha kuwa mustakabali wa maisha yao unawategemea wao. Wakikwama ni wajibu wao, wakisonga mbele ni wajibu wao vilevile. Hakuna mtu ye yote hata awe maarufu au awe na uwezo kiasi gani aweze kubeba jukumu hilo. Hatma ya maendeleo yao ipo mikononi mwao” mwisho wa Kunukuu. (*Makofi*)

Nchi hii ni yetu sote. Hatuna Mjomba. Wadau wetu wa maendeleo wanaunga mkono juhudhi zetu tu, lakini hatma ya maendeleo yetu ipo mikononi mwetu. Tufanye kazi kwa bidii, kila mmoja kwa nafasi na eneo alilopo. Huu ndio msingi utakaotuwezesha kubadili maisha yetu.

Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka 2006/2007 Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake inaomba kumla ya Sh. 44,355,475,000/= kwa ajili ya mishahara na matumizi mengineyo. Ofisi ya Bunge inaomba jumla ya Sh. 34,584,964,000/= kwa ajili ya mishahara na matumizi mengineyo.

Kwa upande wa Fedha za Mpango wa Maendeleo, Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake inaomba jumla ya Shilingi 41,129,779,800. Kati ya fedha hizo, Sh.2,999,999,000/= ni fedha za hapa nchini na Sh.38,129,780,400/= ni fedha za nje.

Aidha, Ofisi ya Bunge inaomba jumla ya Sh. 300,000,000/= kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya hizo, Sh. 200,000,000/= ni fedha za ndani na Sh.100,000,000/= ni fedha za nje. Aidha, Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake inatarajia kukusanya maduhuli ya Sh. 1,881,872,000/=.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2006/2007, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Asasi zake inaombewa jumla ya Sh. 43,838,462,000/= kwa ajili ya mishahara na matumizi mengineyo. Kadhalika, jumla ya Sh.144,980,264,400/= zinaomba kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo Sh. 4,371,996,000/= ni fedha za ndani na Sh.140,608,268,400/= ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2006/2007 Ofisi za Wakuu wa Mikoa zinaombewa jumla ya Sh. 60,514,146,000/= kwa ajili ya mishahara na matumizi mengineyo. Vilevile, Mikoa inaombewa jumla ya Sh. 38,719,839,200/= kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo zikiwemo Sh. 12,929,399,000/= fedha za ndani na Sh. 25, 790,443,200/= fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2006/2007 Halmashauri za Miji zinaombewa jumla ya Sh. 138,484,036,000/= kwa ajili ya Mishahara na matumizi mengineyo. Halmashauri za Miji pia zinaombewa Sh.1,384,940,000/= fedha za ndani kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2006/2007, Halmashauri za Wilaya zinaombewa ruzuku ya jumla ya Sh. 591,801,241,000/= kwa ajili ya mishahara na matumizi mengineyo. Halmashauri za Wilaya vilevile zinaombewa jumla ya Sh. 8,691,660,000/= fedha za ndani kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, nawasilisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2006/2007 ya Sh. 1,148,784,807,000/=. Mchanganuo wake ni kama ifuatavyo:-

(i)	Ofisi ya Waziri Mkuu	Sh. 85,485,254,400/=
(ii)	Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa	Sh. 188,818,726,400/=
(iii)	Ofisi ya Bunge	Sh. 34,884,964,000/=
(iv)	Ofisi za Wakuu wa Mikoa	Sh. 99,233,985,200/=
(v)	Halmashauri za Wilaya	Sh. 600,492,901,000/=
(vi)	Halmashauri za Miji	Sh. 139,868,976,000/=
JUMLA		Sh. 1,148,784,807,000/=

Mheshimiwa Spika, pamoja na hotuba hii, nimeambatanisha majedwali yenye takwimu mbalimbali za Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Ofisi ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofit*)

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

SPIKA: Asante sana. Nina hakika Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote mtaniunga mkono kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba ambayo ni ya aina yake na inaleta matumaini kwa nchi yetu. (*Makofit*)

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea na wachangiaji, kama ulivyo utaratibu, tutaanza na Mwenyekiti wa Kamati inayohusika ambayo ni ya Katiba, Sheria na Utawala, atafuatiwa na Msemaji kutoka Kambi ya Upinzani, Msemaji Mkuu atakuwa ni Mheshimiwa Dr. Wilbrod Peter Slaa. Kabla ya kuwaita hao, nilikuwa na matangazo machache.

Kwanza Kamati ya Mambo ya Nje, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Anna Abdallah, anahitaji Wanakamati mkutane saa 7.00 mara baada ya kuahirisha Bunge, Chumba Na.231 ghorofa ya pili. Kamati ya Mambo ya Nje saa 7.00 Chumba Na.231 jengo la utawala.

Waheshimiwa Wabunge wote CCM ambao watakuwa na nafasi wanaombwa kwenda kule Makao Mkuu ya Chama cha Mapinduzi saa 7.15 kwa jili kumpongeza Mwenyekiti wao mpya wa Chama. (*Makofifi*)

Katika tangazo langu kuhusu *TAPAC*, Umoja wa Bunge unaopambana na UKIMWI nilitangaza kama vile ni Wajumbe wote na kumbe ni Kamati ya Utendaji tu. Kamati ya Utendaji ya *TAPAC* ndio ikutane mara baada ya kipindi hiki cha asubuhi.

Waheshimiwa Wabunge, wakati nawatambulisha wageni, kumbe walikuwepo wengi ambao wahusika wameniletea karatasi baada ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuanza kuongea, ni watu mashuhuri katika nchi yetu. Kwanza nafurahi kumtambulisha ndugu yetu mpandwa ambaye amekuwa katika utawala wetu siku nyingi kwa uaminifu mkubwa. Sio mwingine ni Mheshimiwa Joseph Sinde Warioba, aliyekuwa Waziri Mkuu katika Awamu ya Pili ya Serikali yetu. (*Makofifi*)

Pia nafurahi kumtambulisha kaka yangu Mheshimiwa Joseph Butiku, ambaye amekuwa msaidizi wa Baba wa Taifa toka kabla ya Uhuru, baada ya Uhuru na sasa hivi ni Katibu Mtendaji wa Mwalimu Nyerere *Foundation*. Pamoja nao, yupo Mzee Mirumbe, ni Muasisi wa CCM kule Mkoa wa Mara. Mwisho, ni ndugu yetu Mheshimiwa Ali Mzee Ali, ambaye ni Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar. (*Makofifi*)

Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ili awasilishe taarifa yake. Ni nusu saa na upinzani nusu saa.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni Na. 81(1), Kanuni za Bunge, Toleo la 2004, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mafungu 25 - Waziri Mkuu, Fungu 27 – Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, Fungu 37 – Ofisi ya Waziri Mkuu, Fungu 42 – Ofisi ya Bunge, Fungu 61 – Tume ya Uchaguzi, Fungu 91 – Tume ya Kuratibu Dawa za Kulevyta, Fungu 92 – Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania.

Aidha, napenda kuchukua nafasi hii kuwasilisha Taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Fungu 56 – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Fungu 70-89 na 95 - Mikoa.

Awali ya yote, nianze taarifa yangu kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na timu yake wakiwemo, Waheshimiwa Mawaziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Naibu Mawaziri, Wakuu wa Mikoa, kwa kuteuliwa na kushika nyadhifa katika Serikali ya Awamu ya Nne. Nina matumaini kuwa Kasi, Ari na Nguvu walizozionyesha kwa muda mfupi tangu kuteuliwa kwao ni dhahiri kuwa nyadhifa hizo zimepata watu wanaostahili.

Pili, napenda kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Yussuf Makamba - Mkuu wa Mikoa wa Dar es Salaam, kwa kuteuliwa kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na pia kuchaguliwa kuwa Katibu Mkuu wa CCM pamoja na

Waheshimiwa Wabunge wenzetu waliochaguliwa kushika nyadhifa mbalimbali katika Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama inavyofahamika, Ofisi ya Waziri Mkuu imegawanyika katika sehemu mbili. Kwanza, ni ile inayohusu mafungu niliyoyataja awali na pili, ni Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kwa kuelewa ukubwa na majukumu yaliyopo katika Ofisi hii, Kamati yangu ilitenga jumla ya siku tatu; kati ya hizo, siku moja kwa ajili ya kupitia na kujadili Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mafungu yaliyotajwa na siku mbili kwa ajili ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ikijumuisha Mikoa 21 ya Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ilipitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii, tarehe 30 Mei, 2006 Kamati hii ilipokea Muhtasari wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka 2006/2007 uliowasilishwa na Mheshimiwa Juma Jamaldin Akukweti - Mbunge wa Tunduru na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Bunge na Uratibu wa Shughuli za Serikali). Katika muhtasari huo, Kamati ilijulishwa juu ya dira ya Ofisi ya Waziri Mkuu na majukumu yaliyopo katika Ofisi hiyo na Taasisi zake.

Mbali ya hayo Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka 2005/2006 ambapo ilielezwa jinsi fedha zilizopangwa katika Ofisi hiyo na Taasisi zake zilivyotumika. Aidha, Kamati ilijulishwa juu ya kazi zilizofanyika, mafanikio yaliyopatikana na matatizo yaliyojiteza, kubwa zaidi likiwa tatizo la ukame ambalo liliilazimisha Ofisi ya Waziri Mkuu kutumia fedha nyingi kutembelea kwenye maeneo yaliyoathirika na kugharimia usafirishaji wa chakula cha njaa kwenye maeneo yaliyokumbwa zaidi na ukame.

Pamoja na jitihada zilizofanyika, bado nchi yetu inakabiliwa na upungufu mkubwa wa chakula hususan katika Mikoa ya Dodoma, Singida, Shinyanga, Tabora na kadhalika. Tunaishauri Serikali ijiandae vyema kukabiliana na tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, pia Kamati ilipata maelezo juu ya Mapato kwa kipindi cha mwaka 2005/2006 na matarajio ya kiwango kilichokusudiwa kukusanywa hadi tarehe 30 Juni, 2006. Hali kadhalika Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2005/2006 kwa mafungu yaliyoombewa fedha zikiwemo fedha za ndani na fedha za nje. Utekelezaji huu ulihu uendelezaji wa Jengo la Chimwaga, Ustawishaji wa Makao Makuu Dodoma, Ukarabati wa Ofisi ya Bunge, Dar es Salaam na ujenzi wa Ofisi Ndogo ya Bunge Zanzibar na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, katika muhtasari huo, pia Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa na Kamati katika kipindi kilichopita na utekelezaji wake. Moja kati ya agizo hilo lilikuwa kuitaka Ofisi ya Waziri Mkuu iweke ratiba inayoeleweka ya kuhamia Makao Makuu Dodoma kama ilivyoagizwa na Kamati katika Mwaka wa Fedha 2004/2005. Kwa kifupi Kamati ilielezwa kuwa gharama za kuhamia Dodoma ni kubwa na kwamba azma hii itafanikiwa pale uwezo wa Serikali utakaporuhusu.

Agizo lingine lilihusu kuitaka Tume ya Madawa ya Kulevy ya itoe elimu ya kutosha kwa wananchi kuhusu madawa hayo na kuitaka Serikali izifanyie marekebisho sheria zilizopitwa na wakati zinazotoa mwanya na kuzidisha kasi ya madawa ya kulevy.

Mheshimiwa Spika, karibu maagizo yote haya yametekelozwa kikamilifu. Hata hivyo, Kamati inaona kuwa licha ya maelezo mrefu yaliyotolewa na Serikali kuhusu utekelezaji wa Mpango wa Kuhamia Dodoma, bado agizo la kuitaka Serikali iweke ratiba yenye kueleweka halijatekelezwa ipasavyo. Kwa sababu hiyo, pamoja na hali ngumu ya uchumi bado Kamati inaiagiza Serikali iandae tena ratiba itakayoainisha Wizara zitakazohamia Dodoma hatua kwa hatua. Kamati inadhani kwamba kuwa na ratiba ya uhakika ni jambo muhimu hata kama utekelezaji wake utachukua muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu linafahamu kuwa Waheshimiwa Wabunge, kama Wawakilishi wa Wananchi, hawana Ofisi bora na vitendea kazi katika maeneo yao ya kazi. Kwa kulielewa tatizo hili, katika Mwaka wa Fedha uliopita 2005/2006, Kamati iliyahi kuiagiza Serikali itenye fedha na kuzipitishia Ofisi ya Bunge ili huduma hiyo isimamiwe na Ofisi ya Bunge moja kwa moja. Wakati wa kujadili Bajeti ya Ofisi hii kwa mwaka huu wa Fedha, suala hili lilijiteza tena na Kamati yangu ilitaka kujua utekelezaji wake. Katika kuijibu hoja hii, Serikali ilieleza kuwa katika mwaka huu wa fedha, huduma hizo zimepelekwa kwa Makatibu Tawala wa Mikoa badala ya Ofisi ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, mbali na kupokea utekelezaji wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha uliopita 2005/2006, vilevile Kamati ilipokea maelezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha katika mwaka 2006/2007, yakiwemo Matarajio ya Mapato na Mpango wa Maendeleo. Aidha, Kamati ilifahamishwa juu ya kazi zilizopangwa kufanyika katika mwaka huo wa fedha.

Mwisho, Kamati iliombwa kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kama alivyoeleza Mto Hoja.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kupitisha Makadirio hayo, Kamati ilikuwa na maoni na mapendekezo kadhaa katika Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwanza, kuhusu Mpango wa Kuhamia Dodoma, napenda nikiri kuwa Kamati yangu ilikuwa na mjadala mkali kuhusu suala hili huku Wajumbe wakieleza kusikitishwa kwao na kiwango kidogo cha Bajeti kilichotengwa kuendeleza Makao Makuu Dodoma. Kamati inashauri kuwa katika Bajeti ijayo Serikali itenye fedha za kutosha kwa ajili ya kuendeleza Makao Makuu Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona kuwa zimekuwepo ahadi nyingi zilizowahi kutolewa na Viongozi wa Kitaifa kuhusu azma ya Serikali kuhamia Dodoma. Ingawa Kamati inaamini kuwa zipo sababu za msingi za kuyakarabati na kujenga baadhi ya majengo ya Serikali Dar es Salaam ambako kimsingi si Makao Makuu rasmi ya Serikali, kitendo cha kuendelea kuyakarabati pengine kwa gharama kubwa zaidi hakiashirii nia ya dhati ya Serikali kuhamia Dodoma.

Bila shaka tutakubaliana kuwa, kama fedha hizo za ukarabati na ujenzi wa majengo mapya Dar es Salaam, zingetumika kujenga Wizara moja moja hatua kwa hatua Dodoma, azma hii ingeweza kufikiwa. Tukubali kuwa Jiji la Dar es Salaam sasa hivi limekuwa na kila aina ya msongamano ambaao kwa hali halisi, baadhi ya huduma hizo kama zingekuwa zikitolewa hapa Dodoma nina hakika kuwa msongamano huo kwa kiasi fulani ungepungua. Hivi kama Bunge hili lingeendelea kufanyika Dar es Salaam, hivi sasa hali ingekuwaje? (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, katika kipindi kilichopita, Kamati pia ilipata fursa ya kutembelea jengo la Ofisi ya Waziri Mkuu Dodoma. Kamati imebaini kuwa jengo hilo ni kuu kuu na halistahili kutumiwa na Waziri Mkuu. Kamati inaagiza kuwa jengo hilo lifanyiwe ukarabati mkubwa ili lilingane na hadhi ya Ofisi ya Waziri Mkuu hasa ikizingatiwa kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu ina shughuli, Idara na Taasisi nyingi ambazo Watendaji wake wamekuwa katika Ofisi zilizosongamana. Aidha, Kamati inashauri kuwa kiasi cha Sh. 3,510,000,000/= kinachoombwa kwa ajili ya kukarabati majengo ya Ofisi ya Waziri Mkuu Dodoma na Dar es Salaam katika mwaka huu wa fedha, kitumike kwa ajili ya ukarabati wa Ofisi hiyo Dodoma.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine linahusu Tume ya Uchaguzi. Kwanza, Kamati inaipongeza kwa kazi nzuri iliyofanya wakati wa Uchaguzi Mkuu licha ya matatizo madogo madogo yaliyojitokeza. Hata hivyo, Kamati inashauri kuwa ni vyema Tume ya Uchaguzi ijitahidi kurekebisha dosari zilizojitokeza na kuhakikisha kuwa katika kipindi kijacho wananchi wote wanatumia kikamilifu haki yao ya kupiga kura. Aidha, Kamati inaagiza kuwa Tume ya Uchaguzi iangalie uwezekano wa kupanga tarehe ya Uchaguzi Mkuu iwe katikati ya wiki badala ya siku za Ibada.

Kamati inafikiri kwamba kupanga tarehe ya uchaguzi iangukie siku za ibada kunaweza kuingilia uhuru wa kuabudu wa baadhi ya dini na hivyo kusababisha waumini wengine wasiweze kupata nafasi ya kupiga kura.

Pia, kutokana na uzoefu uliopatikana tangu Tanzania iingie katika mfumo wa Vyama Vingi, imeonekana kuwa Watanzania walio wengi hasa wanaoishi Vijijini bado hawaelewi vyema jinsi mfumo huu unavyofanya kazi. Hivyo, Kamati inaagiza na kusisitiza kuwa kuwe na mikakati maalum ya kuwaelimisha wananchi hasa wa Vijijini namna Mfumo wa Vyama Vingi unavyofanya kazi na hasa juu ya utaratibu wa kupiga kura katika mfumo huu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania, pamoja na kazi nzuri inayofanyika, Kamati inaagiza kuwa Tume iendelee kupanua shughuli zake zaidi ili kuwafikia wananchi wengi Vijijini na kwamba kuwe na mikakati ya kutosha ya kuwasaidia yatima na waathirika wa VVU. Kila inapowezekana Tume ishirikiane na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupambana na janga la UKIMWI Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kwa kuelewa kuwa tatizo sugu la Madawa ya Kulevyaa linaendelea kuwakumba vijana wetu Mijini na vijijini, Kamati inaagiza kuwa Tume ya

Madawa ya Kulevyia iwafuatilie kwa karibu vijana wanaoathirika na madawa hayo na iendeleze mikakati yake ya kupambana na tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, haya ni baadhi ya maoni na maagizo ambayo Kamati yangu iliyatoa ilipochambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mafungu niliyoyataja hapo mwanzo. Baada ya maelezo hayo, sasa naomba nizungumzie Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa ajili ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, Kamati yangu ilitenga jumla ya siku mbili kujadili Makadirio ya TAMISEMI. Kwanza, kutokana na majukumu mengi iliyonayo yanayowagusa wananchi walio wengi na pili, kulingana na Makadirio ya Mikoa 21 ambayo Kamati ililazimika kuyapitia. Kazi hii ilifanyika tarehe 1 - 2 Juni, 2006.

Mheshimiwa Spika, tarehe 1 Juni, 2006, Kamati yangu ilipokea maelezo ya Utekelezaji wa Majukumu ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka wa Fedha 2005/2006 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2006/2007. Maelezo haya yaliwasilishwa na Mheshimiwa Mizengo Pinda - Mbunge na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri wa Mkuu (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa).

Katika maelezo hayo Kamati ilijulishwa juu ya dira ya TAMISEMI na majukumu iliyonayo, kuzielimisha Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwa sababu hiyo Kamati inaagiza kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu ikishirikiana na Wizara nyingine kuzielimisha kwa kina majukumu yake yanayohusiana na Wizara hizo.

Mheshimiwa Spika, katika kuijadili bajeti ya Ofisi hii, Kamati ilitazama kwa kina utaratibu uliopo sasa wa kuwafanya Wakuu wa Mikoa kuwa Washauri wa Halmashauri za Wilaya na Muundo wa nafasi ya Ushauri wa Mikoa na Sektretarieti za Mikoa. Kamati inafikiri kuwa utaratibu huu unawafanya Wakuu wa Mikoa na Kamati za Mikoa kuwa vyombo vya ushauri tu. Hivyo, kutokuwa na meno dhidi ya Halmashauri zinazohusika. Kamati inaagiza kuwa utaratibu huo uangaliwe upya na kuboreshwa ili vyombo hivyo viwe na meno.

Mheshimiwa Spika, kutokana na majukumu waliyonayo Waheshimiwa Madiwani Serikali iangalie uwezekano wa kuongezea posho. Aidha, Serikali iandae mafunzo maalumu kwa ajili ya Madiwani nchi nzima ili kuwawezesha kuelewa majukumu na mipaka ya kazi zao. Mafunzo hayo ni muhimu kwa kuwa yatapunguza migongano katika utekelezaji wa majukumu kati ya Madiwani na Watendaji.

Mheshimiwa Spika, haya ndiyo maeneo ambayo Kamati yangu ilijielekeza kwa kina na kuyatolea maoni. Maeneo ambayo sikuyagusia, natumaini kuwa Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati yangu watayazungumzia pindi watakapotapa fursa ya kuchangia mjadala wa Ofisi hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kukuthibitishia kuwa baada ya Kamati yangu kuridhishwa na kazi nzuri iliyofanyika Ofisi ya Waziri Mkuu na ufanuzi uliotolewa

katika maeneo kadhaa ambayo Kamati yangu ilitaka maelezo, kwa kauli moja ilipitisha makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo.

Mheshimiwa Spika, mwisho nachukua fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati yangu kwa kazi nzuri ya kuchambua makadirio ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa muda wote wa siku tatu, umakini wao na uzoefu wao wa muda mrefu katika maeneo mbalimbali ya Serikali na Halmashauri zake ndiyo uliofanikisha kazi hii.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niwatambue Wajumbe wa Kamati yangu:-

Mheshimiwa George Malima Lubeleje - Mwenyekiti, Mheshimiwa Tatu M. Ntimizi - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Hazara Pindi Chana, Mheshimiwa Stephen J. Galinoma, Mheshimiwa Athumani Janguo, Mheshimiwa Rajab Hamad Juma, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Charles N. Keenja, Mheshimiwa Salim Yussuf Mohammed, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Fatma M. Maghimbiri, Mheshimiwa Ramadhan A. Maneno, Mheshimiwa Halima T. Mdee, Mheshimiwa Nimrod E. Mkono, Mheshimiwa Abbas Z. Mtemvu, na Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa.

Mheshimiwa Spika, vilevile, nawashukuru Makatibu wa Kamati hii, Ndugu Charles Mloka na Ernest Zulu, kwa kutoa huduma wakati wote wa Vikao vya Kamati na kutayarisha Taarifa ya Kamati katika hatua inayoonekana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naiunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati, sasa nitamuita Mheshimiwa Msemaji Mkuu wa Upinzani kwa Sekta hii. Mheshimiwa Dr. Wilbroad Slaa.

MHE. DR. WILBROD PETER SLAA – (k.n.y. MHE. HAMAD RASHID MOHAMED - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI KWA OFISI YA WAZIRI MKUU): Mheshimiwa Spika, kwa ruksa yako naomba niwashukuru wote na niwapongeze. Kwa ajili ya muda sitaingia kupongeza mmoja mmoja lakini wale wote walioteuliwa jana, katika Chama Cha Mapinduzi nawapongeza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa CCM na wale wote na hasa Wabunge wote kwa kuchaguliwa. Napenda niwapongezeni kwa dhati kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee sana, nawashukuru na kuwapongeza sana wananchi wa Karatu kwa kukataa hujuma ya kila aina na kunichagua tena kwa

kipindi kingine kuwa Mbunge wao na kuirudisha CHADEMA kama Chama Tawala Karatu, *UDP* kuwa Chama Tawala Bariadi na *CUF* kuwa Chama Tawala Pemba na hivyo kukifanya kwa mara nyingine CCM kuendelea kuwa Chama cha Upinzani katika maeneo hayo. Naamini sasa inaanza kueleweka miongan mwetu kuwa na Chama Tawala Kitaifa, lakini kukawa na Chama tofauti katika ngazi za Halmashauri.

Serikali badala ya kufanya hujuma ya kuidumaza demokrasia na kufanya kila mbinu kufuta upinzani katika maeneo hayo ianzishe rasmi na kwa vigezo wazi mashindano ya maendeleo kati ya Wilaya zinazoongozwa na upinzani na zile zinazoongozwa na Chama Tawala, huu ndiyo utakuwa ukomavu wa demokrasia katika nchi yetu. Ni imani yetu kuwa ukomavu ulioonyeshwa na CHADEMA na CCM kuunda uongozi mseto katika Manispaa ya Kigoma Ujiji utaendelea kuenziwa katika maeneo mengine kwa manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri Mkuu na Timu yake yote kwa kuwasilisha Bajeti hapa Bungeni kwetu. Napenda niseme kwamba, tunapajaribu kutoa upande wa pili, sio kwa sababu tunataka kushindana na Serikali, bali tunataka kutoa upande wa pili wa Shilingi.

Mheshimiwa Spika, hali ya Siasa Katika nchi yetu, Kama wote tunavyojua hii ni Bajeti ya Kwanza tangu Uchaguzi Mkuu wa Rais, Ubunge na Udiwani uliofanyika tarehe 14 Desemba, 2005. Hata kama wapo waliojaribu kuchezea umoja wetu, ni jambo jema sana kuwa tumebacki kuwa nchi mmoja na kuendelea kupingana bila kupigana.

Tunamshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa neema ya kipekee aliyotujalia sisi Watanzania. Neema hiyo sio nyingine ila kuwa na utamaduni wa uvumilivu na ustahimilivu. Hata hivyo, Kambi ya Upinzani inaanmini kuwa ili demokrasia yetu ipevuke na ili chaguzi zetu ziwe za kweli, haki na huru, mambo yafuatayo ni muhimu kuangaliwa sana katika chaguzi zijazo.

Mheshimiwa Spika, moja, pamoja na sura ya demokrasia changa iliyokuwepo, uzoefu unaonyesha kuwa katika maeneo mengi ya nchi yetu na zaidi, yale yanayoongozwa na Vyama vya Upinzani, ama kule ambako upinzani una nguvu, matendo kadhaa ambayo ni kinyume na misingi ya demokrasia yalijidhihirisha. Sisi tunaotoka maeneo hayo ni mashahidi hai. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, hakuna anayekataa matumizi ya Vyombo vya Dola katika kulinda usalama wa wananchi wakati wa kampeni na hata wakati wa mchakato mzima wa upigaji kura. Mabomu ya machozi, marungu na hata na risasi za moto zilitumika katika maeneo kadhaa ikiwa ni pamoja na Bariadi Mashariki, Tarime, Karatu, Unguja, Pemba na kwingineko. Viongozi wa Vyama vya Siasa walikamatwa na kudhalilishwa. *FFU* kupelekwa hadi Vijijini, kwa wananchi walio wengi hata Polisi wa kawaida wanawaona kwa nadra. Haya yote ni kujenga mazingira ya hofu kwa Watanzania ambao katika hali ya kawaida wamezoea kuishi kwa amani na kushirikiana. Tendo hilo peke yake hufanya upigaji kura usiwe wa haki na huru.

Mheshimiwa Spika, bado kuna mapungufu kuhusiana na Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Tofauti na tulivyofikiri wakati tukielekea katika Uchaguzi, Tume hii imeshindwa kutekeleza yale ambayo kwa pamoja tulikubaliana kama njia makini ya kuondoa muono wa wengi kuwa Tume imeegemea zaidi kulinda maslahi ya Chama Tawala.

Mheshimiwa Spika, Wasimamizi na Wasimamizi Wasaidizi wote ni Watendaji wa Serikali. Mfumo wa kisiasa uliojengwa na Chama Tawala unawalazimisha Watendaji kuegemeza uaminifu wao kwa maslahi ya Chama hicho badala ya wananchi.

Tunaelewa sababu ya kutumia Watendaji wa Serikali katika ngazi hii, lakini iwapo kuna malalamiko, ni vyema Serikali ikasikiliza kilio cha watu na kurekebisha kasoro hii kubwa ili kufanya mfumo wa demokrasia sio tu uwepo, lakini pia uonekane kuwa unafuatwa na kutekelezwa. Demokrasia ni ghali, hivyo ni lazima tuktaka kuwa na uchaguzi huru, usio na mizengwe, ni vyema Tume ya Taifa iwe na Maafisa wake kwenye ngazi ya Wilaya wasio na mgongano wa kimaslahi. Suala la Tume huru nalo litazamwe kwa umakini, bila kutoa tafsiri potofu ya Tume Huru.

Hatua ya kuwa na Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ni njema. Daftari hilo likiandaliwa na kutumika vizuri ni njia mojawapo ya kupunguza udanganyifu kwa kiasi kikubwa. Kutokuwa na Daftari moja la Muungano, ucheleweshaji wa kuvipatia Vyama Daftari kwa uhakiki, Majina kubandikwa siku za mwisho katika Vituo vya Uchaguzi na hata kubanduliwa kwa makusudi kabisa katika Vituo vingine ni dosari kubwa iliyoharibu maana halisi ya Daftari hili.

Katika maeneo mengi, wapiga kura walifika wakakuta majina yao hayapo. Kutohana na mparaganyiko huo wa Daftari la Kupiga kura pamoja na sababu nyinginez, karibu Watanzania milioni tano walishindwa kutumia haki yao ya kupiga kura. Hii inaonyesha kuna tatizo. Ni vyema maandalizi ya Daftari yakaangaliwa upya na marekebisho ye yeyote yanayofanyika yawe ya uwazi kuondoa hisia zinazoweza kujitokeza.

Mheshimiwa Spika, katika ngazi ya Serikali za Mitaa, tunataka mfumo mzima wa Uchaguzi ukaangaliwe upya na uwewe chini ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi na hasa kwa vile tunalo Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ijaze nafasi zote zilizo wazi katika Serikali za Mitaa bila mizengwe ya aina ye yeyote, kama ilivyojitokeza katika Kijiji cha Piaya, Wilayani Ngorongoro siku chache zilizopita.

Mheshimiwa Spika, suala la kuwawezesha kimaslahi Wenye viti wa Vitongoji, Vijiji, Mitaa, Masheha na Madiwani ambao ndio walio karibu zaidi na wananchi, sio la hiari. Serikali Kuu ithamini hadhi ya Viongozi wetu hao na hao ndiyo wasimamizi na watekelezaji wakuu wa MMEM, MMES, Miradi ya Afya na Kilimo tunayotegemea sana kukwamua nchi yetu kutohana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, hata *WEO* na *VEO* kama tunataka waache kuwa Miungu watu kama tulivyosema, ni lazima mishahara yao ipatikane kwa wakati tofauti na sasa ambapo wengi wao zaidi ya miezi mitano hawajalipwa. Hata mwaka 2005 fedha zao zilikuwa kwenye Bajeti lakini hazikutoka. Suala la kuwajengea uwezo wa kielimu na Taaluma, nayo ni ya muhimu ili waweze kutimiza majukumu yao kwa tija.

Kambi ya Upinzani imesisitiza mara nyingi kuwa Wakuu wa Wilaya kwa jinsi walivyo hawana kazi na ni vyema kada hiyo ikafutwa, au Sheria ifanyiwe marekebisho makubwa ili kuwa na uhusiano wa kisheria kati ya Ofisi ya Mkuu wa Wilaya na ya Wakurugenzi Watendaji.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Wakuu wa Wilaya wanafanya kazi za Wakurugenzi na Wakurugenzi wamekuwa Watalii kila kukicha wako kwenye Semina au Mikutano nje ya Wilaya. Hali hii ni lazima irekebishwe mara moja kuokoa fedha nyingi zinazopotea kwenye safari nyingi za Viongozi hao zisizo na tija. Serikali ieleze kwa kina itachukua hatua gani katika eneo hili muhimu.

Mheshimiwa Spika, Sheria zinazoongoza Serikali za Mitaa zifanyiwe marekebisho makubwa kuendena na mabadiliko makubwa ya kiuchumi na kisiasa yaliyofanyika katika nchi yetu.

Sheria ya Vyama vya Siasa sura ya 258 kama ilivyorekebishwa mwaka 2002 kifungu cha 16(2) inataka Serikali kutoa Ruzuku kwa Vyama vilivytotima masharti na kuvivezesha kutimiza masharti na kuvivezesha kutekeleza majukumu yao katika Serikali za Mitaa. Tangu sheria hiyo imetungwa, ruzuku hiyo haijawahi kutolewa kwa Halmashauri au kwa Madiwani. Ni lini sasa Serikali itatekeleza jukumu hilo la kisheria? Tungependa Serikali itupe jibu.

Mheshimiwa Spika, ni kweli nchi yetu imejitahidi kuweka miundo mbinu ya kuboresha misingi ya Utawala Bora wenye kufuata Sheria. kwenye vyombo vya habari tumesikia kuwa wala rushwa wanapewa muda wajirekebishe. Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kila mwaka inaonyesha ubadhirifu mkubwa wa fedha za Wananchi katika Halmashauri ya Miji, Manispa na Wilaya. Hivi ni wapi duniani walarushwa wanapewa muda wa kujirekebisha?

Madiwani katika Halmashauri kadhaa wamechukua hatua kuwadhibiti wahusika. Mathalan Halmashauri ya Singida na Mkuranga, hata kwa kuwang'oa Viongozi waliohusika. Je, ni kweli inawezekana hawakufuata utaratibu? Lakini kutokufuata utaratibu hakuondoi ukweli kuwa upotevu upo, au kuwa wananchi wamekosa huduma muhimu kwa ajili ya uzembe wa wachache.

Serikali ilitakiwa kuingilia mara moja na kuchukua hatua madhubuti na siyo kuwapa vichwa wazembe au wabadhirifu hao kama inavyofanya sasa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mifano hai ya kuzorota kwa utendaji kazi katika Halmashauri iko mingi, kama vile Halmashauri ya Wilaya ya Kahama na Korogwe. Mahali kama Kinondoni, matumizi mabaya yanatokana na uamuvi mbovu kama inavyosemekana wa kutoa vipaza sauti vilivyonunuliwa kwa Kodi ya Wananchi kwa Umoja wa Vijana wa Chama Tawala.

Suala la kutoa Kituo cha Dala Dala toka Mwenge kwenda Makumbusho ambako nako hali imekuwa mbaya zaidi ni dalili ya wazi ya wingu la rushwa na ubadhirifu na kutokuwajibika. Tunawapa pole wananchi wote wanaoendelea kuteseka kwa uzembe huo na Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe kauli kuhusu kadhia hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa utafiti wetu, fedha nyingi katika Halmashauri zinapotea kutockana na udhibiti mbovu. Katika Halmashauri ya Babati kwa mfano chanzo kimoja tu cha Stendi ya Mabasi kina uwezo wa kukusanya Sh. 738,000/= kwa mwezi, lakini Mkataba umetolewa kwa wakala kwa malipo ya Sh. 460,000/=kwa mwezi ambayo nayo hukatwa Kamisheni ya Wakala.

Mheshimiwa Spika, kama kianzio kimoja tu kinaweza kupoteza wastani wa zaidi ya Sh. 4,000,000/= kwa mwaka, ni kiasi gani kinapotea kwa mwaka kwa nchi nzima? Huu ni mfano hai mwingine wa rushwa na ubadhirifu. Ili kuondoa matatizo ya aina hii na kujenga uwezo wa Halmashauri Kambi ya Upinzani, inaitaka TAMISEMI na Serikali kwa ujumla iweke kitengo maalum cha Utafiti kubaini udhaifu na ubadhirifu wa aina hii na kushauri mbinu ya kuokoa fedha nyingi za Wananchi kabla hazijapotea.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais wa Tatoo wa nchi yetu katika hotuba yake Bungeni alisema kuwa, Watendaji wa Kata na wa Vijiji wamekuwa Miungu watu. Serikali inafahamu fika jinsi wengi walio katika kada hii ni kero kubwa kwa wananchi. Mfano hai ni Mtendaji wa Kata ya Kansay, Wilaya ya Karatu anayetuhumiwa kumtorosha mtu aliyembaka. Wanakijiji wakishirikiana na Viongozi wao wanamkamata mbakaji, wanampeleka Ofisini kwake kama mlinzi wa amani, lakini yeze anamtorosha. Madiwani wanachukua hatua, lakini analindwa. Mtu wa namna hiyo bado yuko kazini! Kuna kulindana sana! Ni vichekesho! Tunajenga imani gani kwa wananchi? Maneno yetu matamu yanakuwa kitanzi kwa wananchi wanyonge hata kwa uhai na maisha yao!

Waziri Mkuu alieleze Bunge hili Tukufu, Serikali ina mpango gani wa kurudisha maadili katika kundi hili ambalo ni injini ya maendeleo na tegemeo katika vita dhidi ya Umaskini?

Mheshimiwa Spika, tuna taarifa kuwa kule Bariadi *WE*O anaweza kufika kwenye nyumba na kudai apewe ng'ombe idadi anayotaka, akinyimwa anambambikia kosa la mauji raia asiye na kosa. Taarifa ya Tume ya Haki za Binadamu iliyotembelea Magereza ni ushahidi kamili wa idadi ya Watanzania walioko Magerezani na wamelalamika kubambikiziwa makosa ya mauji, tena yasiyo na mdhamana. Wakati huo huo, Serikali inalalamika msongamano kwenye Magereza yetu. Viongozi kama hao ndio chanzo cha tatizo hili!

Mheshimiwa Spika, Taarifa ziko nyingi za *WEO* wengi kuweka wananchi rumande bila sababu za msingi, na kwa vile wananchi wa Vijijini wengi hawajui haki zao na hata wanaozijua na kuzifutilia wanaminywa kwa kulindana. Taarifa hizi ziko nyingi, tumekwizhazikilisha Serikalini, na nyingine ziko njiani zinakwenda kwa Waziri anayehusika. (*Makofi*)

Kambi ya Upinzani inaitaka Ofisi ya Waziri Mkuu ambaye ni msimamizi wa Shughuli za Serikali Bungeni na mratibu wa shughuli zote za Serikali atuhakikishie ni mkakati gani Serikali ya Rais wa Nne imeweka kuondosha na kumaliza moja kwa moja kero hizi, ambazo kwa hakika ni tofauti na kero ya njaa, ipo ndani ya uwezo na mamlaka yetu kama kweli tumedhamiria kuiondoa.

Mheshimiwa Spika, Utawala Bora na Utawala wa Sheria ni pamoja na wahusika katika vyombo vyote vya dola kufuata Sheria, kanuni na taratibu. Ndani ya Bunge lako hili Tukufu tulitoa taarifa na hata majina ya Mahakimu wanaotumia vibaya mamlaka yao. Serikali katika majibu yake ikasema inafuutilia na kuwa inafanya uchunguzi. Masuala yanayohusu Haki za Binadamu ni masuala yasiyohitaji ‘ngoja kwanza.’ Serikali inapaswa kuonyesha kwa vitendo kuwa kweli ina dhamira ya kweli kuboresha haki za Binadamu.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inataka Serikali inapotoa ahadi, basi ifuatilie na itoe taarifa ya mara kwa mara kwa waliotoa taarifa kujua hatua kweli inachukuliwa. Vinginevyo, Watanzania watajua ahadi hizi ni sawa na ahadi za nyuma ambazo zote hazikufanya kazi.

Ahadi ya Serikali ya Rais wa *Tatu ya kupiga vita Rushwa haikuzaa matunda yaliyotarajiwa na wala kutoa matumaini*. Ahadi ya ‘Ufagio wa Chuma’ nayo ilipokelewa kwa vifijo na vigelele, lakini ikawaacha Watanzania kwenye Mataa na ndiyo tukafikishwa tulikofika. Tatizo ni kutokuwa na mikakati endelevu na badala yake kujigubika katika utamaduni wa kufanya mambo yetu katika mfano wa zimamoto. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, bado Watanzania wanapokwenda Polisi au Mahakamani wanalahimika kununua haki yao. Japo vifungu 64-69 vikisomwa pamoja na 148-160 vya *Criminal Procedure Act*, (*CPA*) viko wazi na vinatoa masharti ya haki ya dhamana, mara nyingi masharti hayo yanafanywa kuwa magumu bila sababu za msingi. Hapa kuna mazingira ya rushwa.

Mheshimiwa Spika, Sheria yetu inawataka watoa na wapokea rushwa kuwa wote wana makosa. Hivyo, inakuwa vigumu kupata ushahidi kwa vile wananchi wengi wanaogopa kutoa ushahidi. Wanaogopa zaidi wanapojuwa kuwa wahusika hawachukuliwi hatua na badala yake wao ndio wanashughulikiwa ipasavyo na wahusika hao hao.

Serikali ni lazima ichukue hatua ya makusudi katika kuwalinda wanachi wake kutokana na watu wachache wanaochafua jina la Jeshi la Polisi na la Mahakama zetu.

Mheshimiwa Spika, wakati wa majibu, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa mpango na mkakati ulio wazi kushughulikia suala hili. Ikiwa lazima, sheria zirekebishwe na kuwekwa wazi zaidi kuwaokoa Watanzania wengi waliofikia hatua ya kukata tamaa. Kile kinachoitwa Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya, ikionekana katika eneo hili mengine yote yatafuata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hatua ya Serikali ya hivi sasa ya kuwateua Wabunge wa Majimbo kuwa Wakuu wa Mikoa au Mkuu wa Mkooa kuwa Mbunge inaelekea kупingana na dhana nzima ya Ibara ya 66(3) hasa ikisomwa pamoja na Ibara ya 67(2)(g).

Pamoja na Kauli ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Bungeni ya tarehe 22 June, 2006, Kambi ya Upinzani inaamini kuwa, tafsiri ya Ibara hizi zinakwenda kinyume na Katiba. Isitoshe, Kauli hiyo ya Mwanasheria Mkuu, ikitafsiriwa kwa mujibu wa Ibara ya 61(l) inaleta utata zaidi wa kikatiba hasa kwa kuwatafsiri Wakuu wa Mikoa kama Viongozi wa Kisiasa.

Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe maelezo ya kina kuhusu tafsiri sahihi ya Ibara hizi. Sio vema Serikali inayotakiwa kuilinda katiba pia iwe mstari wa mbele katika kuivunja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hali ya Uchumi na uchambuzi wa Bajeti ya mwaka 2006/2007, kwa ruksa yako, naomba kurejea jukumu la msingi la Bunge kwa mujibu wa Katiba yetu. Ibara ya 63(2) inatamka kuwa “Bunge ndicho chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano ambacho kitakuwa na madaraka, kwa niaba ya Wananchi, kuisimamia na kushauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake.”

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inapenda kutamka wazi kuwa, inapohoji masuala yoyote ya Serikali, hatuna lengo la kупinga, bali ni katika kutimiza wajibu wetu wa kikatiba. Ibara ya 63(2)(a) inaweka wazi namna ya kutekeleza jukumu hilo, yaani kwa kumwuliza Waziri yeyote swali lolote kuhusu mambo ya Umma katika Jamhuri ya Muungano ambayo yako katika wajibu wake.

Mheshimiwa Spika, tunapohoji kuhusu Ndege ya Rais, na ninarudia hapa tena, siyo kwa sababu tunataka kujifurahisha, bali tunataka kufahamu na tunataka Watanzania wafahamu na waelewe ni kwa nini Ndege iliyonunuliwa kwa bei kubwa namna hiyo, haitumiki inavyotakiwa na kwa jinsi Bunge hili lilivyoelezwa wakati wa ununuzi wake. Huu ndiyo usimamizi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunataka kufahamu na tuna haki ya kufahamu na Watanzania wanataka kujuu kuna taarifa kuwa Ndege hiyo inatumia Shilingi milioni sita kwa kila saa moja inapokuwa angani, ni kweli? Kama kweli inatua tu viwanja vitano hapa nchini kati ya viwanja 23 vilivyopo na mamia ya *air strips* zilizopo, Kambi ya Upinzani inataka kufahamu fedha zilizotengwa katika kasma Na.98 ya Wizara ya Miundombinu ya programu Na.10 kasma ndogo ya 310500 ambayo imeandikwa “T” na wala haionyeshi ni kiasi gani kimetengwa kwa ajili ya “*Mobile, Vehicle and self Propelled Equipment*” ambayo ndiyo inalipia ndege hizo na Kasma ndogo ya 310800 yenye Sh. 700,000,000/=.

Kama ni kweli inawagharimu Watanzania Shilingi milioni sita kwa kila saa inayokuwa angani na mabilioni mengine mbali na gharama za ufundi ambazo mafundi wake tuliambiwa wanaagizwa kutoka Marekani kila wakati, Kambi ya Upinzani inashauri ili kuwapunguzia Watanzania gharama zisizo za lazima, zinazoendelea kujilimbikiza na kuwa mzigo kwa Watanzania, ndege hiyo iuzwe mara moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunapohoji hayo, tuna nia moja tu, kusimamia matumizi ya fedha za kodi kama tulivyosema na ni wavuja jasho wa nchi hii ndiyo wanaoumia. Tunapotaka Bunge au Kamati zake zipitie Mikataba ni kwa msingi huo huo. Mikataba iwe siri kwa mwenye mali, inawezekana?! Hii ni Mikataba mibovu, kama kweli Mikataba ya nchi hii ni siri kwa wenyewe nchi na hasa kupitia Wabunge amba ni Wawakilishi wao! Lakini kule kwao tulikoingia Mikataba, siyo siri kwa Bunge. Sisi tumejifunza wapi basi?!

Mheshimiwa Spika, tutauliza mpaka Watanzania wapate majibu ya kuridhisha. Kama ni kweli matumizi ya Shilingi milioni sita kwa saa ni sahihi wakati nusu ya wananchi wa Wilaya kama Geita wanaishi kwa mlo mmoja tu, tuna haki ya kikatiba kwa niaba ya Wananchi kupiga kelele. Chochote kinachoonekana kuwa sio matumizi mazuri liko ndani ya mamlaka ya Mbunge au mmoja mmoja au Bunge kuhoji Serikali na ni jukumu la Serikali kutoa majibu sahihi.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Mipango katika Hotuba yake ukurasa wa 58 Ibara ya 86 anazungumzia Mpango Maalum wa kuharakisha Maendeleo Tanzania au *Tanzania Mini –Tiger Plan 2020*. Mpango huu unasemekana umeanza kutekelezwa mwaka 2005 kwa kuzingatia uzoefu na mafanikio ya nchi za Kusini Mashariki mwa Asia. Kujifunza kwa wengine ni jambo jema. Lakini je, Mazingira ya siasa tuliyonayo, kihistoria, kijiografia yanafanana na huko tulikojifunza? Tumeyarekebisha kiasi gani kama hayafanani ili yalingane na yaza matunda ambayo yanategemewa? Kwa kiasi gani washauri na wasomi wetu wameshiriki katika maandalizi ya mipango hiyo? Kuna taarifa kuwa maandalizi ya mpango huo yametugharimu Shilingi bilioni saba: Je, kuna ukweli gani? Kama sivyo, Kambi ya Upinzani inapenda kufahamu ni kiasi gani basi kilitumika kuandaa mpango huo?

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Fedha katika hotuba yake anazungumzia MKUKUTA tu, lakini hagusii mipango mingine yote, yaani MKURABITA, *TMTP 2020*, MKUMBITA na wala *Tiger Plan 2020* ambayo majina mengine yanajirudia.

Je Waziri wa Fedha hana habari na mipango hiyo mingine? Kama hana habari, itatekelezwa vipi kama hakuweka mafungu yejote kwa utekelezaji wake? Au huu sasa ni utamaduni kama tulivyosoma kwenye Vyombo vya Habari, Waziri wa Fedha anakwenda Marekani kujadili bei mpya ya Umeme wakati Waziri mhusika hana habari na kweli baadaye bei imepanda! Serikali haikutoa tamko wala kukanusha habari hizo.

Je, kuliko kuwachanganya wananchi na misamati na majina yasiyo na mwisho kila kukicha, ni kwa nini Mipango hii isiratibiwe vizuri na kutoa Mpango mmoja Kabambe utakaotangazwa kikamilifu ili wananchi wauelewe na kuuensi vizuri kama

walivyoelewa Azimio la Arusha, japo sio wengi waliolipenda wala kulikubali Azimio la Arusha?!

Mheshimiwa Spika, sio ajabu tukipewa mtihani kuhusu majina, maana na malengo ya mipango hii humu ndani zaidi ya nusu tutafeli mtihani huo. Sembuse Mwananchi wa kawaida, ambaye mapambano yake ya kila siku ni kutafuta mlo wake wa siku kuliko kuhangaika na mchezo wa maneno ambao matunda yake hayaonekani angalau mara moja!

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani imestushwa sana na kauli ya Waziri wa Mipango katika ukurasa wa 56 ibara ya 83 kuwa, “Zoezi la kuainisha gharama za utekelezaji wa Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005 itaanzishwa.” Narudia: “Itaanzishwa rasmi katika kipindi hicho.” Nao Ukurasa wa 55 Ibara ya 82 na 83 unaonyesha kuwa hata gharama za MKUKUTA yenyewe haijaandaliwa bado.

Mheshimiwa Spika, kwa mchambuzi yejote anayefuata mantiki ya kinachoelezwa na Serikali na hasa kwa kupima maneno ya Mheshimiwa Waziri huyo huyo kama yalivyo kwenye Ibara ya 110 ya hotuba yake ambapo anataka kutumia Vyombo vyta Habari kama *Radio, TV, Tovuti na Magazeti*, nanukuu: “Kuhakikisha kwamba wananchi wanaelewa masuala muhimu yaliyobainishwa katika Ilani ya CCM.” Mwisho wa kunukuu. Kauli hiyo inatia dosari kubwa. Kama anakiri kuwa kazi ya kuainisha gharama ndiyo inaanza, atapeleka nini kwa wananchi?

Mheshimiwa Spika, kama gharama hizo kwa sasa hazijulikani, atahakikisha vipi kuwa ilani aliyoisifia sana katika hotuba yake inatekelezeka? Au ni kama vile ilani ya mwaka 1995 ilivyoelezwa kuwa haitekelezeki, tamko ambalo liliripotiwa sana na Vyombo vyta Habari na haikupingwa wala na Chama Tawala na Serikali yake?

Mheshimiwa Spika, lini Tanzania tutaacha kufanya majaribio ambayo hatima yake ni kutumuia fedha nyingi wakati maandalizi hayajakamilika? Ni kwa msingi huo, Kambi ya Upinzani inataka kufahamu ni vipi mipango inayotuhusu wote, inayotugharimu wote kwa njia ya kodi mbalimbali, hata kama imeibuliwa na Chama Tawala hatuna tatizo, lakini isiwe kwenye mjadala wa kitaifa ili sote kama Taifa tukubaliane na mustakabali wa maendeleo yetu? Ni vipi Ilani hiyo ya CCM inageuzwa kuwa Mpango wa Taifa bila kufuata utaratibu uliowekwa na Ibara ya 63(3)(c) ya Katiba yetu?

Tungependa kufahamu pia kule Urambo kulikuwa na ahadi ya umeme na Balozi wa Sweden aliwahi kutembelea na akaahidi. Tungependa kupata taarifa kamili ya utekelezaji wa mradi huo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007, tumeona kwamba yameongezeka kwa zaidi ya asilimia 17. Fungu 25 tunaitoa tu kama mfano lakini mfano pia kwa Wizara zote ambazo

zimetengewa fedha kwa ajili ya vitu vinavyoitwa *furniture*, samani na kadhalika, mwaka 2005 zilitengwa Shilingi milioni 95, mwaka huu na kwa upande wa magari kwa mfano kwa mwaka 2005 ilitengwa Sh. 95,000,000/= ikapanda kufikia Sh.237,000,000/= magari yamepanda toka Sh. 170,000,000/= kwa Sh. 600,000,000/=.

Mheshimiwa Spika, kwa kiwango chochote, nchi masikini ambayo inategemea ufadhili kwa Bajeti yake kwa asilimia 39, nchi ambayo wengi wa wananchi wake hawana uhakika wa mlo mmoja, nchi ambayo wananchi wamehamasika na kujenga Shule nyingi, nchi ambayo Shule za Sekondari hazina Waalimu wa kutosha, madawati, vitabu na vifaa vya Maabara au Zahanati hazina Manesi na Waganga, kiwango hiki ni kikubwa mno. Ofisi ya Waziri Mkuu ndiyo kiranja au msimamizi wa Wizara nyingine zote. Itawezekana vipi kwa wao kusimamia Wizara nyingine katika zoezi la kubana matumizi wakati wao wameonyesha njia katika matumizi makubwa?

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu ni mfano tu na katika mahesabu ya harakaharaka tumepata kwa Wizara 10 jumla ya bilioni 5 kwa ajili ya kifungu hiki cha 10300 yaani vifaa vya nyumbani na fenicha, tungependa maelezo ya kina na ni kwa nini vifungu hivi visirekebishwe hela ikapelekwa kwenye tija zaidi.

Mheshimiwa Spika, hakuna anayekufa kama mwaka mmoja *furniture* zisiponunuliwa, lakini tukafute upungufu wa Sekondari katika nchi yetu au tukaajiri Walimu wapya na Manesi kwa ajili ya Shule zetu za Sekondari na Zahanati. Ni suala la vipaumbele vyetu kutokuwa sawa. Tungependa kupata maelezo hasa kuhusu vifungu hivi vya vifaa vya ndani na hasa namna Ofisi yake itakavyosimamia Bajeti hii na kuleta tija kwa maeneo yale yanayoleta tija kwa maana ya kilimo, elimu, afya na maji.

Mheshimiwa Spika, suala la Serikali kuhamia Dodoma ni la siku nyingi na limekuwa sugu. Kamati ya Bunge mwaka juzi 2004 tena kwa kusindikizwa na Waziri Lukuvi, ilikwenda kutembelea kule Ofisi ya Dodoma Chimwaga ikaambiwa hii ndiyo Ofisi ya Waziri Mkuu. Sasa hatusikii tena chochote kuhusu hilo, japo tunesikia itakuwa Chuo Kikuu, lakini hatusikii kwamba kwa nini imeacha kuwa Waziri Mkuu kama tulivyoarifiwa na tukaendelea kwenda kuiangalia na tukatoa idhini iwe kweli Ofisi ya Waziri Mkuu.

Tungependa kupata maelezo ya kina tunapopata mabadiliko ya dharura namna hiyo na Bunge limehusishwa, halafu badiliko limefanyika na Bunge halihusishwi. Fedha nyingi zimetengewa na ukiangalia katika Bajeti ya *CDA* zimetengwa kwa ajili ya mishahara Sh. 1,149,285,000/=

Mwaka jana 2005 walipewa fedha karibu hizo hizo. Kazi walizopewa mwaka jana 2005 waliambiwa wataangalia mandhari na wataangalia vilevile *Nyerere Square*. Mwaka huu wanapewa Sh.427,000,000/= kwa kazi ya maendeleo, lakini wanaambiwa kwamba watafanya kazi hizo hizo japo Mheshimiwa Waziri Mkuu ameeleza kwamba wataangalia pia na kazi nyingine ikiwemo kugawa *plot*.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunakubaliana na kazi ya *plot*, lakini tunafikiri hela hizo ni nyingi na kazi hizo zingeweza kufanywa vilevile na Manispaa ya Dodoma, kwa sababu kazi ya kugawa *plot* iko ndani ya Mamlaka hizo na Manispaa imegawiwa Shilingi bilioni saba kwa ajili ya mpango wa kawaida na ina Shilingi milioni 63 kwa kazi ya maendeleo. Vinginevyo, tungeomba maelezo ya kina na kama hakuna mpango wa kuhamia Dodoma, basi tuelezwe. Kama Sera ya CCM ndiyo ilivyo, hatuna tatizo hatuingilii Sera yao, lakini inapofika Sera ya Chama inaingilia rasilimali ya wananchi, tutapiga kelele na ndiyo maana tunapiga kelele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, ni suala la UKIMWI. Tunatoshwa kabisa na Bajeti ya UKIMWI. Ukweli, iko hela nyingi kiasi cha Shilingi bilioni 26 na kwa upande wa Wilaya zimetengewa Shilingi bilioni 14 na zaidi.

Hata hivyo, Kambi ya Upinzani inapenda kutoa tahadhari kuwa pamoja na kutambua kuwa UKIMWI ni janga la Taifa mkakati ulio wazi unaoendana na dhana ya janga hilo haupo, tena tunafanya kazi kwa urasimu na pia tunatishwa na tatizo la Serikali kuteua Mawakala au TACAIDS kuteua Mawakala hao wameteua wao.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda wa kusitisha shughuli za Bunge umewadia, lakini ninayo machache tu ya kusema.

Kwanza, la ufanuzi wakati akiwasilisha hoja zake au tuseme maelezo, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Kamati yake ilitumia sana maneno “inaiagiza Serikali”, sasa kwa mujibu wa Kanuni 88(11) kuhusu mijadala ya aina hiyo na hata Kamati Teule, Kanuni 106 maneno yanayotumika ni “kushauri na kupendekeza.”

Ningeomba Kamati zizingatie hilo kwa sababu kwa mujibu wa Kanuni hizi sio kazi ya Bunge hili kuiagiza Serikali. Nitazisoma Kanuni hapa. Kanuni 88(11) na 106(3)(c) Kamati zinapendekeza na kushauri, ni kweli katika Kikao kingine Serikali ambayo haisikilizi tu ushauri wa Bunge, kuna namna ya kuishughulikia, lakini kwa sasa lugha ni hiyo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa na Kambi ya Upinzani, wamewasilisha hoja au tuseme wamechangia vizuri sana hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na uchambuzi unaonekana ni makini sana. Nafarijika tu kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu ni mtu makini, kwa hiyo nina hakika siku ya kujibu hoja, basi hakuna kitakachoachwa, tupate maelezo ili nchi iweze kuelewa mambo haya yanayosemwa. (*Makofi*)

Mwisho, ninao wachangiaji 90 kwa hoja ya Waziri Mkuu wakiwemo 12 amba walichangia kwenye hotuba ya Bajeti, lakini tutajaribu kwa kipaumbele kuona kwamba wale amba walioachwa hawajaongea waweze kupata nafasi kwanza na baadhi ya wale walioachwa wakati wa kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha nao waweze kupata nafasi.

Kuna moja nataka kueleza kwa ajili ya ufahamu. Ni kwamba, mchangiaji wetu wa kwanza saa 11.00 jioni atakuwa ni Mheshimiwa John Malecela Mbunge wa Mtera, atafuatiwa na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela na baada ya hapo Mheshimiwa Richard Ndassa na atafuatiwa na Mheshimiwa Luhanga. Nilikuwa nimemwomba Naibu Spika awepo kitini saa 11.00.

Kwa wale mnaokumbuka historia, Naibu Spika alikuwa ndiye Matron wa Mheshimiwa Anne Kilango Malecela wakati wa Ndoa. Kwa hiyo, mpangilio huu siyo kwamba ni upendeleo, asije akalaumiwa Naibu Spika kwamba labda anapendelea hawa maharusi wa siku hizo. Ni kwamba mimi nilikwishaipanga hii orodha kabla ya kumwomba Mheshimiwa Anne Makinda.

Kwa hiyo, ni utaratibu tu wa kawaida na taarifa tu ni kwamba ndugu zetu akina Malecela wamepata msiba, kwa hiyo kesho wanakwenda Same na pia Mheshimiwa Richard Ndassa nimemuwahisha kwa sababu anakwenda kwenye mazishi ya Mwenyekiti wa CCM mkoa wa Mwanza ambaye alifariki na baadhi ya Wabunge wa Mwanza wanakwenda huko. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa 11.00 jioni. (*Makofi*)

(*Saa 07:05 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11:00 jioni.*)

(*Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia*)

Hapa(Naibu Spika) Alikalia kitu

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, wakati tunasitisha shughuli za Bunge mchana, Mheshimiwa Spika, alikuwa amemtaja Msemaji wetu wa kwanza jioni hii ni Mheshimiwa John Samwel Malecela. Halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela na Mheshimiwa Richard Ndassa, ajiaande.

MHE. JOHN S. MALECELA: Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu kwanza na mimi niungane na wenzangu katika kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa kwa kura za kishindo na Watanzania na pia kwa historia ya jana ambayo amechaguliwa kwa kishindo kuwa Mwenyekiti wa Chama chetu, Chama Tawala, Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo hapo pia ningependa nimpongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar ambaye naye alichaguliwa kwa kura za kishindo na hatimaye kuwezesha Chama cha Mapinduzi kushika dola Tanzania na Tanzania Visiwani ambayo ndiyo utekelezaji wa Ibara ya 5 ya Katiba ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia nimpongeze sana Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Waziri Mkuu. Nimetumia neno kuchaguliwa

kwa sababu ingawa aliteuliwa na Mheshimiwa Rais, lakini ni Bunge hili hili lililompigia kura tena kwa wingi kabisa kumchaguliwa kuwa Waziri Mkuu wetu, nampongeza. Nina hakika kabisa kwa wote waliosikiliza hotuba yake ya leo watakubaliana nami kwamba Mheshimiwa Edward Lowassa, anastahili kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mimi nimebahatika katika siku za nyuma kufanya kazi na Mheshimiwa Edward Lowassa na nimemwona kwamba ni mtu asiyeyumba wala kuyumbishwa. Ni mtu ambaye akitoa amri anaitoa kwa unyenyevu na upole, lakini akiifua tilia, anafuatilia kama na nyundo ya chuma mkononi. Kwa hali hiyo basi, mimi nina hakika kabisa kwamba ufuatiliaji wa utendaji wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania umo katika mikono safi kabisa mikononi mwa Mheshimiwa Edward Lowassa ambaye ataifanya kazi hiyo kwa uwezo wake wote na mimi ningependa nimwombe kila la kheri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ningependa nianze kwanza kwa kusema naunga mkono hoja na naunga mkono hoja nikijua kwamba Awamu ya Nne hii ndiyo bajeti yao ya kwanza. Kwa hali ya namna hiyo kwa kweli mambo mengine wamelazimika kuyaweka kwa sababu kama Serikali ilivyoahidi haitavunja waliyoyakuta bali watayaendeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo katika hotuba yangu mimi ningependa kwanza niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote kwa kweli tumuunge mkono Waziri Mkuu kama tulivyomuunga wakati wa uchaguzi. Lakini katika kuunga huko mkono tukijua kwamba hii bajeti ingawaje tulipitisha kwa sauti moja, lakini haikuwa kwa uhakika ni ya Awamu ya Nne, ni kwamba wanakuwa wanamalizia ngwe za Awamu ya Tatu na kuanza za kwao. Kwa hiyo, mimi mengi nitakayosema itakuwa kwangu kama maombi kwamba kama hayawezekani sasa na nisipoyaona katika bajeti ijayo sasa hapo ndipo nitauliza kwamba kwa nini hili halimo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kusema kwamba leo kwa kweli nitasema kama Mbunge wa Mtera na nikiseme hivyo mtanisamehe sana kwa sababu nataka matatizo ya Jimbo la Mtera yajulikane kwa Serikali na kama ikiwezekana yachukuliwe hatua.

Kwanza, ningependa sana niishukuru Serikali kwa kasi waliyochukua na nguvu waliotumia na uwezo waliotumia katika kuwasaidia wananchi wa Mkoa wa Dodoma katika suala zima la uhaba wa chakula. Tunasema ahsanteni sana na hongereni kwa kuwa mlilichukua kwa haraka na kwa hiyo, ikawezekana kwamba Watanzania mpaka leo katika Mikoa yote iliyokuwa na upungufu wa chakula hakuna hata mtu mmoja aliyekufa kwa njaa. Tunasema ahsanteni sana.

Lakini la pili, nasema katika siku za usoni ili kuondoa njaa hasa katika sehemu za ukame, sehemu kama Dodoma, Singida, Shinyanga na sehemu fulani fulani za Tabora, sehemu za Arusha, basi tufanye yafuatayo:-

Kwanza, hizi mbegu zinazostahimili ukame safari hii tunaomba mzilete mapema. Tunajua safari iliyopita mlilet kwa dharura, lakini safari hii hizo mbegu mzilete mapema na mlete mbegu kwa watu wa aina mbili. Wale wanaojiweza ili waweze kununua na kwa wale wasiojiweza waweze kupewa mbegu mapema ili waweze kuzitumia kwenye mashamba yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia kutoa shukrani kwa Serikali kuamua kujenga Chuo Kikuu kikubwa na cha aina yake katika Tanzania kukijenga hapa Dodoma. Lakini hapo hapo ningependa kutoa wito kwa wana-Dodoma wenzangu kwamba sasa tukazane, twende tukajenga Shule za Sekondari, la sivyo tutakuwa wasindikizaji tu. Chuo Kikuu kitajengwa na sisi tutakuwa tunapita tunakiangalia, tunapeleka watalii wakakione, lakini sisi wenyewe hakitusaidii. Kwa hiyo, natoa wito kwa wana Mkoa wa Dodoma tujenga Shule za Sekondari ili vijana wetu waweze kufaidika na matunda tulioletewa. Maana yake katika siku za usoni hatutakuwa na sababu ya kusema kwamba oho sisi Dodoma, watasema lakini si Chuo Kikuu tumewajengea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ningependa tu tena niishauri Serikali. Hili nataka niseme nashauri kwa moyo wa dhati kabisa kwamba njia mojawapo ya kupunguza tatizo la njaa ni kuongeza *SGR* yaani Akiba ya Chakula ya Taifa. Kile kiwango cha tani 150 ni kiwango ambacho kimewekwa miaka 15 iliyopita. Sasa Watanzania wamekuwa wengi, Miji imekuwa mingi, na mahali kama Dar es Salaam wanahitaji zaidi ya tani 50,000 kwa mwezi kwa wale amba tu hawana mashamba au Vyuo au vyombo mbalimbali ambavyo vinahitaji kununua chakula. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa sasa niende kwenye matatizo ya Jimbo la Mtera. Mimi ningependa kwanza nikumbushe Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, alipowapeleka wananchi vijijini aliwaahidi mambo yafuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, Shule, Maji na Zahanati. Sasa mimi ningependa nichukue nafasi hii nitoe wito kwa Serikali kwamba katika haya mambo matatu bado jukumu letu ni kubwa sana. Ni kweli kwenye upande wa shule tumepeiga hatua sana na ni kweli kwenye upande wa zahanati mahali pengine tumepeiga hatua, lakini mahali pengi utakuta Kata nzima ina zahanati moja. Lakini kutokana na ahadi ya Baba wa Taifa kwamba zahanati kuwa katika kila Kijiji kwa sababu watu walivyokwenda kukaa kwenye vijiji, hivi vitatu walivichukua kwamba ni vitu ambavyo wanastahili wala wasiendelee kuviomba. Kwa hiyo, mimi ningemba sana vitu hivyo tuvitilie mkazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningependa niseme kuhusu Dodoma. Kwa Dodoma tunaomba mabwawa na visima virefu vya maji. Nikisema juu ya jambo hili la maji pengine ingekuwa ni vizuri Waziri wa Maji akaenda kuangalia *record* za nyuma. Katika miaka ya nyuma tuliwaahidi Watanzania nini? Atakuta kuna wakati tulisema kwamba ifikapo mwaka 2000 kila Mtanzania atakuwa na maji safi. Sasa mimi nataka niseme mimi kwenye Jimbo langu bado watu wanakwenda kilometra 6, 7 mpaka 10 kuchota maji. Sasa mimi kwa kweli kama nilivyosema sitazamii miujizi, lakini ninatazamia kwamba katika bajeti itakayokuja hili tatizo la maji hasa kwenye Mikoa ya ukame kama vile Dodoma, Arusha, Singida, Shinyanga hivi tutaahidiwa mpaka lini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningependa katika siku za usoni nione mpango kabambe unaoshughulikia Mikoa yenye matatizo ya maji. Mheshimiwa Waziri Mkuu tunakupongeza sana kwa uwezo ulioutumia wakati ukiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo kuleta maji ya *Lake Victoria* kufika mpaka Shinyanga na kadhalika. Kwa kweli tunasema hilo ni jambo la kujivunia. Lakini mimi naomba kwamba Mikoa yenye ukame tafadhali iangaliwe kwa umakini katika siku za usoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu nisemee jambo moja tu la jumla. Hapa tumeona mara nyingi sana wanazungumza habari ya watoto wa mitaani, watoto wasio na makazi maalumu. Lakini watoto hawa hutokana na kuvunjika kwa ndoa, hutokana na waume kukana watoto wao. Lakini pia upo upande mwingine sehemu ambayo mwanaume anasema huyu mtoto ni wangu, lakini mama anasema hapana siyo wa kwako, anampeleka kwa mtu mwingine na hasa ikiwa wewe mwanaume huna uwezo unasema mwanangu huyu, anasema hapana huyu mtoto si wa kwako ni wa fulani.

Sasa mimi nasema kwamba Serikali ya Tanzania kwa sababu hili kweli ni tatizo kubwa na kwenye Mahakama, tulete vyombo vya kupimia *DNA*. Mimi sidhani Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba chombo cha namna hiyo kitakuwa cha gharama kubwa sasa tukinunue ili hicho chombo kikishasema huyu ni mtoto wako basi huna cha kusema tena kunakuwa hakuna ubishi, nikimwambia mwanamke kwamba huyu mtoto wangu basi *DNA* inaonyesha kweli ni wa kwangu anipe badala ya kumpeleka kwa mtu mwingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa nisemee juu ya wafugaji. Mheshimiwa Waziri Mkuu ningependa niombe kwa makini kweli suala la wafugaji tuliangalie. Mtu ametembea kwa mguu kutoka Shinyanga, Maswa Meatu mpaka katika Bonde wa Usangu, mtu ametembea kutoka Hanang kwa mguu yeye na watoto wake na mara nyingine mimi nimewaona watoto wanawekwa kwenye mashogi halafu wanawaweka kwenye punda, kusafiri maili hizo mpaka huko, halafu kufika pale kweli ni sawa tunasema kwamba mazingira wanayeharibu, lakini hivi ukweli ni nini? Hivi anayeharibu mazingira kati ya ng'ombe na binadamu ni nani? Ng'ombe hali miti, wanaoharibu mazingira zaidi ni sisi binadamu. Lakini hivi sasa utaona kana kwamba wafugaji kama hatuwataki. Hebu siku moja wakubaliane wote wasichinje ng'ombe utakuta malalamiko yatakayotokea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi kwa hiyo, ningependa Ofisi ya Waziri Mkuu iwaangalie wafugaji kwa jicho la huruma kwamba wasiswage swage. Kuna wakati tulikuwa tunahangaika kupeleka mifugo Kusini. Watu walikuwa wanalia jamani na sisi tunataka mifugo. Sasa wananchi wamejitolea wenyewe tunaambiwa mara tuseme huku hapana, mara huku hapana. Kwa hiyo, mimi ningesema pamoja na mazingira kwanza nasema binadamu ndiyo mharibifu mkubwa wa mazingira tusisingizie mifugo. Wafugaji mara nyingi ni watu wanaotii sana Serikali, wakiambiwa hapa acha, wanaacha, basi tuwatengenezee mazingira ambayo na wao watajiona wako katika Tanzania ya leo. Tuwatengeneze majosho, malambo ya kunyweshea ng'ombe wao na tuwawezeshe kununua madawa ya mifugo na madaktari wa mifugo waweze kupatikana kwa urahisi.

Ningepende nisemee tena neno lingine nalo ni upande wa kilimo cha umwagiliaji. Sasa katika suala nzima la kilimo cha umwagiliaji tunayo mabonde mengi ambayo yamepimwa katika nchi hii na mimi ningependa tu niseme bonde moja ambalo Serikali imekwishalipoteza.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika
muda wa Mzungumzaji)*

MHE. JOHN S. MALECELA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.
(Makofi)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kabla ya Mheshimiwa Anne Malecela, hajasema, ningependa kusema tunao wageni wengine Wajumbe wa Kamati ya Siasa wanatoka katika Jimbo la Fuoni ni wageni wake Mheshimiwa Ameir Ali Ameir. Tunawakaribisha. Mnasimama na kuinama. *(Makofi)*

MHE. ANNE K. MALECELÀ: Mheshimiwa Naibu Spika, tulielewana na Mheshimiwa Mbunge wa Mtera kwamba kwa sababu sisi ni mwili mmoja yeye ashukuru kwa niaba yangu ili mimi nipaye mrefu wa kuzungumza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi naomba nianze kuzungumza moja kwa moja. Kwanza, naomba niipongeze Ofisi ya Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri na endelevu. Pili na hapa niipongeze Serikali ya Awamu ya Nne kwa kuanza kazi kwa kasi nzuri inayoonyesha mwelekeo mzuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi wakati tunapata Uhuru mwaka 1961 ni kweli nilikuwa mdogo. Lakini nakumbuka tangu nimepata akili mpaka sasa hivi umri wangu ni mkubwa kiasi sijawahi kumsikia Mheshimiwa Rais wa Tanzania aliyejkenda nje ya nchi yetu akaomba misaada, lakini akataja Wilaya ya Same moja kwa moja. Naomba niipongeze kwa nguvu zangu zote Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne kwa kitendo cha kipekee alichokifanya alipokwenda kwenye ziara zake za nje na akaiombea Wilaya yangu ya Same maji salama. Kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Same, Same Magharibi na Same Mashariki tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kitendo hicho na Mungu amsaidie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa na usongo mkubwa na hii hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na sababu kubwa ni moja ni kweli hali yangu leo siyo nzuri. Lakini naomba nizungumze *seriously*.(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Chama cha Mapinduzi ilipoamua kwamba inapeleke madaraka Mikoani, nafikiri mwaka 1974 ilikuwa na nia nzuri sana kwamba kule Mikoani maendeleo yaende kwa haraka mpaka Vijijini, basi ikapeleka nguvu kwenye Halmashauri zetu za Wilaya na Manispaa, Serikali ilikuwa na nia nzuri. Lakini Halmashauri zetu za Wilaya hazifanyi kazi vizuri. Serikali Kuu inatuma fedha nydingi sana ndugu zangu kupeleka kwenye Halmashauri za Wilaya, lakini fedha zile haziendi inavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefanya utafiti hiki ni kipindi changu cha pili na mimi ni Diwani, nilikuwa Manispaa ya Kinondoni na kipindi hiki nipo katika Halmashauri ya Same, hapana kazi haziendi zinavyotakiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe mfano, Miradi ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini bajeti hii ya mwaka 2006/2007 Serikali imeleta miradi mitano ya maji kwa sababu nilimwomba Waziri wa Maji anipe hii *document*. Serikali imepeleka katika Jimbo la Same Magharibi, Kisungo, Bonjaza, Malindi, Mteke na Hedaru. Katika Jimbo la Same Mashariki imeletewa miradi mitano, Miombo, Sambweni, Nunguru, Ivunga na Bendera.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nitakuwa napata miradi mitano, mitano kwa miaka mitano na ikisimamiwa vizuri na Halmashauri yangu ya Same hatuwezi kuwa na umaskini uliopo sasa. Kwa hiyo, ndugu zangu Halmashauri ndiyo zinazotutia umaskini siyo Serikali Kuu. Halmashauri zinatutia umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi naomba nizungumze tofauti na hotuba ya Upinzani. Hatuwezi kuiachia Serikali Kuu yenewe ikasimamia jambo hili, hapana. Waheshimiwa Wabunge wa Majimbo, mimi naomba nitoe wito ifikapo wakati wa vikao vya *Council* tuombe ruhusu tuondoche hapa Bungeni, twende huko, twende tuhudurie vikao vya *full council* vyote tusiache hata kimoja na tusihofu kuwaliza maswali hawa watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tusihofu sisi tulisimama miezi minne kwenye majukwaa tukaomba kura kwa wananchi nia yetu ilikuwa ni kuwafanya kazi wananchi wa Tanzania sio kuwafurahisha watendaji. Nimegundua unapomhoji anakasirika, lakini mimi sikuomba kura nimfurahishe yeye. Akikasirika, anayekasirika ni yule ambaye hafanyi kazi yake kwa uadilifu. Ukimwuliza hii barabara viperi aah, Mheshimiwa nina kazi nyingi. *No!!* Watujibu.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba nitoe wito kwa Wabunge wenzangu *full council* tuhudurie kama tunavyohudhuria vikao vya Bunge. Tuhoji fedha za Serikali, kwa sababu Serikali haiwezi kuhamia kwenye Halmashauri zote za nchi hii lakini sisi Wabunge wa Majimbo tuko kule na tunaangalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiangalia miradi ambayo tunaletewa fedha na Serikali tutapiga hatua kubwa sana. Kwa hiyo, rai yangu kubwa kwa wenzangu jamani twendeni kwenye *full council* kila wakati tukasaidiane na Madiwani. Madiwani hawawezi wale watendaji wakorofi kweli kweli. Lazima wakutane na sisi na sisi tuwe imara, kila mtu ajifunze kuwa mkorofi, ili mradi unakuwa mkorofi kwa kujenga nchi yako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe pongezi kidogo kwa Naibu Waziri wa Maji na Waziri wa Maji Mzee Wassira. Tena wale wenye dhana potofu kwamba Mzee Wassira ni mzee wasirudie hilo. Ni Mbunge mzee lakini mchapakazi sana. Unamhoji jambo linalohusu Wizara yake asubuhi jioni amekuletea barua ina maelezo na anafanya kazi. Kwa hiyo ndugu zangu msione kwamba kuwa kijana ndiyo kujuu kufanya kazi, Wassira ni mzee lakini ni mchapakazi. Naomba apokee hizo sifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongee jambo lingine ambalo lipo. Tunazo Wilaya nyingi sana ndugu zangu ambazo zina jimbo zaidi ya moja, majimbo mawili au matatu. Dar es Salaam Wilaya ya Kinondoni ina Kinondoni, Kawe na Ubungo. Majimbo ya namna hiyo yako mengi. Nimefanya *research* nzuri sana Serikali inapopeleka miradi inapeleka vizuri sana mitano huku, mitano huku. Ndugu zangu wa Halmashauri mnaoleta ile miradi kuomba fedha Serikali Kuu miradi ya *immediate measures* mfuate mfano wa Serikali. Kama ni matatizo ya maji ni majimbo yote yana matatizo ya maji. Yale matatu yote yana matatizo ya maji. Unaleta miradi kumi unaiombea fedha minane unapeleka jimbo hili, majimbo yale mengine mawili ni hatari kubwa. Tutajenga katika Wilaya moja jimbo ambalo ni *paradise* na jingine ni *jehanam*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasihi Serikali Kuu muwaelekeze Halmashauri kwamba majimbo 232 yote yapate fursa sawa. Hilo nilikuwa naomba tu kutoa maombi

kwamba Serikali Kuu simamieni Halmashauri zitafanya mambo ya kiajabu kweli kweli katika kuomba miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nizungumzie barabara zangu, jamani hili ni tatizo kubwa. Barabara zangu za Same Mashariki lakini Same kwa ujumla Mashariki na Magharibi, Same yote. Mimi nimeweza kuhudhuria mukutano sibakishi mikutano, Bodi ya Barabara Mkoa wa Kilimanjaro. Kwa hiyo barabara zote za Mkoa Kilimanjaro nikapewa picha yake. Barabara ya kutoka Mkomazi kwenda Ndungu, Kihurio, Mahore mpaka Same ni barabara ya Taifa (*Trunk Road*). Lakini ndiyo barabara pekee katika Mkoa wa Kilimanjaro ambayo ni *unpaved*, haina lami. Si kwamba haina lami tu barabara hii haina hata changarawe ni ya udongo. Lakini naomba niwakumbushe hasa mtu kama Mheshimiwa Edward Lowassa atakuwa anakumbuka. Zamani kulikuwa na *East African Road* unataka kwenda Nairobi ilikuwa lazima unapita barabara hiyo ndiyo ufile Same uende Moshi uende Nairobi. Barabara hii ina hadhi kubwa. Hadhi ya barabara ni uchumi wake. Ukienda unaanzia Bendera kuna hekta 300 za mpunga zinalimwa pale, ukienda kata yangu wa Kihurio, mimi nimelelewa na wali, ugali nakula nikipenda hekta 1,200 kuna Mto wa Saseni una maji miezi 12, tunavuna mpunga mara mbili. Ukienda Ndungu kuna mradi wa umwagiliaji maji wa Wajapan jamani ambaa una thamani zaidi ya bilioni mbili. Wale wanavuna mpunga mara mbili kwa mwaka na mahindi. Ukienda Mahore wao ni matajiri kuliko kata zangu zote kwa sababu wana Mto Hingillili una maji mengi miezi 12. Ukienda kisiwani ni kata ya Magharibi ina hekta 350 wanalima mpunga wanakwenda Same. Barabara hii *surplus* hatujui sijui tuipeleke wapi? Tunavuna, hatuna njia ya kupelekea mazao yetu ya ziada kwenye masoko makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninazo kata 8 milimani zina hekta 2,040 wananchi wanalima tangawizi, hiliki, kahawa kidogo, ndizi hawa ndio wenye ziada kuzidi kiasi, tupeleke wapi mazao yetu. Walangazi sasa ndio wanakuja wanachukua tu. Pia ielewewe hatuna soko la karibu lazima twende Tanga, Dar es Salaam au Moshi, mpunga wa Same Mashariki mchele ule unalisha mkoa wa Tanga, Kilimanjaro wote mpaka mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina barabara nzuri, kwa hiyo, ni kwamba ile ziada wanakuja walangazi wanachukua na wanapochukua wanawapa wananchi bei ya chini zaidi ya hapo baya kuliko yote jamani kama hamjui Same ni Halmashauri tegemezi wanashindwa kukusanya mapato maana yake walangazi wanafirisha mchele saa 8 usiku. Hakuna mapato ukiwaliza kwenye msimu wa 2004/2005 mwulize kata ya Mahoro wamekusanya shilingi ngapi Halmashauri ya Same itakwambia imekusanya 110,000. Shilingi 110,000 ni lori moja tu la *Fusso* sasa kila gunia moja la kilo 100 ni shilingi 1,000. Mapato yanapotea hatupati mapato kwenye Halmashauri ya Same.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli kipindi hiki siwezi kuilalamikia Serikali ya Awamu ya Nne. Si bajeti yake haswa, lakini naomba mnifikirie kwamba barabara yangu hii ndiyo pekee katika mkoa wa Kilimanjaro ambayo si bora haina changarawe wala si pana ya kutosha na aina mfano. Namshukuru Mheshimiwa Waziri Mramba.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipokuwa kwenye Bodi ya Barabara nilieleza vizuri akamwambia Mkuu wangu wa Mkoa ashirikiane na *TANROAD* waende wakaziangalie barabara zangu nashukuru Mkuu wangu wa Mkoa aliitikia mara moja alifanya ile kazi na nafikiri yuko hapa ameleta ripoti kwa Mheshimiwa Waziri. Nitaomba ripoti yake ifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee sasa suala la jamii ambalo linanigusa sana. Kwa ruhusa yako naomba ninukuu Ilani ya Uchaguzi ukurasa wa 164, naomba kunukuu hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tatu aliyoitoa Bunge la zamani tarehe 29 Julai, 2005 alisema hivi: "Lakini kuongoza ni kuonyesha njia ni kuwa mfano bora ni kuwafanya wananchi waridhike kukuona uko mbele na wao wanakufuata. Wanakufuata si kwa sababu wanakuogopa, kwa sababu wanakuamini na imani ya kweli haipatikani kwa kauli tu bali hasa kwa vitendo vyako, mwelekeo wako na kuwajali wananchi."

Mheshimiwa Naibu Spika, wiki iliyopita niliuliza swali ambalo nafikiri lilikuwa halikuelewaka vizuri kuhusu watoto yatima. Watoto yatima ni watoto wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na katika bajeti aliyosoma Mheshimiwa Waziri Mkuu anazungumza kwamba tuna watoto yatima zaidi ya 1,200,000. Lakini hawa watoto ni wetu na ni wa kila mtu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofî*)

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi jioni hii na mimi nichangie hotuba hii ya Waziri Mkuu. Kabla sijaanza kusema naomba nianze kusema kwamba naiunga mkono asilimia mia moja. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ni tarehe 26 Juni, 2006 Mheshimiwa Waziri Mkuu hii ndiyo hotuba yake ya kwanza hii ni rekodi kwako Mheshimiwa Waziri Mkuu utaiandika na nikupongeza kwa hotuba nzuri kabisa yenye matarajio na mategemeo kwa Watanzania wote. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mchangiaji wa asubuhi ndugu yangu wa Kambi ya Upinzani, kaka yangu alisema maneno fulani kidogo tu lakini naomba na mimi nieleze kama ifuatavyo, watendaji watafuata Ilani ya Chama cha Mapinduzi na maelekezo ya Serikali iliyoko madarakani si vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pili, kwa sababu huu ulikuwa ni uchaguzi wa kwanza wa kutumia daftari la wapiga kura si vizuri kuanza kuibeza Tume ya Uchaguzi. Tuishukuru na kuipongeza kwa kazi nzuri iliyofanya. Lazima makosa yawepo ni mara ya kwanza. Naomba nimshukuru sana msimamizi Mkuu Bwana Rajab Kiravu, kwa kazi nzuri aliyoifanya. Lakini si vizuri sana wenzetu kulaumu kila siku lazima kuna vitu vingine mshukuru. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo niseme tena kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hotuba yake amejielekeza kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. Bahati nzuri ameanza kusema majukumu yaliyoko mbele yetu ameya-solve.

Mimi nitakwenda ukurasa wa 22 inapozungumzia kuhusu kilimo. Kilimo cha kisasa ndio msingi wa uchumi wa kisasa, (a) pale. Wakulima walio wengi hawajajibwa na kutekeleza kanuni za kilimo bora za mazao wanayoyalima, hivyo kilimo chao hakina tija na mavuno yao ni kidogo, hili ni kweli.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, mimi naomba kusaidia kama ifuatavyo, ili tuongeze tija katika kilimo chetu lakini katika kitabu chako umetuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba Waheshimiwa Wabunge mshiriki kikamilifu katika usimamizi wa suala hilo. Kuhusu suala la chakula mimi nilikuwa na mapendekezo yafuatayo hasa upande wa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, hifadhi ya chakula, mtu mmoja kwa mwaka hutumia magunia matatu ya mahindi, kama una watu wanne nyumbani kwako kwa mwaka mzima utatumia magunia tisa. Kama una watu watano nyumbani kwako utatumia magunia 12 kwa mwaka mmoja. Kama utaweza kula ugali peke yake utatumia magunia 12 kwa watu watano. Gunia moja la kilo 100 na bahati nzuri kwa sababu Ma-RC wako hapa na hili ni agizo la Waziri Mkuu na umesema na sisi tushiriki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa mtama mtu mmoja hutumia magunia matatu kwa mwaka mzima, watu watano hutumia magunia 12 ya mtama, kama watakuwa mtama peke yake mchana na jioni. Kwa upande wa mpunga mtu mmoja hutumia kwa mwaka mmoja magunia matano. Lakini watu watano kwa mwaka mzima watatumia magunia 27 kama watakuwa wanakula mpunga kwa maana ya mchele peke yake kwa mwaka mzima. Sasa kwa sababu Mheshimiwa Waziri Mkuu ametuomba tusaidiane kule vijijini tuwaombe wananchi wetu, tupime kaya zetu tuna watu wangapi kwenye miji yetu ili chakula hiki kiweze kutunzwa. Kama wewe una watoto wanne una watu kule nyumbani kwako kwa mwaka mzima utatumia magunia tisa.

Mheshimiwa Waziri Mkuu hii ndiyo *formula* ya kilimo ya utunzaji wa chakula. Lakini haya mahindi au mtama tutaupataje? Lazima twende kwenye kilimo cha tija na bahati nzuri katika hotuba yake umesema na bahati nzuri kwenye ilani yetu imesema sisi bahati nzuri tunalima bila kufuata utaratibu, tunalima kiholela. Ili tufuate utaratibu wa kulima vizuri na tupate mazao mengi upande wa upandaji wa mahindi hekta moja kama ikipandwa vizuri kwa kufuata utaratibu kwa maana ya sentimita 90 kwa 30 utapata mimea 37,000 na mavuno yake ni magunia 47 mpaka 67 kwa hekta moja. Kama utalima mtama na haya mahindi unatakiwa upande mmea mmoja mmoja.

Kwa upande wa mtama kama ukipanda vizuri sentimeta 60 kwa 15 utapata 111,000 mavuno yake ni magunia 22 mpaka 28 kwa hekta moja. Lakini kwa wale ndugu zangu kwa zao la biashara la pamba tunatakiwa tupande mbegu mbili mbili si zaidi ya hapo kwa sentimeta 90 kwa 40 tutapanda mimea 56,000 na mavuno yake tutapata kilo 1,000 mpaka 1,600 hicho ndicho kilimo cha tija tunachokitaka leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, endapo tutafuata utaratibu huu bahati nzuri mwananchi alime heka 2 afuate utaratibu wakati tumesema kwamba hekta moja inatoa magunia 47 kwa maana hekta 2 utapata magunia 88 hapatakuwa na njaa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Njaa tunaitafuta sisi wenyewe kwa sababu tunapanda bila utaratibu. Naomba kwa sababu wataalamu wako hapa, Ma-RC wako hapa na Ma-DC nafikiri wanansikia huko walipo ili tuondokane na suala la kuhemea chakula kwa sababu kwenda kuomba chakula ni aibu, naomba tukasimamie kilimo chetu kiwe cha tija. Lakini ili tuyafanye hayo naiomba Serikali tunavyo vyuo vyetu, tunayo Sokoine, Ukitiriguru, Uyole, Tengeru na kadhalika wale maafisa ugani wako wapi, wanaozalishwa kwenye vyuo hivi wenyе Digrii, *Diploma* na *Certificate* wako wapi? Kwa sababu haya niliyoyasema ya kupanda sentimeta 90 kwa 40 bila ya kuwa na maafisa ugani kilimo chetu kitabaki pale pale hatutasonga mbele. Tunataka tuendeleze kilimo kisonge mbele na ili kisonge mbele lazima maafisa ugani waende vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa Wilaya ya Kwimba tunao maafisa ugani 27 tu, tunahitaji maafisa ugani 84. Naiomba Serikali ili tutekeleze haya lazima tupate maafisa ugani 84 pamoja na vifaa vyao kama pikipiki na magari na kadhalika hapo ndipo tutakuwa tumefanya kazi nzuri ya kutekeleza kilimo cha tija. Lakini nizungumzie la pili kuhusu makato ya pembejeo niliuliza swali hapa Mheshimiwa Naibu Waziri alijibu vizuri lakini naomba kuweka msisitizo makato haya wananchi wamekuwa hawapati faida nayo hata kidogo. Kwa sababu tunaambiwa kwamba kwa mwaka 2003/2006 kwa Mkoa wa Mwanza walikusanya jumla ya shilingi 4 bilioni lakini hawa wakulima wa zao la pamba wanapokwenda kuomba kule kwa sababu wanazo zile *passbook*, wanapokwenda kuomba turudishiwe fedha zetu wakati wao hawakutumia yale madawa pamoja na mbegu wale watu wa *Tanzania Cotton Marketing Board* wanasema hapana kwa sababu hukua kuchukua basi na fedha zako hatukupi. Naiomba Serikali fedha hizi ni za wakulima tunaomba kama namna gani basi wazitumie kwa awamu ijayo au vinginevyo fedha hizi warudishiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho naomba niishukuru sana Serikali kwa kazi nzuri iliyofanya. Nimeambiwa na Naibu Waziri wa Nishati na Madini niliomba Serikali kwamba naomba umeme upelekwe Sumve na Malya, nimeambiwa kwamba ikiwezekana kesho umeme utawashwa Sumve. Naipongeza kwa dhati Serikali naomba sehemu iliyobaki ya Malya basi umeme upelekwe kwa sababu vifaa vyote viro na sehemu ya Mvomero nako lipo tatizo la ukosefu wa umeme vifaa viro naomba vifaa vipelekwe ili kusudi Mvomero nayo ipate umeme sehemu ya Mngeta. (*Makofi*)

Mwisho Mheshimiwa Rais aliwaagiza watu wa *Tanzania Football Association* kwamba tutafute mwalimu wa mchezo wa mpira wa mguu inashangaza kama sio kusikitisha mpaka leo wamekaa kimya. Kama hajapatikana hivi midomo si mnayo Mheshimiwa Joel Bendera yuko pale mtaalamu kwa nini msiseme kwamba bado tunafanya utafiti huu na huu ili mseme kwa sababu mkikaa kimya hata kama ninyi mtakuwa mnajua kwamba mmekwama kitu fulani lakini wale wananchi hawajui kutoa taarifa ni nzuri zaidi. Tunaomba mtoe taarifa mmekwama nini ili wananchi wajue kuliko kuwa wanasema kwamba hawa hawataki kutafuta kocha wagoni, wanataka makocha wao wa ndani. Naiomba sana Serikali hasa Wizara ya Michezo suala la kocha litafutiwe ufumbuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo niseme tu kwamba naunga mkono hoja. Tanzania yene neema. Ahsante sana. (*Makofit*)

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli mimi ni mgumu sana wa kusema pongezi lakini nasema nampongeza sana Waziri Mkuu Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, kwa hotuba nzuri aliyoisoma, hotuba ambayo inaonyesha kulenga kutatua matatizo ya wananchi wetu. Naishukuru sana Serikali kwa kuweka shilingi milioni 500 kwa kila mkoa kwa ajili ya uwezeshaji wa wananchi kiuchumi na ajira nchini. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niseme nianze kuchangia moja kwa moja kwa sababu muda usije ukaniishia nikiendelea kutoa pongezi. Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na Halmashauri za Wilaya pamoja na Manispaa. Kwanza niseme kwamba nazipongeza sana zile Halmashauri za Wilaya 62 zilizopata hati safi. Niipongeze sana Wilaya yangu ya Meatu kwa kupata hati safi. Nampongeza sana Mweka Hazina wangu Ndugu Sembugabo pamoja na timu yake kwa kazi yao nzuri kuiletea hati safi Wilaya ya Meatu. Kuna Halmashauri zile 51 zilizopata hati yene masharti, kuna Halmashauri 4 zilizopata hati chafu. Kwa kweli mimi sioni sababu ya kwa nini Halmashauri hizi zinapata hati chafu, kwa nini zinapata hati yene masharti. Miongozo ipo, kanuni zipo, taratibu zote za fedha wanazo kwa nini wanapata hati chafu, kwa nini wanapata hati za masharti. Lazima watendaji hawa tuwatazame hawa mara mbili lazima hatua zichukuliwe dhidi yao hatuwezi kuendelea tu kusema wanapata hati chafu sisi tunaendelela tunawatazama tu. Wanapata hati zenye masharti tunaendelea tunawatazama tu kwa nini wapate hati za masharti.

Mheshimiwa Naibu Spika, miongozo yote ipo na uzembe huu umesababisha hasara kubwa sana kwa wananchi wetu. Umepelekea baadhi ya Halmashauri kushindwa kukidhi vigezo vya kupata fedha za maendeleo (*Government Support Programme*) wameshindwa. Baadhi ya Halmashauri zimekosa *in terms of billions*, kuna Halmashauri zingine zimekosa zaidi ya shilingi bilioni moja kwa sababu ya kushindwa kukidhi vigezo vinavyotakiwa. Ukitisoma vile vigezo ni vya kawaida kabisa lakini kwa nini wanashindwa kuvififikia. Sasa fikiria Wilaya inapata hasara ya shilingi bilioni moja ya maendeleo kwa ajili ya uzembe wa mtu tu. Lazima watendaji hawa sasa huu ni uzembe wa hali ya juu ni lazima hatua kali zichukuliwe kwa watendaji wa namna hiyo. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niseme kwamba kwa kuwa sasa hizi Halmashauri ambazo zimekosa vigezo kwa sababu kadri Halmashauri zote zilitengewa hizi fedha *LGSP* zilitengewa fedha ili kwamba wakikidhi viwango waweze kupewa zile fedha. Lakini kuna Halmashauri zilizokidhi vigezo lakini kuna Halmashauri zilizoshindwa kukidhi vigezo. Mimi nasema kwa sababu hizi fedha zilikuwa zimetengwa basi zile Halmashauri zilizofanya vizuri kwa kufanikiwa vile vigezo pamoja na zile za kwa ambazo wamepata tayari basi hizi za Halmashauri ambao wao wamefeli bado wanajiandaa kimaendeleo hizi fedha ziwekewe zile Halmashauri zilizofanya vizuri ili ziweze kufaa kimaendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwa nimechangia Halmashauri sasa niende kwenye Utawala Bora. Utawala Bora unawezekana tu katika eneo ambalo unaweza ukalimudu kiutendaji kazi. Katika Halmashauri zetu toka mwaka 2004 katika Halmashauri yangu ya Wilaya ya Meatu tulipendekeza usajili wa vijiji, tulipendekeza kuvigawa vile vijiji vikubwa ili viweze kutawalika na huduma iweze kuwafikia wananchi katika muda muafaka.

Katika vijiji hivi vimejitokeza kuwa na idadi kubwa ya watu, kuna ongezeko kubwa la kaya, kuna umbali wa kutoka jumuiya fulani kwenda jumuiya nyine kiasi kwamba wasimamizi wa shughuli za maendeleo walinzi wa amani amba ni watendaji wa vijiji katika maeneo hayo wanashindwa kumudu maeneo makubwa hayo kuyatawala.

Kwanza watendaji wetu hawa amba tunawahitaji washughulikie shughuli hizi za maendeleo, washughulikie shughuli za ulinzi hawana usafiri, lakini unakuta kwamba tunawapa jukumu kubwa kijiji kimoja sawa na kata nzima mtendaji huyo ambaye hana hata baisedhi anawezaje kumudu eneo hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda nitolee mfano kwamba katika Wilaya yangu ya Meatu tulipendekeza vijiji 25 viweze kusajiliwa vigawanywe mara mbili toka mwaka 2004 mpaka leo hakuna. Kuna vijiji kwa mfano Mwanduichinde, kina kaya zaidi ya 300 na watu wanaoishi ni zaidi ya 3000, lakini kijiji kilichopendekezwa ambacho ni Sangijo chenyewe kina zaidi ya kaya 270 na watu wake ni zaidi ya 200. Kuna kijiji kingine kinaitwa Longalonigha kina zaidi ya ya kaya 400 watu wanaoishi ni zaidi ya 2000, kijiji kilichopendekezwa ambacho ni Matale kina zaidi ya kaya 270 na watu wanaoishi ni zaidi ya 150. Kuna kijiji kingine kinaitwa Mwakisandu kina kaya 300, watu wanaoishi hapo ni zaidi ya 4000 lakini kijiji kilichopendekezwa ambacho ni Mwanindwa kina zaidi ya kaya 250 na watu wanaoishi hapo ni zaidi ya 2500. Katika kusema kwamba kijiji kilichopendekezwa na kijiji mama ni zaidi ya kilomita saba, Mtendaji huyu anamudu vipi majukumu hayo.

Mimi sioni sababu ya kuwa na kigugumizi katika mambo ambayo hayana hata gharama kubwa suala kugawanya vijiji halina gharama kubwa gharama labda ni kulipa watendaji wa vijiji lakini watu wetu wakapata haki zao za msingi wakapata huduma zao za msingi kwa muda muafaka. Sisi vijiji vyote hivyo 23 katika Bajeti ya Halmashauri ya Wilaya ya Meatu tumekubaliana kabisa kwamba kwanza tunalipa wenyeviti wa vitongoji, tunalipa wenyeviti wa vijiji na katika wenyeviti wa vijiji wale 23 amba tunawaombea katika vijiji vipyta tulipendekeza Bajeti yao iingizwe.

Naomba sasa Serikali ilione hili, ilione uzito kwa hawa watendaji wetu wadogo walioko kule chini ule ugumu wanaopata katika kumudu madaraka yao na hatimaye kushindwa kutekeleza utawala bora. Vijiji hivi vipate usajili ikiwezekana mimi Mheshimiwa Mbunge basi niende na zile hati za usajili wa vijiji vile 23 kwa sababu imekuwa ni muda mrefu sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naona muda wangu nimeutawala vizuri, nimekuwa na maombi ya muda mrefu ya kuhusu ukarabati wa vituo vyetu vya afya nchi

nzima. Vituo vyetu vya afaya haviwezi kuongeza damu, haviwezi kutibu kwa vipimo, havina usafiri yaani gari la kusafirisha wagonjwa. Niende moja kwa moja katika mfano wa kituo changu cha afya cha Mwandoya ambacho ni kijiji pekee katika Jimbo la Kisesa. Kituo hiki cha afya ingawaje nimekuwa nikiahidiwa kwamba nitapelekewa waganga mapema iwezakanavyo na kwamba kiweze kuongeza damu, kiweze kutibu kwa vipimo. Lakini mpaka sasa ninavyozungumza hakuna mganga aliyepelekwa wala hakuna huduma hizo nilizozitaja hazifanyiki vituoni humo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo katika Jimbo langu hilo kwa kuwa sasa Jimbo lenyewe liko umbali wa zaidi ya kilometra 60, kutoka kituo cha afya pale kilipo mpaka kwenye hospitali ya Wilaya wananchi wanapata matatizo makubwa sana. Watoto wengi wakiishiwa damu wanakufa kwa kuishiwa damu, akina mama wengi wanapoteza maisha kwa sababu hakuna huduma ambayo ni nzuri ya afya. Nimekuwa nikishuhudia matukio makubwa kabisa ambayo ni ya kusikitisha, mtoto ameishiwa damu umtembeze kilometra zaidi ya 100 kumpeleka kwenye kituo cha afya gari hakuna, kituo cha afya nilichonacho hakiwezi kuongeza damu watoto wenge wamekufa. Mama mmoja akiwa anapatanisha nauli na taxi dereva hawa wa baiskeli mtoto wake alifariki wakiwa wanashindana bei. Kwa sababu fikilia mtoto anabebwa kwa baiskeli kutoka kilomita 60 mpaka afike kwenye hospitali ya Wilaya ameishiwa na damu utamfikishaje. (*Makofi*)

Mama wa watu, mtoto amepoteza maisha akiwa anapatana bei na mtu wa daladala na mimi mwenyewe ninapokuwa pale Jimboni gari langu ndilo linatumika kama *ambulance* la kuwahisha wagonjwa, siku mmoja nilitaka mpaka kupata ajali mtoto ninaye kwenye gari anazimia anashushwa chini anaanza kufanyiwa huduma, bahati nzuri katibu wangu wa ofisi yangu ni nesi kwa hiyo walikuwa wanampa matibabu. Lakini nilimbeba kwenye gari langu kumpeleka hospitali ya Wilaya na nilimwambia dereva aendeshe kwa kasi inayowezekana kuhakikisha mtoto huyo tunamfikisha hospitali ya Wilaya. Kwa hiyo, hata mimi mwenyewe yawezekana ningeweza kupoteza maisha kulingana na kasi ya gari ilivyokuwa ikikimba kwa sababu ya kuokoa maisha ya mtoto yule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niseme kwamba naishauri kabisa Serikali kwamba ilikuwa na mpango wa kutoa *ambulance* kwa mgao katika vituo vyetu vya afya ambavyo viko mbali na hospitali ya Wilaya, hili suala la mgao lisiwepo tena, Serikali ichukue uamuzi ilione tatizo hili ni la dharura itupelekee *ambulance* kwenye vituo vyetu vya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo kama nilivytangulia kwamba muda wangu nimeutawala na kwamba najiaandaa kuchangia kwenye Wizara zenyewe husika basi niseme kwamba naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

MHE. SAMUEL M. CHITALILO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nachukua nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia katika Bunge hili Bajeti, vile vile nachukua nafasi hii kukupongezeni wewe pamoja na Spika mwenyewe. Pongezi zangu zitaendelea mimi ninaendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa miezi sita hii ya kazi sasa ameonyesha Serikali yake kwamba inakoelekea ni kuzuri na kuna matarajio kwa wananchi. Vile vile nampongeza sana

Mheshimiwa Waziri Mkuu hasa pale ambapo huwa anaona kuna utata wa swali na yeze mwenyewe husimama na kwenda kujibu pale. Hiyo huwa inatufariji sana sisi wengine Wabunge. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru na nawapongeza sana Wabunge wote bila kujali itikadi ya vyama pale walipoamua kupitisha Bajeti kwa asilimia mia moja bila kujali mimi ni chama fulani wala mimi ni fulani bali walijali maslahi ya wananchi wote wa Tanzania. Kwa wastani kwa nchi yetu huu ni mfano hata nchi nyininge zitaiga mfano huu na mimi nawashukuru wenzangu kwa wale amba ni chama pinga kwamba sasa wameiva kisiasa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu wa Spika, mambo mengi sana yameshazungumzwa na waliotangulia kuzungumza katika Bajeti pamoja na hii hotuba ya Waziri Mkuu. Lakini nami nitakuwanayo machache ya kuzungumza. La kwanza ni kuishukuru Serikali pale ilipochukua uamuzi wa haraka sana wa kuona kwamba uhalifu katika nchi yetu ultaka kuzidi. Serikali ilichukua hatua ya tahadhali ya hali ya juu hadi sasa uhalifu tunausikia kwa jirani au kwa mbali zaidi. Kwa hiyo, naomba kasi hii iendelee. Lakini isisahaulike kwamba uhalifu huu bado upo kwa kiasi fulani. Katika Jimbo langu la Buchosa kila mara nimekuwa nikilalamika tangu Bunge lililopita, lakini kwa sasa nashukuru kwamba *at least* au hawa wahalifu wanaenda wanatulia tulia.

Kuna visiwa vya Zilagula, Mchangani, Iyozu pamekuwa na matatizo makubwa sana ya uhalifu wa kila siku wa kuuwawa wavuvi wakiwa katika shughuli zao za kila siku za uvuvi. Lakini kwa taarifa ya hapa karibuni baada ya Serikali kuweka tahadhari ya kutosha uharifu huu umepungua. Kwa hiyo, naiomba Serikali iendelee kutia mkazo kwa hali na mali ili tena hali isije ikabadilika, na ninaamini kwamba hali haitabadilika tena kwa sababu uzi ni ule ule na Rais ni yule yule na Waziri Mkuu ni yule yule, najua mmeanza kwa kasi na kasi hiyo haita legeza kamba kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile katika Jimbo langu la Buchosa kulikuwa na matatizo mengi sana ya barabara, kwa miaka mingi lakini naendelea kuishukuru Serikali kwamba hata hivi ninavyozungu sasa barabara zangu ambazo ziliwa sugu ambazo ziliwa hazijatibika kwa muda mrefu kwamba ziliwa zinapitika kwa shida, lakini mpaka hivi ninavyozungumza wakandarasi wako mabarabarani. Sasa mimi nilazima niendelee kuishukuru Serikali. Kuanzia barabara ya Ruchili - Bukokwa zinaendelea kutengenezwa Bukokwa - Nyehunge, Nyehunge - Kaunda, Nyehunge - Nyamadoke, Bukokwa - Nyakalilo, Nyakalilo - Rushamba, barabara hizi pamoja na kwamba sehemu nyininge wakandarasi hawajafika lakini pesa ipo kwa jaili ya matengenezo. Kwa hiyo mimi hapa naishukuru tu Serikali kwamba iendelee kunitengenezea barabara kwa manufaa ya wanabuchosa na manufaa ya wananchi wote wa Buchosa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaposema amani hapa nchini, kwamba ipo na tuidumishe ni lazima tuwe *serious* na kauli yetu. Amani hii kuna jambo moja lililojitokeza nililojifunza kwenye uchaguzi uliopita kwamba tunasema tunaendelea na kuwa na amani au tunayo lakini kuna jambo watu wengi nafikiri hawalione hili. Kwamba wakati wa uchaguzi uliopita, kuna *group* tu la vijana amba walikuwa wanaweza kupewa

hata shilingi 500/= na kuweza kuzomea wagombea mbalimbali. Hili si jambo la mchezo huu ndiyo mwanzo wa kuharibu amani ya nchi hii. Mimi ninaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu jambo hili muangalie kwa makini kwamba amani huwa inaanza kutoweka hivyo huku tunacheka.

Kwa hiyo, hili jambo ni lazima lifanyiwe uchunguzi wa hali ya juu. Hapo miaka mingine yote iliyopita huko nyuma hakukuwa na mchezo wa namna hii mimi nasema kwamba pamoja na kwamba propaganda za kisiasa wakati wa uchaguzi huwa zinakuwepo lakini tabia hii si tabia ya mtanzania, ni tabia ilioletwa na *group* fulani lazima iangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, asubuhi nilipokuwa nauliza swali hapa kuhusu vituo vya afya au kujengewa hospitali ambayo inaweza ikakidhi watu zaidi ya laki mbili katika Jimbo langu la Buchosa. Nilikuwa nina maana, lakini nimejibowi kwamba tuna hospitali ya Serikali.

Mimi nasema Wilaya nzima ya Sengerema ambako ndipo alipo Mheshimiwa William Ngeleja na mimi kule Buchosa hakuna hospitali ya Serikali, ile hospitali ni ya *mission*. Kwa hiyo, naomba jambo hili mllichukue ni Serikali mpya, lakini naomba kwamba jambo hili sasa mjue kabisa kwamba Buchosa wala Sengerema hakuna hospitali ya Serikali ni vituo vituo tu vya afya hata Sengerema Mjini ni kituo cha afya. Kwa hiyo, naomba jambo hili lichukuliwe, kama ni taarifa zilitoka kule Wilayani zinakuja kusema kwamba hiyo ni hospitali ya Serikali ni uongo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kuhusu elimu, kila Mtanzania sasa anataka kupata elimu iliyo bora na Rais hatimaye akasema kwamba Dodoma pajengwe Chuo Kikuu ambacho kitabeba zaidi ya watu 40,000. Mimi nashukuru ni wazo zuri sana na tumelipokea karibu wote lakini tatizo ni la walimu. Tutafute dawa kwanza ya kutibu tatizo la shule za msingi pamoja na Sekondari. Ni tatizo kubwa, tunapozunguka kwa wanachi wetu kila unapopita kwenye kijiji wanakwambia hapa tunatatizo la walimu. Unakopita kwenye sekondari iwe sekondari iwe shule ya msingi wanakwambia tunatatizo la walimu. Hili ni tatizo kubwa sana ambalo si la Buchosa peke yake wala Sengerema peke yake ni tatizo la nchi nzima. Naomba kabisa tujielekeze kwamba tufanyeje tupate walimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu spika, hivi karibuni kuna nchi nyingine ziliomba kupata walimu kutoka Tanzania mimi nafikiri hili lingesitishwa ili wafundishe hapahapa nchini kwa sababu hatuna walimu wa kutosha. Pamoja na kwamba ni hiari mtu akitaka kwenda sehemu nyingine lakini wangeshauriwa wafundishe kwanza watanzania wenzao. Hata kama wataende wasiende kwa idadi kama ilivyokuwa wanataka kwenda wote, waende baadhi. Pamoja na elimu hii ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu pale tu alipoamua kurudisha masomo yaliyokuwa yameporwa kinyemela. Namshukuru sana na wananchi wengi sana wanamshukuru kwa hili. Kwa sababu masomo waliyokuwa wameyazoea wananchi wetu watoto wetu au wadogo zetu walikuwa wamepoteza kabisa imani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali hii kweli ina miezi sita na tumeona hata hotuba ya Waziri Mkuu hapa inaonyesha kila kitu, hotuba ya Waziri wa Fedha ilionyesha kila kitu sasa kusema kwamba utazungumza mambo yote yamejipanga hapa na Waziri Mkuu hapo alipo ukitaka hapo sasa hivi kwamba unashida yoyote unataka kumuona ukimwomba mara mmoja mnakwenda pale mnaongea yanaisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nafikiri sina haja ya kuzungumza mengi lakini hapa namwomba tu kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu ajaribu kuangalia jambo la watendaji ambao badala ya kufanya shughuli zao wao wanakwenda kujihusisha na siasa. Kama ni uchaguzi ulishaisha hapa tunatakiwa kufanya kazi tu, kuna baadhi ya watendaji wa Serikali wanaacha kufanya majukumu yao kila siku ni kwenye vijiwe vyta kisiasa haya ndiyo ujaribu kuyaangalia. Lakini vinginevyo mimi ninaunga hoja hii mkono asilimia mia moja kabisa ikiwezekana na nyongeza naweka huko juu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa naibu spika, kwa hiyo, mimi naomba nisiisumbue Serikali hii kwa sababu mambo mengi ni mazuri yanayotendeka. (*Makofi*)

MHE. WILSON M. MASILINGI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi niweze na mimi kushiriki katika mjadala huu wa hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Kwanza kabisa napenda kusema kwamba naunga mkono hoja ya Waziri Mkuu na pili napenda kuungana na Mheshimiwa Waziri Mkuu katika kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa kuaminiwa na chama chetu ili awe Mwenyekiti wetu mpya na pili naunga na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kumpongeza Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kwa kazi nzuri aliyoifanya kulitumikia Taifa letu.

Aidha, nimalizie kwa sababu muda ni mfupi kwa kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wenzetu ambao wameaminiwa na chama chetu baada ya Mheshimiwa Mwenyekiti wetu kuonyesha imani ya kwanza kabisa kuongoza Idara Kuu, Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Yusuf Mkamba na Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Katibu Mwenezi, Mheshimiwa Asha-Rose Migiro, Mambo ya Nje, Mheshimiwa Rostam Azizi Hazina na Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe, Mipango, kuna niliye msahau? Wamekwisha. Hongera sana na nitawapa ushirikiano wote kama mwana-CCM. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi katika kuunga mkono hoja hii sina mambo mengi sana, lakini la kwanza ambalo napenda kuchangia katika hotuba ya Waziri Mkuu ni lile la afya ukurasa wa 58.

Mheshimiwa Waziri Mkuu amerifahamisha Bunge hili mikakati ya Serikali yetu ya kuendelea kuboresha sekta ya afya ukurasa wa 58. Mimi naipongeza sana Serikali na naungana na wachangiaji walionitangulia kwa kutambua ugumu wa Serikali ya awamu ya nne kwa vile ndiyo inaanza katika kutekeleza majukumu au changamoto zilizoko mbele ya Serikali yetu na sisi wote kutokana na ufinyu wa Bajeti. Lakini zaidi muda wa kujiweka sawasawa baada ya kuwa wameanza vizuri sasa kwa mwendo wa bomba, ari

mpya, kasi mpya na nguvu mpya, bomba. Ni muda mfupi sana kwa kweli kusema kwamba tunauwezo ndani ya Bunge hili kuwapatia fedha za kutosha kufanya mambo mazito.

Lakini mimi ninalopongeza hapa sio uwezo wa kifedha bali uwezo wa utashi wa Serikali dhamira thabiti ya kujali mambo ya msingi ya vipaumbele kwa wananchi wetu bila ya kupingana na ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, wewe mwenyewe dhamana ya kusimamia shuguli za Serikali hapa Bungeni.

Sasa katika afya Mheshimiwa Waziri Mkuu ametambua uwezo mdogo wa Halmashauri za Wilaya kwamba watazijengea uwezo Halmashauri za Wilaya. Kazi hii ilianza zamani lakini haijakamilika kwa hiyo sina budi kuipongeza Serikali itazijengea uwezo Halmashauri za Wilaya katika miradi ya ukarabati wa vituo vya kutolea huduma za afya. Kwa kuboresha majengo kutoa vifaa vya kitaalam samani kwenye hospitali za Wilaya na hili wanalenga sio hospitali za Wilaya tu, vituo vya afya na zahanati. (*Makofi*)

Nikupongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, mimi kwa niaba ya wananchi wa Muleba Kusini nimefurahishwa na hili na hili nalisema kwa sababu sisi Muleba Kusini au niseme Wilaya nzima kwa sababu ni Mbunge wa Muleba Kusini. Lakini Wilaya yetu ina Majimbo mawili na tuna Halmashauri ya Wilaya moja. Hatuna hospitali ya Wilaya, lakini Mheshimiwa Rais na Serikali yake wameahidi kutujengea hospitali ya Wilaya, kwa niaba ya wananchi wa Muleba Kusini na Wilaya nzima ya Muleba ahsante sana Mheshimiwa Rais, ahsante sana Serikali nzima ya awamu ya nne, tutafutilia na tutatoa ushirikiano unaohitajika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la kusikitisha zaidi sasa hivi, tumezidiwa tunajua uwezo wa Serikali ni mdogo, Bajeti ni finyu, mipango imekamilika tumepeata janga, janga hatukultarajia la kusikitisha sana watoto wanakufa kwa kasi ya kusikitisha.

Lakini kwa vile nimeshatoa taarifa Serikalini na Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii ataongeza nguvu niseme tu kwamba naiomba Serikali kwa niaba ya wananchi wa Muleba Kusini kufuatia mlipuko wa ugonjwa wa malaria kwa sababu sio mara ya kwanza. Mwaka 1998 tulidhani ni ugonjwa wa ajabu, sasa hivi tunadhani kwasababu inatoka kila mwaka lakini huwa tuna udhibiti kwa kusaidiwa na Serikali, kwa sababu Serikali ina mkataba na hospitali ya Rubya, hospitali ya Kanisa Katoliki, madaktari wanafanyakazi nzuri na wauguzi wanajitahidi na mashirika ya nje walitusaidia mwaka 1998.

Safari hii hawapo hawa wageni kutoka nje lakini Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii amesema ataongeza nguvu, nakuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa sababu *speed* yako naipenda sana. Tuma Tume na Mkuu wangu wa Mkoa yupo hapa, mmetuletea Mkuu wa Mkoa *number one* na tunabahati ya kupata, kwa sababu sisi tuko mpakani tunabahati ya kupata Majemedari, sio Majemedari kwa sababu mimi ni askari wa akiba nimetumia neno baya nafuta hilo. Wapiganaji kwa sababu mimi ni mpiganaji hawa ni makamanda, makanali. Lakini tulikuwa na Jenerali Kiwelu ambaye amefanya

kazi nzuri sio tu ya kupigana vita ya Kagera bali ameongoza Mkoa wetu mpaka akastaafu Kagera, anastahili pongezi Mheshimiwa Jenerali Kiwelu. (*Makofi*)

Sasa tumeletewa Kanali Mfuru, anaweza akapata, hawaruhusiwi kuingia kwenye siasa anafaa hata na yeje kuwa Meja Jenarili au Jenerali. Lakini ninachotaka kusema ni shahidi yupo watoto wanakufa lakufanya ambacho nashauri Mheshimiwa Waziri Mkoo tuma ujumbe watathimini kama mnavyofanya inapotokea ajari ya watu kugongana kwenye magari. Sasa watoto wakifa kwa *speed* inayoendelea hospitali ya Rubya Serikali fikeni muwape pole hamuwezi kushika roho za watoto tunajua na wananchi wa Muleba Kusini wanajua, fikeni muangalie tunaweza tukafanyaje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu spika, mwaka 1998 niliomba msaada wa mashirika ya nje yakasaidiana na Serikali kuweka mahema kwenye Kata na kwenye hospitali kuokoa watoto. Watoto wanafia kwenye mikono ya akina mama hili ninalolisema si kuwatisha ni ukweli. Kunasikitisha tulijaribu kuvumilia tukadhani tutadhibiti tumezidiwa naomba mtusaidie kwa sababu hatuna hospitali ya Wilaya na hiyo Tarafa ambako kuna hospitali ya Rubya ya Nshamba, wananchi kwa sensa ya hivi karibuni wako 117,000 hatuna kituo cha afya na mimi nilikua Waziri. Sasa watu wanaweza kuuliza wewe ulikua Waziri umeshindwaje kupeleka kituo cha afya, kazi ya uwaziri sio kupeleka mahospitali ni kujenga taifa sio kujenga Jimbo kwa hiyo Mawaziri najua ndivyo wanavyofanya na wananchi wanadirudisha kwa kujuu hili.

Mimi nikisema tuunganishe nguvu wananchi wameanza kujenga, karibu kinakwisha. Lakini tumezidiwa tena namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkoo amesema ataweka nguvu na ameshaagiza Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa watenge fedha kwenye huu ukarabati kituo kiishe cha Nshamba watu wapate huduma. Hawa wasingefia kwenye hospitali za Kanisa Katoliki. (*Makofi*)

Kwa hiyo, mimi naomba tathmini iende, ifanyike hata ninayoyasema haya yahakikiwe, mapesa yaliyotengwa kwa Bajeti ya Halmashauri ya Wilaya Muleba kwa vipaumbele tu kama watoto wanakufa zinatosha sana kuepusha vifo vyta watoto. Isipokuwa tunavyopanga Bajeti zetu ni mfumo wa zamani wa mimi na wenzangu. Sasa awamu ya nne mtabadilisha polepole ili hata ikibidi Sheria inayotufunga kwenda hivi ije Bungeni turekebishe. Kwa sababu wajibu wa Bunge ni sisi kuwawezesha Serikali msikwame lakini sisi tusifungwe na ukiritimba, pesa zipo haziwezi kuokoa maisha hii haikubaliki katika mantiki ya kawaida, najua si tatizo la Serikali la Bunge na jamii nzima tubadilishe mfumo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna sababu gani ya kusema kuna fedha za ukarabati wa vituo vyta afya na zenyewe hazitosh, lakini zingine tunapeleka mfuko wa barabara na nyingine sijui wapi tunazisambaza sambaza huku watoto wanakufa. Nasema si tatizo la Serikali ni letu wote hapa nimeona nizungumze hili kwa sababu linaniuma na najua linawauma na ninyi linawauma Wabunge hasa Wabunge wa Bunge hili ambalo wanansikiliza wanajua ni muhimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nimalizie kwa kusema yafuatayo, kwa kuwa Halmashauri zetu za Wilaya, Mheshimiwa Waziri Mkoo ametambua kwamba zina uwezo

mdogo wa kifedha na kiutendaji. Mimi nashauri Serikali mtafakari upya wazo la kuanda mikataba na Halmashauri hizi. Mikataba ya Serikali na Halmashauri za Wilaya. Mimi nivyolisikia kwenye hotuba mimi muda haukunitosha kufanya utafiti, ndiyo maana naomba Serikali ilitafakari, mnafanya mkataba na nani na Mkurugenzi wa Halmashauri, mnafanya mkataba na Madiwani, mnafanya mkataba na wananchi au mnafanya mkataba na nani? Tumesharingia mkataba na wananchi kwa njia ya Ilani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu amenifurahisha na Serikali imenifurahisha. Anasema, pamoja na kuwepo mgawanyo huo wa majukumu, Serikali Kuu ndiyo inayowajibika kwa ujumla kwa wananchi katika kuhakikisha kuwa huduma zinawafikia wananchi na zina ubora wa kiwango kinachostahili, huo ndio msingi nambari *one*, huo ndio mkataba, msiingie mwingine, mnaingia na nani!

Kwanza, Wakurugenzi mnawaleta ninyi, Watendaji mnawaleta ninyi, wanatuvuruga. Mnasema, Halmashauri dhaifu, Halmashauri dhaifu, Halmashauri tangu lini akawa Mkurugenzi na watendaji! Halmashauri inaundwa na Serikali za Vijiji, tuwezeshe vijiji. Kwa mfumo wa *TASAF* wameonyesha wanavijiji wana uwezo wa kusimamia pesa kuliko Halmashauri. Tumefanikiwa *TASAF*, tumeingia awamu ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pesa wanazopeleka *TASAF*, 80% zinaingia kwenye huduma, 20% zinaingia *administration*. Unazopeleka kwenye Halmashauri, 20% ndiyo huduma, 80% *administration* na Wenyeviti wa Serikali za Vijiji na Serikali za Vijiji zilizoundwa Kikatiba hazina bajeti. Kwa nini watendaji wa Halmashauri wawe na hela, Serikali za Vijiji zisipate hela na zikifanya kazi *MMEM*, *TASAF* tunaona matunda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali mtafakari mambo ya mikataba hii, muingie mkataba na wananchi, siyo Halmashauri na ikifanikiwa sana, ingia mkataba na Serikali za Vijiji zina akaunti tayari kuititia mpango wa *MMEM* uliofanikiwa na *TASAF*. Serikali za Vijiji, Mheshimiwa Waziri Mkuu na ye ye anazifahamu na Wabunge wanazifahamu, Serikali za Vijiji zinajali tena bila posho wala mshahara, wana-deliver elimu, afya na maji kwenye miradi. Sasa tutakaa tunalia na Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofi*)

MHE. WILLIAM M. NGELEJA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia fursa kama hii ili nami niweze kuchangia katika hotuba hii kutoka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote natamka wazi kwamba mimi naunga mkono hoja hii iliyoko mbele yetu kwa asilimia zote. Lakini kabla sijaendelea na michango yangu ambayo ninayo hapa, naomba nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri waliko chini ya ofisi yake pamoja na watendaji kwa ujumla kwa hotuba hii nzuri ambayo mimi naiona kama ni elekezi katika kufanikisha na kutekeleza malengo ya Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kupongezana. Wiki iliyopita tulipitisha bajeti sisi sote kama Bunge kwa kauli moja. Wenzangu nawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajadili bajeti ya kipindi cha mwaka wa fedha 2006/2007. Misingi ya utekelezaji wake ni ya kuzingatia Ilani ya Uchaguzi. Kwa sababu tunazingatia Ilani ya Uchaguzi, Ilani ya Chama cha Mapinduzi, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa jana kuwa Mwenyekiti wa Chama chetu cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia niwapongeze sana wajumbe wa Mkutano Mkuu walioshiriki jana kumchagua Mheshimiwa Rais ambaye sasa hivi ni Mwenyekiti wa Chama chetu na pia niwapongeze sana wanachama wa Chama cha Mapinduzi wote ambao jana wamechaguliwa kushika nyazifa za juu katika Chama chetu, nawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nijikite moja kwa moja kwenye mchango. La kwanza, mimi naangukia kwenye sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wiki iliyopita tuliletewa hapa hotuba ya Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji. Ukiisoma ukaioanisha na hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu leo, unaona hotuba zote zinakubaliana kwa jambo moja, kwamba uchumi wetu sisi Watanzania bado ni tegemezi kutoka kwenye sekta ya kilimo. Ni ukweli ambao hauwezi kupingika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ndilo lililonivuta nianzae kuchangia katika sekta hii. Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu imeelezea mambo mengi mazuri sana. Inafikia mahali unaona tu kwamba kweli tukienda kwa *spirit* hii, hakuna sababu ya kuiona Tanzania kufikia mwaka 2010 ina kuwa tofauti kwa kiwango kikubwa sana jinsi ilivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa mikakati na nia ya dhati ambayo imejionyesha katika hotuba hizi ambazo tumekuwa tukiziona wakati huu wa mjadala wa bajeti yetu ya mwaka unaofuatia wa fedha. Kuna mambo mengi ya msingi sana yamesemwa na yanatia faraja na kwa kiasi kikubwa yanajibu hoja ama haja na matarajio ya wanachi. Lakini pamoja na uzuri huo ninaomba niongezee machache, pengine ikiwezekana kuboresha katika ufanikishaji wa malengo ambayo tuliojiwekea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, nashauri wakati mipango mizuri sana imeelezwa hapa ya utekelezaji na kuboresha sekta ya kilimo, naomba, niiombe Serikali tuiwekee malengo kwa kila ngazi ya utawala ambao tumejiwekea katika mfumo wa uendeshaji wa Serikali ya Tanzania. Tuwekeane malengo ya uzalishaji, iwe mazao ya biashara ama chakula. Na hili tulifanye kwa maelekezo rasmi kutoka kwenye ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Tuanzie ngazi ya Mkoa, Taifa tunafahamu. Twende ngazi ya mkoa, kila mkoa upewe lengo la uzalishaji. Tushuke chini ngazi ya Wilaya, tushuke chini ngazi ya Kata na kwa sababu kilimo hakifanyiki mitaani, bali kinafanyika mashambani

ambako viongozi wa chini wa kule Watendaji ni viongozi wa vitongoji, Serikali za vitongoji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tuweke malengo yaliyobayana kwa kila kiongozi wa kitongoji na mji. Hawa ndio wanafahamu, hawa ndiyo tunaoshirikiana nao. Wanafahamu tulime kwa kiasi gani. Kwa hivyo, huo ulikuwa ni ushauri wa kwanza.

Mhesimiwa Naibu Spika, ushauri wa pili, tuweke msukumo mpya katika matumizi ya mbolea. Mimi ninakotokea katika Jimbo la Sengerema ni wafugaji. Tunafahamu mbolea aina ya samadi haijawahi kutumika ipasavyo hasa mikoa ya kwetu. Hili nalisema wazi. Lakini naamini pia hili limechangiwa pia pengine kutokuwa na msukumo uliodhahiri unaotaka kuonyesha mafanikio ya kiwango ambacho tunakitaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba hili nalo tulichukulie katika ile mikakati ambayo kimsingi tuifanye kama ya dharura kuhakikisha kwamba kwa sababu tunasema tutawashirikisha viongozi wa vitongoji, basi kila mwananchi hasa kila Kaya kule sisi tunatoka kwenye sehemu za wakulima. Tuhakikishe kwamba mbolea inayopatikana kule aina ya samadi itumike ipasavyo na tuweke utaratibu wa kuratibu kuona kwamba mambo haya yamefanyika. Nadhani tukiamua kudhamiria tunaweza kufanya. Mambo haya yalishafanyika nchi zingine, tunasoma historia ya mapinduzi halisi ya kilimo kule China. Lakini pia tumeona mambo mengine watu wakiamua. Tunafahamu Mtawala hapa Uganda majirani zetu, Kabaka alishawahi kuchimba bwawa kubwa, likajazwa kwa nguvu za watu. Sasa mimi naamini kwamba sisi tukiamua kufanya haya mambo kwa dhati kabisa, tunaweza kufanikisha kwa kiwango kikubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala la chakula. Pengine kwa sisi ambao hatujakua siku nyingi sana, dhoruba tulioipata mwaka jana na mpaka mwaka huu ilikuwa inatishia hata fikra zetu. Lakini nafahamu wale ambao mmekuwepo siku nyingi, mmeona mabalaa makubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kusema ni kwamba katika suala la chakula hili tulione kwamba ni suala la dharura wakati wote. Naomba niishauri Serikali kwamba hili nalo tuliwekee mikakati kama nilivyokwisha kusema awali kwamba kila mkoa upewe lengo la kuhakikisha kwamba unajitosheleza kwa chakula.

Mimi siamini kama nchi hii kila mkoa unaweza kushindwa kupata Wilaya mbili, tatu za kuweza kama tukizingatia kwa dhati utaalamu wa kilimo cha kisasa, washauri na sisi wenyewe viongozi mbali mbali kwa ngazi ya Kata, Wilaya, Mkoa, Wawakilishi, Madiwani, Wabunge tukasimamia kwa dhati, siamini kama kuna mkoa ambao unaweza kushindwa kulishwa na baadhi ya Wilaya zinazopatikana ndani ya mkoa huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimesoma Mpwapwa Sekondari, Wilaya ya Mpwapwa inatosha kulisha Mkoa wa Dodoma tukiamua kufanya kwa dhati. Mkoa wa Singida, naamini Mheshimiwa Juma Killimbah ananisikia hapa, Iramba inaweza kulisha Mkoa wa Singida. Tulime mtama, mazao ambayo yanawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba niishauri Serikali kwamba tuonyeshe nia ya dhati na tufanye haya mambo tukidhamiria, tukiogopa njaa, maisha ni mafupi sana. Tusifanye kama vile tutaishi hapa miaka mingi sana, milele, hapana, tufanye mambo ya dharura haya. Tulikumbushwa juzi na Rais wa *Ireland* kwamba ili maendeleo yafanyike kunahitaji uvumilivu na kutokuwa mvumilivu pia. Kwa hiyo, naomba pia hili jambo tulizingatie.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka niseme niishauri Serikali, tuna Idara ya Utabiri wa Hali ya Hewa, tunaiomba sana, mimi naamini kwamba haijatumika ipasavyo.

Mimi niko Kamati ya Miuondombinu, juzi tulipokuwa pale tunazungukia tulipokuwa Dar es Salaam, tumeambiwa wana vifaa ambavyo wanaweza ku-*predict* hali ya hewa miezi mitatu mbele ama kabla. Sasa, nadhani ya kwamba tukiitumia hii vizuri itakuwa ni mwongozo mzuri sana kwanza kuwawezesha wananchi wetu walime kwa muda gani kwa sababu wakati fulani tunapoteza nguvu kwa sababu hatupati mwongozo sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Idara ya Hali ya Hewa tuitumie ipasavyo na *promotion* ya taarifa zake tuhusishwe sisi wawakilishi wa wananchi, Wabunge, Madiwani, Viongozi kama Wakuu wa Wilaya, Halmashauri na hizi taarifa tuzifanye kama kitu ambacho ni *promotion* ya biashara. Tufanye haya mambo kwa dhati, tuwaelekeze wananchi wetu na sisi wanasiasa twende kule tupite tunawakumbusha wananchi twende kuwashauri. Naamini tukiamua kufanya haya mambo yatafanikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine ambalo ninataka niseme katika kuishauri Serikali katika suala hili ni wataalamu wa kilimo. Mimi ninadhani kwamba katika suala hili tunasema moja wapo ya mikakati tuhakikishe kwamba kilimo cha umwagiliaji kinafanikiwa. Lakini mpaka sasa hivi nafahamu baadhi ya maeneo katika nchi yetu yameishawahi kutambuliwa yamekuwa *identified* kama ni *potential* kwa kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwamba maeneo ambayo yameshatambuliwa yapewe kipaumbele kwanza *immediately* kiuzalishaji kwa umwagiliaji. Serikali ilione hili kwa sababu kuna maeneo ambayo tayari yameishatengwa kwa mfano Jimbo la Sengerema kuna sehemu inaitwa Katungulu kule, kwa Mheshimiwa Samuel Chitalilo, kuna sehemu inaitwa Nzelu ukifika kule utapata kuona mambo mengi. Kwa hiyo, nadhani ya kwamba tuangalie maeneo ambayo yameshatayarishwa tayari, basi tutekeleze kilimo cha kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ninalotaka kushauri ni masuala ya mazao ya biashara. Hapa niongelee, nimesema misingi ya ukulima wa kisasa tuizingatie, lakini kuna suala la kuja bei za uzalishaji. Gharama za uzalishaji, ninaomba Serikali itusaidie sana. Mimi siamini kama leo tukiwaachia wananchi watawaliwe na soko huria,

tunaweza kufika. Sasa hivi tumekuwa tukihamasisha kwamba wananchi wajunge katika vikundi na vinginevyo vitakuwa vyta uzalishaji mazao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji kuwasaidia wananchi. Tuelewe kwanza gharama za uzalishaji na kwa kutambua bei *bottom line*, nadhani haitakuwa kuingilia soko huru, hapana. Tukishajua gharama za uzalishaji, basi wafanyabiashara ambao watakuwa wanajiingiza katika ununuzi wa mazao kama pamba, basi bei yake ijulikane na wasiende chini ya hapo. Hii tutakuwa tumewasaidia sana wananchi kufikia lile lengo letu la maisha bora kwa kila mmoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee suala la mifugo. Mimi natoka kwenye familia ya mfugaji. Wengi tumekuwa tukisema hapa, ni wazi kwamba kweli hii sekta ndogo ya mifugo haijapewa msukumo unaostahili. Naomba Serikali ilione hili kama sekta zingine. Tuwalinde wafugaji wetu na tuwahamasishe, tuwasaidie, tu-*invest* katika hili, tuwekeze kama kuna gharama za kuendesha warsha kwa ajili ya wafugaji, zifanywe, pesa zitengwe, waelewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini, jambo lingine tuwasaidie wafugaji kwa kuwajengea soko ambalo linaaminika na moja wapo ni kuwa na ... Sasa hivi tuna wawekezaji mbali mbali tumekuwa tukilalamika, basi tujaribu kulinda mazao ya wanyama ambayo yanatokana na mifugo yetu hapa nchini. Tuweke kodi ama ushuru kwa nyama inayotoka nje ya nchi. Hili kwa namna moja tutakuwa tunawasaidia sana wafugaji wetu na tutawaboreshea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee suala la Uvuvi. Ukitoka Mkoa wa Mwanza usipoongelea uvuvi, hujaelewaka. Sehemu kubwa kule kwetu ni wavuvi. Tunaisifu Serikali kwa juhudhi ambazo imechukua kuimarisha ulinzi wa raia na usalama wa mali zao. Mimi kule Ziwani kuna heka heka sana hasa uvuvi wakati wa usiku. Majambazi wanakuja kule wanapora boti za uvuvi. Naomba sana suala hili la ulinzi katika Ziwa liimarishwe. Ninaamini hata sehemu zingine za Bahari ambako shughuli za uvuvi zinafanyika. Kwa hiyo ninaomba jambo hili lizingatiwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Askari wetu Solomon. Tukio la tarehe 20 Aprili, 2006 lililotokea pale Ubungo lilikuwa linatisha. Lakini nina ombi kwa Serikali. Tumekuwa na utaratibu, tumejiwekea utamaduni wa kuenzi mashujaa wa nchi hii. Nina amini kitendo alichokifanya askari wetu Solomon siku ile kinastahili kuenziwa ikiwezekana tuangalie namna ya kumleta hapa Bungeni *to recognise his effort* aliyofanya na uzalendo alionyesha kwa nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kabla ya moja ni suala la Idara ya Ushirika. Sasa hivi tumekuwa tukisema tunahamasisha *SACCOS* zianzishwe, hizi zinatawaliwa na sheria ya Ushirika. Lakini pia *SACCOS* hizi tuna vijiji zaidi ya 10,000 na mijini ndiyo kuna vikundi vingi vya shughuli nyingi za vyama tunavyovihamasisha. Lakini bado tuna Vyama vya Ushirika ambavyo vimekuwepo. Naipongeza sana Serikali katika hili kwa juhudhi ambazo imekuwa ikichukua kusaidia kukiokoa Chama cha Ushirika Mkoani Mwanza, Nyanza. Natoa shukrani. Lakini naomba Idara ya Ushirika iimarishe,

iimarishwe kwanza kwa kupewa nyenzo za kisasa kwa sababu naamini mahitaji ni makubwa kuliko ilivyokuwa awali. Lakini pia ikiwezekana tuone kama kuna uwezekano Serikali iajiri watumishi wanaohusiana na masuala ya kilimo na ushirika moja kwa moja kutoka vyuoni ili kuweza ku-cover, ku-meet hii *demand* ambayo inakuja sasa hivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, ni Utawala Bora. Mheshimiwa Waziri Mkuu amekuwa aktuonyesha njia nzuri sana, tunampongeza kwa wepesi wake wa kutatua kero. Lakini, kuna mambo, kuna Idara ama baadhi ya watendaji katika Serikali hawajaenda na hii *speed*. Sisi kwa mfano kule Sengerema tuna tatizo la maji. Tumeomba mashine moja inaitwa *Floating Pump* kwa sababu kiwango cha maji kimeshuka kule, sasa hivi ni miezi zaidi ya mine hatujajibiwa. Jambo hili liko pale Hazina. Maji tunapata kwa mgao lakini sisi tuko Ziwani pale. Tumeomba shilingi milioni 49.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine, ni suala la watendaji wa vijiji. Kule Halmshauri ya Wilaya ya Sengerema tuna watendaji 70 ambaeo leo ni zaidi ya mwaka hawajalipwa mishahara yao. Mbunge wa Jimbo la Sengerema anafuatilia, Halmashauri inafuatilia, Mtendaji wa Wilaya anafuatilia lakini hatujawahi kupata jawabu. Naomba hili Serikali ilione. Tuna kero, tunawakatisha tama watendaji wetu. Naomba Serikali ilione hili na kwa kweli tungependa kupata ufanuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kuongezea majukumu Halmashauri. Nimepata taarifa kwamba kuna majukumu yameelekezwa. Tunaambiwa Halmashauri zetu ziwalipie watendaji kadhaa, kulipa posho kwa Wenyeviti wa Vijihi vilivyoko ndani ya Halmashauri, kulipa posho kwa Wenyeviti wa Vitongoji, kulipa posho kwa Makatibu wa Mabaraza ya Ardhi pamoja na kulipa posho kwa Makatibu wa Mabaraza ya Kata na vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwangu kwa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema tunadaiwa shilingi milioni 400. Naomba Serikali ilione hili. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. JOB Y. NDUGAI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii jioni ya leo na mimi niweze kuchangia katika hotuba nzuri ambayo imeletwa mbele yetu na Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niwashukuru wananchi wa Kongwa kwa kunichagua na kuniwezesha kuja kwa mara ya pili na kuwawakilisha hapa na kwa niaba yao natoa pongezi nyingi sana kwa Serikali ya Awamu ya Nne na hasa kwa Mheshimiwa Rais kwa jinsi ambavyo amekuwa akifanya kazi nzuri inayoturidhisha sisi sote akisaidiwa vizuri sana na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa karibu sana na hasa kwenye suala la njaa ambalo lilitukumba sisi watu wa mkoa wa Dodoma na hasa sisi watu wa Kongwa. Tulipata ushirikiano mkubwa sana kutoka ofisi ya Waziri Mkuu. Tunatoa shukrani zetu za dhati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikumbushe tu kwamba tatizo hilo la njaa halijaisha. Bado tuna upungufu mkubwa wa chakula kule Kongwa na sababu yake kubwa ni mvua ilichelewa sana kuja halafu ikaondoka kwa wakati wake. Kwa hiyo, mazao yakaachwa katika *stage* ambayo kwa sehemu nyingi hatukuvuna chochote. Kwa hiyo, tunaomba Serikali ijue kwamba kwa mwaka huu kuanzia mwezi huu mpaka kwenye mwezi wa nne, wa tano mwakani tena kuna ngwe ya kuweza kutusaidia saidia wakati tunajiandaa kwa msimu unaokuja. Tunashukuru sana kwa msaada ambao tulipata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maandalizi yaliyopo hivi sasa, *World Food Programme* wameisha ahidi kutoa msaada wa chakula kwa Wilaya ya Mpwapwa, kwa Wilaya ya Dodoma Vijijini na kwa Wilaya ya Kondo. Kwa hiyo, katika msaada wa WFP, Kongwa tumeachwa pembeni, hatupo katika mradi huo. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali itutazame kwa macho mawili kwa sababu kwa kweli hali ni ngumu. Tusipoangalia vizuri yanaweza kutokea ambayo hatuyatarajii. Katika eneo hilo tuna maombi matatu:-

La kwanza, tunaomba chakula cha msaada kwa familia zitakazo kuwa na hali mbaya sana. La pili, tunaomba mbegu za Mtama mapema na ombi la tatu, ni kwamba kuwasisitiza wananchi wa Kanda ya Kati haya maeneo makame kama Dodoma, Singida na kadhalika kulima mtama. Lakini mtama huo kama hauna soko, itakuwa ni kazi bure tu. Watu walime kitu ambacho kinauzika. Kwa sababu wakulima wetu Tanzania wanalima vitu ambavyo kwa kiwango kikubwa wanavitumia wao wenye kama chakula, halafu sehemu nyingine inakuwa ni sehemu ya biashara. Ukiwalazimisha watu hawa walime tu kitu kwa sababu ya chakula peke yake, hakina soko popote, uitikio wake hautakuwa mkubwa. Kwa hiyo, ningeshauri *SGR* wanunue na vile vile kwa sababu tunasikia kuna baadhi ya nchi huwa zinahitaji mtama wa aina mbali mbali, ufanyike utafiti kwa haraka ili tuimarishe kilimo cha mtama tukijua soko lipo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa shukrani sana kwa niaba ya watu wa Kongwa kwa mambo mawili mengine ukiacha lile la chakula. Moja, la Chuo Kikuu kujengwa Dodoma. Haliwezi kupita bila kusema chochote. Tunashukuru sana. Lakini pili, ahadi ya Serikali ambayo imerudiwa mara kwa mara kwamba barabara ya kutoka Minjingu - Dodoma - Iringa, itafanyiwa kazi ya uhakika ndani ya mika mitano hii itakuwa imewekewa lami. Kwa hilo tunashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoke huko. Leo asubuhi palikuwa na maswali kama kawaida yetu. Swalil la kwanza lilikuwa la Mheshimiwa Mohammed Rished Abdallah, lilikuwa linahusu Sheria yetu ya Bungeni ya *Parliamentary Service Commission* ambayo inatoa madaraka ile Sheria kwa Bunge kuwa na bajeti yake na kuisimamia. Mimi niko kwenye kuisimamia bajeti yake. (*Makofi*)

Maoni yangu ni kwamba majibu yale yaliyotoka, hatukukubaliana nayo sana tulio wengi na ndiyo maana Mheshimiwa Mbunge aliuliza na mimi sidhani kama kuna kutoelewana kokote au mgongano wowote kati ya Serikali yetu na Bunge hili. Umeishafika wakati ambao lazima kabisa na ni vema Bunge hili likasimamia bajeti yake. Tusiseme tu Wabunge wakasimamie Halmashauri, wakafanye hivi... Tukitaka Bunge

likae sawa sawa ili nalo lifanye mambo yake, hapana. Tukubaliane kimsingi na jambo hili ni jema kwa Bunge hili Jipyä jinsi lilivyo na mambo yake mapya na *speed* na ili *standard* ziende sawa sawa nina hakika Serikali kwa hili wala halina maneno. Bunge liwezeshehwe lisimamie bajeti yake. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, makofi hayo ni salaam kwamba jambo hili Waheshimiwa wanalikubali kabisa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la Mradi wa *MMES*. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Suala la usimamizi wa Sekondari, tumepega hatua kweli kweli. Sisi Kongwa muda wote tulikuwa na Sekondari tatu tu. Lakini sasa hivi tunaongelea habari ya sekondari 12 na mwaka huu tumeweza kuchukua watoto wote waliofaulu Darasa la Saba kwenda Sekondari asilimia 100, tumepeleka Sekondari kwa kujitahidi kwa ushirikiano wa wananchi na msukumo wa Serikali tuliopata kupitia Halmashauri zetu. Lakini tunao Mradi wa *MMES* uko wapi? Juhudi zote tulizokuwa tunafanya za kukimbia na kujenga Sekondari, *MMES* imesaidia nini? Kidogo sana. Ni mradi ambao ni kama upo, haupo. Tunauliza kulikoni! Tungependa maelezo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niliwhi kusimama mara mbili, tatu niliongelea *MMES* na leo nasimama nikiongelea tena *MMES* ni *mess* kweli. Iko wapi? Hela zake zikija zina njia zake zinapita pita huko kwa Ma-*Headmaster*. Tumetekeleza *MMEM* kupitia Halmashauri madarasa hayakujengwa, kwa nini hela za *MMES* zisipite Halmashauri. Shule zinajengwa kwenye Kata anasimamia Diwani, anasimamia Mtendaji wa Kata ambao wako chini ya Halamashauri. Pesa zinapita kwa *Headmaster* aliyoko kilomita 30. Wala hana habari na ile Kata inayojenga Sekondari. Kwa nini iwe hivyo? Halmashauri ipo. Fedha za *MMES* zinazokuja zipite Halmashauri. Kama hawawajibiki Halmashauri washughulikiwe. *MMES* itakaa sawa sawa kwa utaratibu huo. Lakini huu utaratibu uliopo hivi sasa wa kimundo wa huo mradi hasa kiutekelezaji upande wa fedha, una mapungufu makubwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama walivyosema wenzangu suala la kugawa vitongoji, vijiji na kata na sisi tuna kilio kikubwa sana. Tarafa hazina maneno sana hata ukizigawa. Unajua Katibu Tarafa ana *impact* lakini *impact* yake siyo kubwa, ni Vitongoji, Vijiji na Kata. Kwa mfano, kule Kongwa nina Kata ya Pandambili *total population* yake karibu watu 30,000 Kata moja. Tuna Wilaya hapa zina watu 30,000. Sasa tunaposema kila Kata iwe na Sekondari maana yake ni kwamba sisi tutakuwa na Sekondari moja kwa eneo ambalo ni *almost size* ya Wilaya. Kwa hiyo, tunaposema kila Kata iwe na Sekondari, tuijulize swali la msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jJe, Kata zetu zimegawanyika sawa sawa! Kata ya Hogoro watu 27,000, Kata ya Mkoka watu 29,000. Tugawe Kata ili Watendaji hawa wa Kata na Madiwani watakaopatikana baadaye, wasimamie masuala haya ya ujenzi wa Sekondari na maendeleo mengine ya Vituo Vya Afya na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili tulipe kipaumbele sana, mapendekezo yalishakuja TAMISEMI muda mrefu. Tunawaomba tu muangalie mafaili. Kama hayapatikani vizuri tuarifuni, tulete tena upya kwa mtazamo ambao upo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Harith Mwapachu na *IGP* mpya Ndugu Said Mwema na wenzao katika Wizara yao ya Usalama wa Raia kwa kazi nzuri sana ambayo wameifanya ya kupambana na majambazi. Wamefanya kazi nzuri kweli. Lakini kuitia nafasi hii niwajulishe kwamba baadhi ya yale majambazi ambayo wameshughulika nayo huko mijini, sasa yanakimbilia vijijini. Watu hawalali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule kwangu Kongwa, kwenye Bunge lililopita kama Mheshimiwa Charles Keenja yupo, nilitumia miaka miwili kumshawishi Bwana tembelea Kongwa, nikupeleke kwenye kijiji kimoja uone vijana wanavyohangaika. Mwisho kabisa pale akanikubalia, tukaenda naye, tulitoka hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikampeleka kijiji kinaitwa Hembahemba. Hakuamini, akasema mbona hukuniambia nije na Waandishi wa Habari na nikawa nimewaambia wananchi wangu andaeni matrektta Waziri wa Kilimo na Chakula aje aone, maana tuna mradi wa pembejeo, wananchi wangu hawajawahi kukopa hata trekta moja. Lakini, Hembahemba pale akakuta zaidi ya trekta 50 kijiji kimoja wamezipanga kwenye uwanja wa mpira na pikipiki kadhaa na kadhalika. Alishangaa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikamwambia juhudhi yote hii hawa wananchi wamefanya wenyewe. Ile mipango mlioweka kule *Exim Bank*, sijui wapi na wapi, huku haifiki. Hawa watu hawana hati miliki wala nini. Kwa hiyo vijana wanajitahidi kweli. Wanununa *Fuso*, wanununa *Tractors*, wanajenga nyumba za kisasa kwa kuhangaika wenyewe. Hii mipango ya kwetu sisi haiwafikii. Sasa katika kuhangaika kwao hali imebadilika baada ya majambazi hawa kukimbilia vijijini. Ndani ya mwaka huu peke yake *SACCOS* ya Kata ya Mlali imevamiwa na majambazi, wakaibiwa shilingi milioni 3.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndani ya mwaka huu peke yake *SACCOS* ya Kibaigwa ambayo ilikuwa ni *SACCOS* bora katika Kanda ya Kati. Tulikuwa tunategemea kuipandisha hadhi iwe ni Benki ya Wananchi, mlisikia ninyi nyote Waheshimiwa Wabunge, imevamiwa na kuvunjwa wameiba zaidi ya shilingi milioni 14.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi Jumamosi wamevamia *SACCOS* ya Kata ya Hogoro na wameiba fedha, sijapata idadi yake ni kiasi gani. Ndani ya mwaka huu mfanyabiashara mmoja pale Ntanana alivamiwa na kuuwawa. Wiki moja kabla ya *SACCOS* ya Kata ya Hogoro kuvamiwa, kwenye Kijiji cha Songambele, mwananchi mmoja alikuwa amepeleka *Fuso* nimejaa mahindi kuuza Dar es Salaam alivyorudi, usiku ule ule alivamiwa na majambazi akauwawa, na majirani zake wawili walikuja kumsaidia waliuwawa pia, wiki mbili zilizopita. Tumenda pale kuzika maiti tatu kwa mpigo. Kijiji kizima kimezizima.

Mheshimiwa Naibu Spika, huko Hembahemba, kijana mmoja naye kauza mahindi yake gunia 100, wamefuata siku hiyo hiyo, bwana, wewe umeuza 100, umepokea kiasi fulani, lete, kauwawa. Kijiji kimoja kinaitwa Ndulugumi, kijana kafuga nguruwe wake, kauza nguruwe wake 30 siku moja, wamemfuata usiku ule ule, ameuwawa na wamechukua pesa.

Mheshimwia Naibu Spika, kwa hiyo, juhudhi hizi za usalama inabidi ziangaliwe upya eneo hili la ulinzi na usalama. Pendekazo langu, Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya ziangaliwe mfumo wake. Je, mfumo ulioko sasa unatosha, unakidhi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Halmashauri za Wilaya ikiwezekana tuwe na kikao kimoja cha kujadili matatizo ya kiulinzi na kiusalama. Tusiachie tu kikundi cha watu wachache. Tukishajadili sisi wao wakakae kwenye kuweka mipango na mikakati ya kutekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa hakuna *forum*. Hatujui kama wanakaa sawa sawa au vipi! Hilo ni pendekezo muhimu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kongwa ina vituo viwili tu vya polisi. Kituo cha Kongwa Mjini na Kituo cha Mkoka, tunaomba Kituo cha Kibaigwa kifunguliwe haraka na hili nimelisema kwa miaka minne mfululizo, hatujasikilizwa bado. Kibaigwa panastahili polisi kwa sababu pana soko la kimataifa na ndiyo kwenye kichaka cha baadhi ya majambazi. *Recruitment* ya polisi itazamwe utakuta wanatakiwa vijana kumi kwenye Wilaya, Wilaya inachagua vijana wakifika *level* ya Mkoa nane au tisa au wote kabisa wanarudishwa wanapatikana wengine katikati ndio wanakwenda kuwa polisi. Tusikubali kabisa hili Jeshi liwe ni la nchi nzima pamoja na Majeshi mengine. Kama wamepungua sifa ilitakiwa Wilaya ile ile ijaze kuliko utaratibu ulioko sasa ndiyo unaotuletea matizo. *(Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuangalie kwa nini kuna matatizo kiasi hiki. Namwonea huruma Waziri wa Usalama wa Raia, ana kazi kubwa kweli. Gongo inapikwa mbele ya Gairo pale Turiani zinajazwa *Fuso* kadhaa zinapita barabara ya lami mpaka Kibaigwa, Kongwa, hawaoni? Vituo vya gongo vinafahamika polisi hawaoni? Vijana hawafanyi kazi wanacheza kamali na kuvuta bangi haijulikani kweli? Polisi wako wapi? Ni eneo ambalo ninaishukuru sana Serikali ya Awamu ya Nne imeanza nalo vizuri sana.
(Makofit)

Lakini nilichosimama kuzungumza hapa ni kwamba kazi bado mbichi kabisa, sasa tuongeze juhudii tuimarishe, tushone kabisa ili ujambazi huu uishe kwa vile sasa ni hatari sana kwa kila kijana anayejjitahidi sana kupambana na umaskini na kuwa na hali bora kidogo, huyo kijana majambazi wanamlenga sasa huyo anaondoka. Kwa hiyo, hii itakatisha tamaa sana wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante. (*Makofî*)

MHE. MAIDA HAMADI ABDALLAH: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuweza kutujalia kuwa hai na wenyе afya njema na kuweza kukutana katika ukumbi huu mpya tukijadili Bajeti ya Serikali yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, naomba nichangie hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, aliyoiwasilisha mbele yetu katika mapitio ya kazi na Bajeti ya Serikali ya mwaka 2006/2007. Pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake ambayo haikuacha kitu katika kumwendeleza Mtanzania kuondokana katika uchumi ulio nyuma. Imezingatia zaidi ahadi zilizopo katika Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 2005. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niseme tu kuwa naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Mheshimiwa Waziri Mkuu hotuba yake imeangalia zaidi suala zima la MKUKUTA ili kumtoa Mtanzania katika uchumi ulio nyuma na kumwendeleza katika uchumi tegemezi katika taifa linalojitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwezeshaji wa wananchi kiuchumi kwa kupatiwa shilingi milioni 500 kila Mkoa tuzingatie zaidi katika vikundi vyta ushirika (*SACCOS*) zilizopo. Lakini zaidi ukiangalia zaidi katika Mikoa yetu pamoja na kuwa zimetolewa shilingi milioni 500 kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kiuchumi, lakini bado kunakuwa na usumbufu katika kuzipata fedha hizo.

Kwanza wananchi wanapokwenda katika hatua mbalimbali katika kuzipata fedha hizo wanaweza wakawekewa vikwazo vyta hatimiliki na mengineyo. Hizo hati miliki katika kushughulikia wanaweza wakafika hata miezi sita hawajaipata hatimiliki. Kwa hiyo, naomba Serikali ishughulikie katika suala hilo ili kuwawezesha wananchi kuwaendeleza kiuchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *TASAF I* ilifanya kazi nzuri kwa upande wa Tanzania Zanzibar na kwa upande wa Tanzania Bara. Kwa hiyo, naipongeza Serikali kwa kuweza kufikia lengo walilokusudia. Naiomba *TASAF II* itekeleze yale malengo yote yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nizungumzie kuhusu suala la elimu. Kwa kweli nchini Tanzania bado tumeshuka katika kiwango cha elimu. Lakini kushuka katika kiwango cha elimu kumetokana na kuwa wapo wasomi wengi waliofikia kidato cha sita na wengine wapo waliofikia kidato cha nne lakini wazurura kutoptana na kukosa ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naishauri Serikali kuangalia vijana hawa ambao wanahangaika bure matokeo yake wanajiingiza katika vikundi vyta uporaji, wizi na dawa za kulevyo. Kwa hiyo, naishauri Serikali kuliangalia suala hilo kwa vijana ambao ni wasomi lakini hawana ajira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika usala hilo hilo la elimu, kuongeza ajira za walimu kwa kweli tuna upungufu mkubwa wa walimu katika nchi yetu. Pia suala la

elimu limeshuka pia kwa kuzingatia zaidi wengi wanashindwa kulipia gharama za elimu. Mwanafunzi anakuja kukulamikia atakwambia nimefaulu kuingia kidato cha nne, tano, au cha sita mpaka kuendelea Chuo Kikuu lakini, anashindwa kabisa kulipa gharama za kuendelea na masomo hayo. Kwa hiyo, naiomba Serikali kupunguza gharama hizo ili kuwasaidia wale ambao hawana uwezo wa kulipia gharama hizo. (*Makofi*)

Pia namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika Bajeti yake amesema kuwa kuna wanafunzi walibahatika kuingia katika kidato cha kwanza lakini walishindwa kuendelea kutokana na upungufu wa majengo ya shule za Sekondari. Kwa hiyo, naipongeza Serikali kwa kuongeza majengo ya sekondari na kuongeza madarasa na kuendelea na masomo wanafunzi hao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la viwanda bado nchini Tanzania tunayo matatizo makubwa ya upungufu wa viwanda. Katika kutekeleza juhudzi za kuondoa umaskini tunaiomba Serikali kulifirkira zaidi suala la viwanda kwa kuwakaribisha wawekezaji katika suala la viwanda.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia zaidi katika nchini Tanzania tunayo mazao mengi yanayofaa kutengenezwa *juice*, lakini bado tunategemea *juice* kutoka nchi za nje. Kwa hiyo, naiomba Serikali kulifirkira suala hili ili kuwapatia ajira vijana wetu kwa urahisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la UKIMWI, Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hotuba yake kafafanua vizuri kuhusu suala la maambukizo ya UKIMWI. Kwa hiyo, mimi naongezea kwa kusema kuwa tujitahidi kuwahamasisha vijana Mijini na Vijiji pamoja na familia zetu ili kujikinga na maambukizi haya na vile vile kuwahamasisha wale ambao hawajaathirika kwenda kwenye vituo vyta afya kupata ushauri nasaha na kupima afya zao na kujija kama kweli wameathirika au hawajaathirika ili kupata ushauri nasaha na kupata utaratibu mzima wa utumiaji wa kupata dawa za kurefusha maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kilimo nataka nizungumzie suala hili kuhusu kilimo kwa upande wa Zanzibar. Naiomba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ishirikiane na SMZ katika suala zima la kilimo cha Zanzibar. Wakulima wa Zanzibar bado hawajakuwa na kilimo endelevu kutokana na kutokutumia mbolea, kutokuwa na huduma za ugani katika kilimo cha umwagiliaji kwa hiyo, naomba Wizara ya Kilimo ya Muungano ishikiriane na Wizara ya Kilimo Zanzibar katika kuliona suala hili ili wakulima wetu waweze kuendelea katika uzalishaji wa kilimo cha umwagiliaji maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumzie suala la Jengo letu la Ikulu ya Wete, nataka nilithibitishie Bunge hili kuwa Ikulu ya Wete ni Ikulu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na bado Ikulu hiyo iko katika hali mbaya, hairidhishi kabisa kuonekana kama hii ni Ikulu ya Jamhuri ya Muungano au ni Ikulu ya Rais wa Jamhuri ya Muungano. Utakumbuka kuwa nilimuuliza swali Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Ikulu na akanithibitishia kuwa Ikulu hiyo ni ya SMZ lakini bado nimthibitishie kama Ikulu hiyo ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa sababu wafanyakazi

waliostaafu katika Ikulu hiyo wamelipwa mafao yao na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mpaka sasa hivi hapajakuwa na uthibitisho kamili kama Ikulu hiyo ni ya SMZ.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati huo huo Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tatu, alipofanya ziara Kisiwani Pemba mwaka 2004 alipangwi katika Ikulu ya SMZ kutokana na hali ya Ikulu hiyo ilivyo, kwa hiyo, baada ya kufanya matayarisho katika Ikulu ya SMZ yeye kabla hajamaliza shughuli zake akaseme mnanipeleka wapi, tukawmambia unakwenda Chake Chake, akasema hatu mimi nastahili kupata mapumziko katika Ikulu yangu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nikitoka hapo ndiyo naondoka.

Kwa hiyo, ikibidi tufanye marekebisho katika Ikulu ya SMZ matayarisho yote tuliyofanya Ikulu ya SMZ tuhamishie katika Ikulu ya Jamhuri ya Muungano pale Wete. Kwa hiyo, naiomba Serikali kuliona suala hili na kuliingiza katika bajeti ijayo katika kushughulikia matengenezo kamili ya Ikulu hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nami napenda nichukue nafasi hii, kukushukuru kwa nafasi uliyonipatia ya kuweza kuchangia hotuba hii katika Bunge lako Tukufu. (*Makofi*)

Vile vile napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mwenyekiti wa Chama chetu cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Vile vile napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Wabunge wenzangu waliochaguliwa kushika nafasi za juu katika Chama cha Mapinduzi. Vile vile napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri Mkuu, kwa hotuba yake nzuri ambayo amewasilisha leo hii katika Bunge letu. Nawapongeza pia Mawaziri, Manaibu Waziri, Makatibu Wakuu walioko kwenye Wizara hiyo ya Waziri Mkuu kwa kumsaidia Waziri Mkuu katika kuandaa hotuba hii nzuri ambayo imewasilishwa leo kwetu. (*Makofi*)

Mimi binafsi naanza kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Kwa kweli hii hotuba inatuonyesha mwelekeo mzuri wa Serikali inaelekea wapi na imetupa matumaini makubwa siyo sisi Wabunge tu bali hata wananchi waliokuwa wakisikiliza hotuba hii ya Waziri Mkuu. Mimi binafsi nitapenda kuchangia kwenye sekta ya kilimo kama walivyofanya wenzangu lakini sitapenda kuongea maneno mengi kwa sababu mengi yameshaongelewa na wachangiaji waliopita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuongelea hali ya ukame. Hali ya ukame imekuwa ni balaa kubwa katika nchi yetu na hatimaye kusababisha nchi yetu kuingia katika janga la njaa. Tumepata tatizo la kutumia fedha zetu za kigeni kuagiza chakula kutoka nje ya nchi na hata kuomba msaada wa chakula kwa wahisani. (*Makofi*)

Vile vile hali hii ya njaa imesababisha umaskini mkubwa kwa wananchi wengi ambao wanategemea sekta hii ya kilimo kwa karibu asilimia 70. Hali hii ya njaa pia imesababisha ucheleweshaji wa utekelezaji wa mipango muhimu ya maendeleo kama vile mpango wa MKUKUTA na ile ya *millennium development goals* ambao tumeipanga kuitekeleza katika kipindi chote cha mwaka 2005/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kabla ya kuendelea inabidi tuangalie ni sababu zipo zimesababisha, je, zipo sababu mbadala maana yake tumekuwa tukilalamika mvua, je, sababu mbadala ni nini ambazo zimesababisha hali hii ya ukame? Katika ukurasa wa 12 wa hotuba ya Waziri Mkuu amefafanua ufumbuzi wa kudumu katika kukabiliana na tatizo hili la njaa. Lakini ni lazima tukubali Wabunge wote tulipo humu ndani na Watanzania kwa ujumla kwamba kilimo chetu bado ni duni sana, bado Watanzania wengi wanatumia jembe la mkono kwa hiyo, mimi nafikiri sisi Wabunge pamoja na Serikali kwa ujumla wakati umefika sasa wa kuwahimiza wakulima waache kutumia jembe la mkono na kutumia zana za kukokotwa na wanyama, vile vile na matreta katika kuimarisha sekta hii ya kilimo. (*Makofi*)

Vile vile kuna kilimo cha viraka, viraka, mtu analima hapa, anahama analima pale, mimi nilikuwa nafikiri kuna haja ya kuanzisha *style* ya kupima maeneo na kuwayaweka katika *style* ya *blocks* ambayo itasaidia *ma-extension officers* kuwashudumia wakulima ipasavyo. Mashamba yakiwa katika mtindo wa *blocks* inakuwa ni rahisi kutoa utalaam inavyopaswa na kuachana na kilimo cha viraka viraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tukitegemea sana mvua katika kilimo lakini yapo maeneo ambayo yako kandokando ya mito, maziwa ambayo tukiyaimarisha vizuri tunaweza kuyatumia vizuri sana kwa kilimo, hasa maeneo yaliyoko kandokando ya ziwa kama maeneo ya Mara, Mwanza na hata Bukoba tukiyatumia vizuri tunaweza tukaendeleza kilimo chetu vizuri. Nimeona Mheshimiwa Wilson Masilingi, amefurahi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia maeneo ya mabondeni rasilimali zinazohitajika hapa ni chache sana kwa hiyo, maeneo haya tukiyaangalia vizuri tunaweza pia tukiyatumia vizuri katika kilimo. Hotuba inazungumzia kuwepo kwa Mfuko wa Pembejeo katika ngazi ya Wilaya. Lakini mimi kama Mbunge nilikuwa nashauri si kwa ngazi ya Wilaya peke yake, lakini tuanzie ngazi ya Kata na hata kijiji ili kumrahisishia kila mkulima msimu unapoanza aweze kupata pembejeo kwa urahisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile napenda pia umuhimu utiwe katika hawa *ma-extension officers* kumekuwa na vyuo vingi sana vya *extension officers*, lakini je, wanao utalaam wa kutosha? Maana yake mimi ninavyoolewa kila Mkoa unakuwa na *package* ya utalaam fulani katika kilimo. Je, hawa watu wanapokuwa *posted* kwenye maeneo wanao huo utalaam?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano Afisa Ugani anakuwa *posted* kule Mwanza, je, anayo *package* nzima ya ukulima wa zao la pamba? Mimi nilikuwa nafikiri

tuwa- *post* hawa Maafisa Ugani wakiwa na *package* kamili kutokana na Mikoa jinsi mazao yanavyolimwa. (*Makofi*)

Vile vile hawa maafisa ugani wamekuwa hawana motisha, hawana vitendea kazi na mishahara yao imekuwa ni midogo sana. Hii inawapelekea wasiweze kufanya kazi yao inavyopaswa na kuwasababishia wakae ofisini muda wote baada ya kuzunguka kwa wakulima kama inavyotakiwa.

Jambo lingine ambalo ningependa kuchangia katika hotuba hii ni Sekta ya Afya. Kwanza napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Wizara kwa kuwaongezea mishahara madaktari na hatimaye kuwarudisha kazini. Lakini hii peke yake haitoshi kwani watu hawa wamekuwa wakifanya kazi muda mrefu sana. Daktari anaingia asubuhi pengine analala huko huko haonani na mke wake, haonani na mume wake yaani analala huko huko hospitali, hajui watoto, hajui chochote yaani daktari ukimuuliza yeze na wagonjwa. Sasa lazima tuwafikirie watu hawa wanafanya kazi katika maeneo magumu sana. (*Makofi/Kicheko*)

M heshimiwa Naibu Spika, mimi mume wangu ni daktari naelewa. Kwa kweli watu hawa wana kazi ngumu sana yaani vile anavyoondoka asubuhi unaweza ukamuona kesho yake lakini *at the end of the month* mtu anapata mshahara ambao ni kidogo sana. Kwa hiyo, Serikali iwafikirie kwa ukaribu sana watu hawa ili waweze kufanya kazi yao inavyopaswa. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii pia inawasababisha madaktari hawa waweze kukimbilia nje kutafuta *green pastures*. Kwa hiyo, Serikali inawasomesha lakini *at the end of day* tunajikuta hatuna madaktari katika nchi yetu ya Tanzania. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Serikali iwaangalie kwa ukaribu sana madaktari wa nchi yetu hasa Madaktari Bingwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuchukua nafasi hii pia kuisemea kidogo Hospitali yangu ya Mkoa wa Mara. Kwa kweli ukienda kwenye hii hospitali utasikitika ukiingia pale wodi ya wazazi, wanawake wanalala wanne, wanne, mtu amebanwa na uchungu watu wapo kitandani wamebanana. Kwa kweli hali hii inasikitisha sana. Tulikuwa tunaomba mtufikirie angalau Mkoa wa Mara muweze kutupa nafasi ya kutosha hasa kwa wodi ya wazazi na wodi ya watoto.

Vile vile tuna daktari mmoja tu bingwa. Sasa hapa tunapoongelea mimi nashindwa kuelewa binafsi, wakati nashindwa kuelewa hivi Mkoa wetu wa Mara uko Tanzania? Naona daktari mmoja kwa Mkoa mzima huyo huyo Gainakolojisti, *Pediatrician* huyo huyo *Surgeon* yaani mambo yanakuwa magumu sana. Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba angalau Serikali itufikirie kuwapeleka Madaktari Bingwa, japo hata watatu wakaweza kusaidiana na yule mmoja aliyepo ili kuweza kuendeleza sekta hii ya afya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile ningependa kuongelea hizi *NGOs* ambazo zinaanzishwa kwa ajili ya UKIMWI. *NGOs* nyingi wamekuwa wakitumia UKIMWI

kama mgongo tu, wanakaa hapo juu wanaweza kuanzisha *NGOs* zao lakini wanakuwa hawasaidii a wagonjwa wa UKIMWI. Inakuwa ni kama njia mojawapo ya kujipatia kipato. Misaada inakuja lakini haifiki kwa walengwa. Kwa hiyo, mimi binafsi nilikuwa naomba hizi *NGOs* zote ziangaliwe kama mtu kaanzisha *NGO* kwa ajili ya kusaidia wagonjwa wa Ukimwi basi iwasaidie ipasavyo na si vinginevyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri nimetumia muda wangu vizuri sana kwa mara nyingine narudia kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hoja yake nzuri na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaomba radhi Mheshimiwa Juma Killimbah, kufuatana na kifungu 49(2) wewe umekwishachangia katika Bajeti ya Fedha na kwa mujibu wa Kanuni hii kama umeshachangia na wanaochangia ni wengi na muda hautoshi kwa hiyo, wewe ulishachangia katika Bajeti ya Fedha. Kwa hiyo, sitakupa nafasi badala yake nitampa nafasi Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Sanya. (*Makofi*)

MHE. IBRAHIM MOHAMED SANYA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nichukue nafasi hii, kumpongeza Mwenyekiti mpya wa Chama cha Mapinduzi aliyechaguliwa jana. Sambamba na kuwapongeza wenzake wote waliochaguliwa kufanya naye kazi bega kwa bega. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi mara nyingi tunaposimama katika Bunge hili huwa tunaambiwa ama humu ndani ya Bunge au hata nje ya Bunge kwamba tunajali sana maslahi ya Zanzibar kuliko maslahi ya upande mwingine wa Muungano. Lakini nataka nielezee kitu kimoja sisi tumetumwa na wananchi wetu, tumechaguliwa kwa kura halali kuwawakilisha wananchi, kwa hiyo, lazima kwanza tuzingatia na kuchangia michango madhubuti inayowahusu wao waliotutuma na baadaye tuka-cross ocean tuje zetu upande wa pili wa Tanzania Bara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi leo nitakachokizungumzia zaidi ni maslahi ya Zanzibar katika Muungano. Muungano huu umedumu kwa miaka 40 na ni tunda la kulifurahia na kulijenga na kuliengayenga ili lifike mahali ujulikane kwamba ni muungano wa kweli madhubuti unaoleta manufaa kwa pande mbili za Muungano yaani Zanzibar na Tanzania Bara. (*Makofi*)

Tatizo kubwa lililojiteza hapa kuna *crisis* mbili *crisis* ya kisiasa ya Zanzibar na matatizo ya Muungano ambayo sasa hivi yamekaliwa kitako kutokana na mwamko mzuri na jasiri wa Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, wa kuanza kuleta *dialogue* baina ya watu wa Zanzibar na watu wa Tanzania. Lakini sasa tuangalie suala moja, hivi kweli tuko *serious?* Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, alipotoa hotuba yake katika Bunge la Jamhuri ya Muungano hotuba ya kwanza aligusia mpasuko wa kisiasa ulioko Zanzibar na akasema atautafutia dawa. (*Makofi*)

Lakini ninachotaka kusema mimi baada ya kumaliza hapo Mheshimiwa Rais akawachukua watendaji wake wote akawapeleka Arusha kwenda kuandaa mikakati ya kuanzisha mbinu mpya za kuendesha Serikali mpya ambayo inakwenda kwa ari mpya, kasi mpya na nguvu mpya. Hatukatai hilo, baada ya muda mfupi tu Waziri Mkuu,

akakutana na Waziri Kiongozi wa Zanzibar kujadili mambo yanayohusu Muungano. Lakini mimi nasema tusimalizie hapo hili ni suala la Watanzania, tuwashirikishe kikamilifu viongozi mbalimbali na wananchi wa kawaida na wasomi wa nchi hii wakiwemo wanasheria wakuu, Viongozi wa Kidini, Viongozi wa Vyama vyaa Siasa ili tulete mustakabali na tutoke na kitu kizito kitachokuwa tena hakina sulubu ndani yake isipokuwa kusimamia maendeleo ya Muungano kwa pindi zote mbili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu spika, tuchukulie mfano mmoja mdogo tu kwa hili suala la Muungano. Suala la Muungano kuna mambo mengi tu sisi hatufaidiki nayo. Niliwahi kuuliza suala katika Bunge hili hili kipindi kilichopita kuhusu *Air Tanzania* nikaambiwa kwamba Zanzibar hatuhusika wala si Shirika la Muungano. Itakuwaje iwe hatusiki halafu katika Bodi ya Wakurugenzi kuna Mzanzibar, katika Menejimenti kuna Mzanzibar wamekujakujaje, kwa *formula gani?* Mbona kwenye Bodi ya Wakurugenzi na Menejimenti ya *railway* hatumo sisi Wazanzibar, *definitely* kwa sababu sisi tuna *share* yetu katika *Air Tanzania*. Shirika hili likaingia *airline* na *South Africa* matokeo yake sasa ni *burden*. Tunakwenda na hasara ya bilioni tatu na Serikali bado haijaliona hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni tatizo kubwa kwamba barabara unaiona ina miba na bado unatembea kwenye barabara hiyo hiyo, inakuchoma miba hiyo hiyo kwenye miguu yako. Kwa nini mara moja tusizifanye hivi ndege za *Air Tanzania* zikawa *grounded tuka-review* mikataba yetu na *South Africa* ili tusiweze kuendelea kubeba mzigo na lawama ya hasara zinazoingizwa na Shirika la Ndege la Tanzania? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu spika, achana na hilo, mimi nakumbuka wakati alipokuwa Rais Aboud Jumbe, Elimu ya Juu na Ufundu ilioneckana kwamba Zanzibar kiwango chetu cha elimu hakifanani na kiwango cha wanafunzi wanaosoma Bara. Ikitengenezwa mipango na *formula* ya kutuwezesha sisi kwa viwango vyetu hivyo hivyo tuchukuliwe tuingizwe katika Vyuo Vikuu ili watoto wetu wasome na ndugu zetu wengi tu wa *attain degrees* kutoka *Universities* za Dar es Salaam na nyinginezo kwa msaada huo, leo nafasi hiyo imeondoshwa, anapotaka Mzanzibar nafasi ya Chuo Kikuu Bara, hata kama ana *division one* inabidi aende kwenye *matriculation* na asichaguliwe utaona zile nafasi ni ndogo sana kwa upande wa Zanzibar, kwa sababu wanafunzi wetu ni kidogo na wanaopasi ni kidogo.

Kwa nini zirejeshwe nafasi zile wakapata Wanzanzibar nao wakaendelea kusoma, kuna tatizo gani? Si mna nia safi ya kutusaidia sisi. Halafu mnapokuja kutenga nafasi za wananchi wa Zanzibar kujaza nafasi kama za Mabalozi nchi za nje, nafasi za Benki Kuu, tunaambiwa hamna watu wenyе *qualification* nyingi, kwa nini hatuna? Elimu ya juu ya ufundu ni chombo cha Muungano, kwa nini ndugu zetu mnatoa kauli kwamba mko tayari kuisaidia kiuchumi Zanzibar huwezi ukasaidia uchumi mahala popote bila ya kwanza kumfunza raia wako ukampa elimu inayofaa na inayokwenda na wakati ili aweze kuchukua nafasi nzuri katika madaraka ya kuongoza mashirika au ya kufanya kazi katika sehemu muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TRA* ni Shirika la Tanzania. Liko kisheria lakini *TRA* hao hao wanawa-harass Wazanzibar kiasi ambacho leo wafanya biashara mimi nawajua

zaidi ya 15 wamehamishia biashara zao kutoka Zanzibar wanakuja Bara. *Revenue* ile ilikuwa inaingia katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Leo haingii tena. Anakwenda mfanyakazi wa *TRA* dukani, anakwenda kwa nia safi tu kwa sababu yeze ni *collector* na anaisaidia Serikali kuwa na *revenue* nzuri lakini wanapo-negotiate mfanya biashara kutokana na kiwango cha biashara kuanguka anafika mahali anamwambia unapenda utalipa, hupendi funga biashara yako. *This is not a language.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima wawe na nidhamu ya kuwatembalea wateja, mteja ni mfalme. Halafu *TRA* hawa hawa, kiutendaji wanaruhusika wakati wote kuja kuangalia biashara zako, *investment* yako. Lakini anakuja anarejesha *investments* ya miaka mitano. Biashara ya miaka mitano uliyofanya nyuma anakuabia faili lako liko hivi. Kwa hivyo, tunachotaka sasa ufanye ulipe malimbikizo haya au idadi hii ya fedha ambayo hukulipa huko nyuma. Hatukatai, wanaruhusika kisheria. Lakini ukianzia na mpango huo unakarabisha mianya ya rushwa ndani yake. Kwa nini wasipitie kila baada ya mwaka. Kwa nini wasipitie kila baada ya miaka miwili.

Mheshimiwa Naibu spika, kwa hiyo, haya yarekebishwe haraka sana. Vyombo vyetu vya Muungano, chukulia mfano nzuri wa *immigration*. Kuna vijana wetu Zanzibar pale wamekuja kusoma na vijana wao wazawa wa Bara huku. Wakapasi sawasawa, waliporejea wakafanya kazi Zanzibar, matokeo yake wao mpaka leo zaidi ya miaka 8 hawajapewa vyeo. Wenza huku tayari wamepandishwa vyeo. Kwa nini? Si *rank* wamesoma pamoja, wanatumikia Taifa moja, wanatumikia umma mmoja? Sasa haya matatizo madogo madogo kama haya kuangalia ndiyo haya yanawafanya Wazanzibar waamke kisiasa waone kwamba kuna kitu hiki, labda kuna kitu hiki.

Sasa jambo lingine ambalo nataka kulizungumzia ambalo ni muhimu sana. Mimi sijapata kuona kiongozi wa nchi hii katika mfumo wa vyama vingi aliyekuwa jasiri kushinda Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete. *He is really logic.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi alikuja hapa akafanya mikutano ya kisiasa baina ya viongozi Wabunge wa CCM halafu akatutengea muda sisi, tukazungumza naye mambo mazito sana na akayachukua vizuri kabisa na tukajua kwamba *President* yuko *serious* kushughulikia matatizo ya kisiasa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hatuwaambii alichozungumza. Mnatutafuta sana lakini hatuwaambii na hatutawaambia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu spika, lakini sasa Zanzibar kuna tatizo la kisiasa. Tatizo la Zanzibar la kisiasa siyo la historia kama mnavyoliona ninyi na historia yetu isitufunge ikawa ndiyo kitanzi cha kujimaliza katika Visiwa hivi vya Unguja na Pemba au katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa nini nikasema hivyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Afrika ya Kusini chini ya Nelson Mandela juzi, baada ya kupatikana Uhuru watu wali-*expect* lingine kabisa. Lakini akaona hakuna, *no, no way back. Is a nation, is a rumble nation.* Akaondosha tofauti baina ya mzungu na muhindi na *colour* na *African as indigenous* akawafanya kitu kimoja, Taifa moja, hatua moja mbele na sasa hivi tuwaoneni *South Africa*. Msumbiji walipigana pale miaka mingapi.

Angola, leo historia imekwisha, wanajenga nchi zao, *economy* inakwenda. Sisi kuna watu wawili, watatu tu ambao hawavitakii mema Visiwa vyetu vya Unguja na Pemba. Rais Jakaya Kikwete, tunakuomba na tunakutaka uwe na msimamo huo huo, asiyetaka akae upande wa kushoto sisi tutakuwa na wewe bega na bega tuondoshe matatizo ya Zanzibar na tuijenge Zanzibar mpya kwa matumaini ya Wazanzibar na Watanzania na kwa ajili ya Bara la Afrika nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vietnam ilipigana miaka mingapi na Marekani, 50,000 walipotea Wamarekani pale. Leo Vietnam kuna ma-investors kutoka Amerika. Japan ilipigwa bomu la Hiroshima, leo tuwatazame Wajapan wanafanya kazi na Wamerekani. Rwanda hiyo hapo ukiwazungumzia mambo yaliyofanyika Rwanda wanakuambia tunaona aibu, tumesahau, tunakwenda mbele, tunaangalia mustakabali wa nchi yetu. Hapa hakuna Mtusi, hakuna Mhutu, kuna Mrwanda na Mnyarwanda. Leo Zanzibar mpaka leo ukizungumza watu wanasema hakuna matatizo, hawayaoni kwa sababu kengeza, wanaona nusu nusu. Lakini matatizo ya kisiasa yapo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri Mkuu nakuomba sana hili, kipindi hiki ambacho Rais Jakaya Kikwete amechukua nafasi zote za uongozi wa Chama na uongozi wa Serikali kusimamia kidete na kuondosha tatizo hili. Tumechoka, tumechoka, tumechoka na Wazanzibar tumaini lao jipya ni kutoka kwenu katika uongozi mpya unaoongozwa na Rais jasiri, Rais Jakaya Mrisho Kikwete. (*Makofi*)

Mwisho nimalizie muda wangu unakwisha, nizungumzie Dodoma. Tuna jengo zuri, tuna Wabunge madhubuti, imara, wenye mwamko wa kisasa. Tuna vijana wengi tu, Wazee wanaanza kung'atuka na waliobakia 2010 tuwamalize. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachotaka sasa mji wa Dodoma uonekane kama Dodoma. Mheshimiwa Waziri Mkuu namwomba, tuwekewe mataa ya barabarani kutoka kwenye majumba mapya yapite *round about* yapite kwenye jengo letu, yamalizikie kwenye *Zuzu round about* yaelekee Hospitali na mengine yaelekee *Airport* na mengine yaelekee juu kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu na nyumba yake na Dodoma Hoteli walau watu wa Dodoma wajue kwamba sasa Serikali yao iko *serious* inataka kuleta mabadiliko na kuonekana Dodoma inang'ara. (*Makofi*)

Hivi sasa Wabunge wakitoka na magari yao na Waheshimiwa Mawaziri utafikiri tuko New York, wacha tarehe 15 Agosti tuondoche hapa. Kila mmoja anaogopa kutoka bila ya tochi. Kwa sababu nini kinachong'arisha mji wa Dodoma ni mataa na magari ya Waheshimiwa Wabunge. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, juzi hapa alikuja Waziri Mkuu wa Uchina, akatoa nafasi nzuri tu ya kusafirisha mazao ya nchi yetu kwa kuondosha ushuru kule China. Lakini Wachina wako mbali, wanataka bidhaa za kisasa, zilizokuwa *packed* kwa njia *standard* ya kisasa, je tume-determine kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia bajeti hii ya Mheshimiwa Waziri nikiwa kitinda mimba kwa siku ya leo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi ya awali kumpongeza Mheshimiwa Rais, Jakaya Mrisho Kikwete, Waziri Mkuu na Serikali nzima kwa jinsi wanavyoenda sambamba na kauli mbiu ya kasi mpya, nguvu mpya na ari mpya. Mungu awabariki sana, awape afya, maarifa, hekima ili Taifa hili liendelee kufarijika na uongozi wenu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nitumie nafasi hii kumpongeza Spika, wewe mwenyewe na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwa kuteuliwa kwa nafasi zenu. Kwa kweli nyinyi akina mama mmeweka historia ya nchi hii na mmetujengea heshima kubwa sisi akina mama wa Tanzania. Mungu awatangulie sana sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo sasa nitumie muda huu kuchangia Bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu iliyo mbele yetu. Mimi naanza na suala la dawa za kulevya. Suala ambalo linanikera kweli kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wanaoingiza dawa za kulevya, hivi Serikali haiwajui. Mbona kama naona wanafahamika na kama wanafahamika kwa nini tusiwafichukue na wanaouuza dawa za kulevya ina maana hawafahamiki? Mimi mwenyewe naishi Dar es Salaam kipindi cha Kamati. Kwa vipindi hivyo tu ninavyokaa Dar es Salaam vitu kama hivi naviona. Hata ukinichukua leo kwamba tuonyeshe, kwamba mlango ule pale na mlango ule pale. Kwa nini Serikali inapata kigugumizi kwa hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imegawanya Mkoa wa Dar es Salaam kuwa mikoa mitatu, tuna ma-*RPC* watatu. Tuna Kamishna wa Kanda, *IGP* yuko kule, kwa nini Jiji la Dar es Salaam lisafishwe. Tunataka Jiji la Dar es Salaam lisafishwe. Madawa ya kulevya yanaathiri vijana wetu. Taifa la kesho, tunategemea watashika nafasi mbalimbali tutakapong'atuka. Lakini wameathirika, Taifa la leo na kesho wameathirika. Wanatembea ovyo ovyo barabarani, hawaijishughulishi, wamekuwa kama wajinga. Ninaomba Serikali itazame kwa undani sana sauala hili, na ikiwezekana basi vijana hawa tuangalie namna ya kuwasaidia. Wameathirika, wagonjwa, watibiwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vijana wetu hawa, tunawahitaji, wamekuwa kero katika familia na yote haya kwa sababu wale wachache tunaowafumbia macho. Nina hakika maaskari wa Dar es Salaam wanafahamu hili. Sasa madawa ya kulevya yameshafika mpaka Singida. Niambie nchi inavyokwenda sasa. Tunatokomeza ujambazi tunasahau hili. Kwa nini tuisafishe yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara ya Usalama wa Raia iende sambamba kwa mambo yote ambayo ni kero kwa Taifa. Nina hakika wakifanya hivyo watakuwa wametusaidia sana. Tunahitaji amani, tunahitaji vijana wenye mwelekeo, wenye kufanya kazi kwa kuwajibika, siyo kuzurura, kutangatanga, wanakuwa kama wajinga wajinga, wanakuwa wadokozi, hatimaye wanaingia kwenye ujambazi.

Baada ya kusema hayo hebu niongee juu ya akinamama kwa sababu ndiyo walionifikisha hapa. Akinamama wa Singida ndiyo walionipa hili jukwaa hili hapa, lazima nizungumze. Akina mama wa leo sio akina mama wa jana. Wameshaondoka kwenye miradi midogo midogo, hawahitaji tena mikopo ya shilingi 50,000/= au laki moja, wameenda kwenye miradi mikubwa mikubwa, wanahitaji mitaji mikubwa. Kwa nini Serikali isiwawezeshe? (*Makofi*)

Mheshimiwa Rais aliyeng'atuka, aliagiza Halmashauri zote ziwe zinatenga mfuko huu kwa ajili ya akina mama. Lakini mara ilipofutwa vyanzo nya mapato vingine mapato ya Halmashauri yamekuwa madogo. Lakini Serikali inatoa ruzuku ya fidia kwa nini Halmashauri haichukui ruzuku ya fidia ikakata asilimia 10 hapo na asilimia 5 kufidia ili akina mama waweze kupata fedha za kukopeshwa. (*Makofi*)

Ninaomba Serikali iwaambie hilo bado wanaendelea kutenga kuptitia mapato ya Halmashauri, wanasahau kwamba ruzuku ya fidia nayo inahusika. Nina hakika akina mama wakiwezesha Taifa hili litasonga mbele. Akina mama hawana utani. Wana mkakati wa kutosha wa kupambana na suala zima la MKUKUTA. Sasa wanachohitaji ni uwezeshwaji tu na vile vile Serikali nayo huwa inatoa milioni 4 kila mwaka kwa ajili ya mfuko huu wa akina mama. Hivi jamani milioni 4 ni kitu gani kwa karne hii ya leo. Milioni 4 watakopeshwa gharama vikundi vinne. Je, hivyo vikundi 500 nya Mkoa wa Singida na mikoa mingine nchi nzima, vipate wapi? (*Makofi*)

Tunaomba pia Serikali ihakikishe inaiwezesha Wizara ya Maendeleo ya Jamii ili iweze kuwasaidia akina mama kwa nini Wizara hii kila mwaka ni ya mwisho kwenye bajeti. Wizara nyeti, yenye kutumikia watu wengi akina mama, vijana, watoto, wazee nani atawahudumia kama bajeti hii kama kila mwaka watapangiwa ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba bajeti ya Maendeleo ya Jamii itiliwe maanani ili akina mama waweze kukopeshwa na siyo kukopeshwa tu hata elimu akina mama hawana. Wanabubiri mpaka Wabunge wafanye ziara wawaelimishe. Kwa sababu Wabunge wanatembea na Maafisa wa Maendeleo ya Jamii. Hivi kweli elimu ya dakika tano Afisa Maendeleo anapewa dakika tano na Mbunge aongee hivi atatoa elimu pale. Wawezesheni Maafisa Maendeleo ya Jamii ili waweze kuwawezesha akina mama. Huwezi ukaendesha biashara yoyote, mradi wowote bila elimu. Wanahitaji elimu, wanahitaji kubuni miradi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nina hakika kwa hili Serikali itakuwa imesikia. Ni matumaini ya wanawake wa Singida na Taifa zima kwamba sasa Serikali itawapa mitaji mikubwa kama azma ya Rais wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuongea hayo, naomba nirudie suala la barabara. Barabara ya Dodoma-Manyoni. Manyoni-Singida. Hivi ujenzi wa barabara hizi ni viini macho? Tatizo liko wapi? Watu walisaini mkataba, Mheshimiwa Waziri alitualika, mikoa mingi tu tukahudhuria wakati wanasaini mkataba, akasema mkondarasi

ambaye hatawajibika hatamaliza kwa mkataba, atapelekwa Mahakamani. Kawapeleka wangapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *KONOIKE* ile pale, iko nyuma ya miezi 16 mbona haijafika Mahakamani? *SIETKO* ile pale iko nyuma ya 16 mbona Mahakamani haijafika? Mnawakatisha tamaa Watanzania. Wana imani sana na Serikali yao. Wakandarasi wababaishaji tuwaondoe, tuna maslahi gani nao?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini Serikali imewachukua kwa malengo mazuri tu, lakini kama wamefika mahali wameshindwa wakae pemberi ili tupate wakondarasi watakaomalizia barabara zetu kwa wakati muafaka. *Sietco* ndiyo kabisa, mara wasimame, mara wabadili ma-*Engineer*. Mara sijui kifaa gani kimeharibika, hivi watabadili mpaka lini? (*Makofi*)

Nina hakika kuwa hili Serikali itakuwa imesikia, wananchi wa Mkoa wa Singida wana uchu kweli kweli na barabara za lami. Na sisi tutembee kama mikoa mingine inavyokwenda.

Baada ya kusema hilo naomba niongee kuhusu ruzuku za fidia. Utakuta Halmashauri inaomba pesa kulingana na mahitaji yao ama kulingana na pesa walizozikosa baada ya kodi kufutwa. Halmashauri inaomba shilingi milioni 800 inaletewa milioni 400. Hivi kweli huo ni ubinadamu? Mtu kaomba shilingi 800 milioni unampelekea shilingi milioni 400 afanyie nini. Matokeo yake ndiyo unampa kishawishi anafanya mambo mengine anakuja kukuambia kwamba pesa tulioletewa ni ndogo. Bajeti kubwa ni safari Dar es Salaam-Dodoma wapi. Si hela ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba basi Serikali ianze kutoa fedha za fidia kama ilivyoomba Halmashauri, na siyo hivyo tu hata pesa hizi za miradi mbalimbali zinapelekwa kwa kuchelewa. Pesa zinapelekwa Desemba, wakati watu wanafunga mahesabu. Pesa hizo matokeo hazifanyiwi kazi, zinafanyiwa mwaka mwingine. Sasa si umeshawachelewesa Halmashauri hiyo. Ingepata na mwaka mwingine ruzuku nyingine lakini sasa imekuwa tatizo kwa sababu ruzuku iliyopewa mwaka taarifa hamna. Ninaomba tuende sambamba na kalenda ya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee suala la maji. Singida miaka miwili iliyopita tulipewa mradi wa maji yalitoka bwawa la Itamka mpaka Singida Mjini. Bwawa lile tumeliimba kwa miaka mitatu, kila mwaka nikisimama naongea hilo suala mpaka leo hii ni kiini macho. Tatizo liko wapi kwa wana Singida? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiuliza watu wanapata vigugumizi, mara ooh! Tumesitisha, maji yana matatizo, yana chumvi nyingi. Maji hayatoshi, hivi wakati wanafanya utafiti haya yote hayakuwepo, kwa nini watafiti hawakuyaona hayo. Tunaomba basi ufanywe ufumbuzi kwa hiyo, mtafute mbini ya kutuletea maji wana Singida Mjini tuache tabia ya kupata maji kwa mgao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee suala la mishahara. Naishukuru sana Serikali imeongeza mishahara lakini kima cha chini tutakipandisha zaidi, maana kuna tabia ya kusema kwamba aliye nacho ndiye anayeongezewa. Tuwajali zaidi wale watumishi wa chini. Ndiyo wanaohangaika, wanamalizia mishahara yao kwenye daladala. Ikifika mwisho wa mwezi anapokea hela yote inaingia kwenye madeni. Unakuta *TRA* watu wanapata mamilioni. Sijui *TANROADS* mamilioni eti kisa wanashika pesa. Kushika pesa ukampa mshahara mkubwa siyo tiba, kama aliumbwaa mwizi ni mwizi tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata ukamkabidhi kitu kikubwa, atadokoa tu. Kwa hiyo tuende sambamba kwa wafanya kazi wote wapate haki zao za msingi kila mmoja anastahili haki na kila kazi ina umuhimu wake. Hakuna kazi bora kuliko nyingine, wote tunategemeana. (*Makofi*)

Niongelee suala la hospitali ya Mkoa wa Singida. Hospitali yetu ilijengwa mjini eneo dogo na msongamano wa watu ni mkubwa wa wagonjwa kwa sababu Wilaya ya Singida haina hospitali. Sasa Mkoa tayari ilishaona umuhimu wa kuipanua hospitali, Kituo cha Afya cha Sokoine tumeomba shilingi milioni 110, tunaomba tupewe tuweze kuipanua kituo chetu cha Afya ili msongamano wa wagonjwa katika hospitali ya Mkoa upungue.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba mtufikirie jamani na sisi tuende sambamba na Mikoa ambayo imeshapiga hatua. Kinachowezekana kisingoje kesho jamani, mbona vitu vingine viko chini ya uwezo wa Serikali? Nina hakika kwa hili Mheshimiwa Waziri Mkuu amenitazama kwa uchungu mkubwa, litafanyika kesho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee suala la *TACAIDS*, jamani semina zinatosha, tumeshapewa semina za kutosha, sasa pesa ziende kwa walengwa, waathirika wapewe dawa za kuongeza maisha, waathirika wapewe lishe. Tuachane na Semina hazitufikishi popote. Ni matumizi mabovu ya pesa. Na walengwa walio wengi wapo vijijini, hata namna ya kupata huduma hii hawajui. Ninaomba taratibu zifanyike walengwa wapatikane kwa majina ili muweze kuwafikia muape lishe jamani, wanahitaji kuishi wale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine wana mawazo tu, familia zinawategemea vizuri tu. Sasa tunapowaacha wanaendelea kwisha, mwishowe tutawapoteza. Nina hakika tukiwajali hawa watu siku zao zitaongezeka. Naomba niongelee kuhusu suala la vituo vya watoto waliokuwa wanaishi kwenye mazingira mabovu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwanza ninaomba niwashukuru sana kwa kazi tuliyofanya kwa siku ya leo. Lakini ninapenda kuwafahamisha kwamba hii hotuba ya Waziri Mkuu, wadau wakuu ni Wakuu wa Mikoa wapo hapa. Tutakuwa nao nadhani mpaka mwisho wa Bajeti hii. Kwa hiyo, nimeona watu wameleta orodha

nitawataja wengine na wengine nitawasahau. Lakini Wakuu wa Mikoa wanahitajika kuwepo hapa. Kwa hiyo, mtawaona wamekaa katika *Speaker's Lounge* pale.

Baada ya kusema hayo, kesho asubuhi atakuwa kwenye kiti, Mwenyekiti, Mheshimiwa Jenista Mhagama. Keshokutwa asubuhi atakuwa kwenye kiti, Mwenyekiti, Mheshimiwa Job Ndugai. Kwa hiyo, ninaomba sasa kuahirisha Kikao mpaka kesho saa tatu asubuhi. (*Makofi*)

(*Saa 01.45 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumanne tarehe 27 Juni, 2006 saa tatu asubuhi*)